Wale Wanawali Kumi, Na Wayahudi Mia Na Arobaini Na Nne Elfu

Habari za asubuhi. Ni furaha sana kuwa hapa tena asubuhi ya leo katika huduma ya Bwana. Hali mbaya ya hewa huko nje, bali, loo, ndani ni kuzuri sana. Huu ni wakati mmoja tunaoweza kusema ni vizuri kuwa ndani ukiangalia nje (sivyo?) . . . kuwa nje ukiangalia ndani.

2 Nilikuwa na mapumziko mazuri jana usiku na ninajisikia vizuri zaidi asubuhi ya leo. Nasi tulikuwa na wakati mzuri sana jana usiku, sivyo? Wakati mzuri tu! Nami ninathamini hilo. Tumekuwa . . . ibada ilionekana ni kama moja ya zile tulizokuwa nazo huko Shreveport, karibu tu ni mwe—mwendeleo wa kufuatwa kwa Roho akienda moja kwa moja. Uh-hum. Kwa hiyo tuna furaha sana na tunamshuruku sana Mungu kwa wema Wake na rehema, na kwa ninii yenu . . . ninyi watu mkimtolea roho zenu katika ushirikiano kusudi apate kutuongoza na kutuelekeza.

3 Mnaona, kama una wasikilizaji wanaopinga, Roho Mtakatifu hata hatafunua. Inawabidi kuwa na kitu fulani, kule kufanya kazi pamoja. "Walikuwa mahali pamoja na nia moja," ndipo ikaja sauti kutoka Mbinguni ikienda kasi. Mnaona. Lakini mnaponinii . . . Haidhuru nitaomba jinsi gani, na kukesha usiku na mchana nikisoma na kuomba mbele za Bwana, nishuke nije huku, labda upako ukiwapo juu yangu, niingie hapa na kuhisi hiyo chuki, mnaona, Yeye—Yeye ananinii tu . . . linamhuzunisha mara moja, hatafunua chochote. Bali unaposhuka kuja hapa chini ya upako na kuhisi wasikilizaji wako chini ya upako, hapo ndipo Roho Mtakatifu huanza kufanya kazi basi, Naye anaanza kujongea na kutufanyia mambo makuu. Kwa hiyo, mnaona?

4 Sijazungumza na mchungaji bado kuhusu . . . Nilisikia *Amini Tu* na kwa hiyo nikaingia upesi na kuona—kuona kile alichokuwa . . . alikuwa amepanga asubuhi ya leo. Sasa, Ndugu Neville, nitakwambia nini, nitaanza na hili darasa dogo na kama nikimaliza yapata saa tano, sawa, wewe chukua nafasi hiyo na uanze kuhubiri. Vipi kuhusu hilo? [Ndugu Neville anasema, "Naam, usikatize upako hata kidogo, endelea tu mbele."—Mh.] Loo, ninaamini upako hapa nyuma, pia, upako hapa nyuma pia. Yeye ni . . .

5 Ndugu Neville sikuzote ameninii. . .Kwa wageni hapa wasiokuwapo hapa awali, yeye ni (sio kusema hivi usoni mwake, bali) ni mtu mwema, amekuwa hivyo sikuzote. Sikuzote yeye husoma hilo—hilo. . .huyaishi hayo Maandiko, “kumtanguliza mwenzako,” sikuzote katika Kristo na sikuzote *anawatanguliza*. Na tangu nilipomjua amekuwa hivyo; sio wakati tu amekuwa hapa maskanini, bali tangu nilipomjua na hiyo imekuwa ni miaka mingi iliyopita. Mara ya kwanza ninaamini nilipopata kukumbuka kumwona Ndugu Neville, kumjua, nilienda kumsikiliza akihubiri wakati mmoja huko chini kwenye kanisa la Methodisti, yeye. . .huko chini Howard Park, miaka mingi, mingi iliyopita. Imekuwa, nadhani, miaka ishirini (nadhani) iliyopita ama zaidi tangu nilipomjua. Ndipo yeye. . .naye alikuwa. . .alifanya kazi, pia, yeye ni. . .Loo, nadhani, mpaka hivi karibuni, sikuzote amefanya kazi kule kwenye shirika la misitu na kadhalika huko, Henrysville, ambako anatoka; na kufanya kazi kujipatia riziki, akihubiri kwa ziada. Jinsi nimefanya maishani mwangu, pia, mpaka hivi majuzi, ndipo tukafikia ambapo tusingefanya jambo lingine lolote ila hili. Kwa hiyo ninashukuru kwa jambo hilo. Ninashukuru kwa ajili ya Bosi wetu mpya, sivyo, Ndugu Neville? Naam, bwana! Hakika napenda Hilo. Naam, bwana. Nimeridhika sana Naye!

6 Na sasa naamini wataachana na madarasa ya shule ya Jumapili. Naam. Darasa la Jumapili la watoto, wataliacha kwa kuwa chumba ni. . .wameondoa mgawanyo, kwa hiyo inalifanya tu kanisa kupanuka mpaka huko nyuma.

7 Sasa, usiku wa leo tutakuwa na ule wakati wa mwisho mashuhuri wa huu, Laodikia. Na jana usiku tulichukua wakati wa Filadelfia na tukafikia mwanzoni mwa wakati wa Laodikia na kule kuingiana. Na halafu hizo siri kuu ambazo Mungu alianza kutufunulia katikati ya nyakati hizo, “Mlango uliofunguliwa,” na “nguvu kidogo,” “kulishika Neno Langu,” “mna Jina Langu.” Vitu hivyo vyote vidogo humo, jinsi ambavyo Mungu alivifanya halisi kwetu, ambalo tunashukuru sana, sana.

8 Wala msisahau, kukiwapo na wageni wowote miongoni mwetu walio na watu wagonjwa, tutakuwa na maombi kwa ajili ya wagonjwa Jumapili ijayo, juma moja kutoka leo. Na hiyo itaninii. . .Bwana akipenda. Na hiyo itakuwa. . .Je, sikuzote mnaona jinsi ninavyopenda kuliweka hilo, “Bwana akipenda”? Biblia inasema tufanye hivyo, “Bwana akipenda.” Hatujui bado; kamwe hajapata kuniambia ya kwamba nitakuwa hapa, na kanisa litakuwa hapa, nasi sote tungekuwa hapa, ama lolote zaidi. Basi yakiwa ni mapenzi Yake, tutakuwa hapa, mnaona. Yakiwa si mapenzi Yake, bila shaka, hatutakuwako.

9 Ndugu Neville ataendelea kutangaza kwenye matangazo yake, na watu mbalimbali, nadhani, ndugu huyu hapa na wale walio na matangazo. Na halafu mje mapema mwezavyo Jumapili asubuhi, maana tunatarajia umati mkubwa kama

huu wa kuombewa, nasi tunataka kuingia. Tutaninii...vema, hebu tuone, mimi...Kama kuna umati mkubwa kama huu, daima ni bora zaidi kuwa na kadi za maombi kwa maana wanasongamana sana, mnaninii tu...mmoja akimsukuma mwenziwe na vitu kama hivyo. Nafikiri kama mkilifanya tu kwa utaratibu kusudi waje tu mmoja mmoja inalifanya... inapunguza kuchanganyikiwa miongoni mwa watu, mwajua.

10 Na—na basi ninii tu...Na hata haikubidi kusimama mpaka kadi yako iitwe. Keti tu mahali ulipo ikiwa wewe ni mgonjwa na unasikia vibaya, wala haitakubidi kusimama kwenye mstari mrefu. Wakati tu kadi yako imeitwa, njoo tu papa hapa juu ukaombewe kisha ushuke chini, na mwingine aje, namna hiyo. Ninapenda hilo vizuri zaidi. Kwa kawaida mimi huwaagiza wavulana hao kuweka kiti, kama mtu akisikia vibaya wakati wakingojea, nikiita wachache kwa wakati mmoja; wanasikia vibaya, mbona, acha—acha wangoje hapo kitini mwao mpaka... ama kuketi kitini mpaka namba yao iitwe, mpaka wanapoweza kuombewa.

11 Nami ninaamini katika uponyaji wa Kiungu; ni moja ya mafundisho makuu ya Biblia. Lakini uponyaji wa Kiungu una mengi kwake zaidi ya kuwa tu uponyaji wa Kiungu. Uponyaji wa Kiungu unasema tu ya kwamba "kuna Mungu anayekuja tena." Uponyaji wa Kiungu unanena juu ya nini? Ni arabuni ya ufufuo wetu. Ikiwa hakuna uponyaji wa Kiungu basi hakuna ufufuo, mnaona. Na ikiwa hakuna Roho Mtakatifu sasa kutubatiza, hakuna Uzima wa Milele katika ulimwengu ujao. Biblia ilisema, "Hii ni arabuni ya wokovu wetu." Nanyi mnajua *arabuni* ni nini? Ni "malipo ya kwanza," mnaona. Ukishuka uende na kulipa...Tuseme ulinunua shamba, walitaka dola elfu kumi kwa ajili yake, nawe ukalipa elfu mbili, hizo ni pesa zako za "arabuni," wanaziita arabuni yake. Sasa, kama ubatizo huu wa Roho Mtakatifu ni arabuni tu ya yale yajayo, loo, itakuwaje wakati sisi—wakati tutakapopata bei kamili? Litakuwa tukufu!

12 Sasa, asubuhi ya leo tutajaribu kufunganisha, Bwana akipenda, baadhi ya mambo hayo, ya...kati ya nyakati za kanisa (hizi papa *hapa* ndani) kuna kitu kinachoingia. *Wale Mia na Arobaini na Nne Elfu, Wale Masalia, Wale Wanawali Waliolala, Wale Wanawali Wenye Busara,* na *Kutiwa Muhuri na Roho Mtakatifu, Kutiwa Alama ya Mnyama,* mambo hayo yote kuninii tu...Ni mwisho wa wakati, na kila kitu kinaangukia papa hapa ndani mahali pamoja, kwa hiyo basi inatupasa kuuchukua msimu wote uliosalia wa baridi kali kulielezea hili, bali sisi...kukipata Kitabu cha Ufunuo, tuone jinsi kinavyofungamana pamoja.

13 Ulipata kuona? Ustaarabu umesafiri vile vile, Bw. Wood. Ni...Hili, mwanadamu ana hisi zile zile, ana hisi sita, ama hisi tano, hasa, ambazo amekuwa nazo tangu—tangu alipokuja duniani miaka elfu sita iliyopita. Lakini papa hapa katika miaka

ya mwisho, ile michache ya mwisho, mia moja iliyopita... Jamani! Yeye amekuja, kule nyuma, akisogea polepole katika gari la maksai. Lakini kutoka kwa hilo gari la maksai, katika miaka mia moja iliyopita, ametoka kwenye gari la maksai hadi kwenye ro—roketi inayoruka karibu maili elfu mbili kwa saa. Hivyo ndivyo ameamka upesi mno, kutoka kwenye gari la maksai hadi kwenye roketi. Pia, angalia, imekuwa tu ni miaka michache iliyopita, mbona, ningesema si zaidi ya miaka hamsini iliyopita.

14 Nilipokuwa mvulana mdogo hapa juu katika Utica Pike, walikuwa na ninii ya kale...kulikuwako na jamaa jina lake Elmer Frank aliyekuwa akiishi huku. Yeye kwa namna fulani ni wakili wa sheria. Alimwoa maskini msichana mmoja huko juu barabarani ambaye baba yangu alimfanyia kazi ba—baba yake, jina lake lilikuwa ni Lusher. Nao...naye alikuwa na ninii, namna fulani ya motokaa; ilikuwa na hendeli, unatoka kando yake na kuzungusha namna *hii*, nayo ilikuwa na gia moja tu. Nawe ulikuwa na kitu ki—kikubwa cha raba kwa ajili ya honi, nawe ungekipiga namna *hiyo*. Nao walisema, "Kitu hicho kingeenda mwendo wa kasi mno wa maili kumi na tisa kwa saa." Sasa, Papa alishuka akaenda akapakia mchanga kwenye behewa, na ku—na kuupandisha pale juu na kuupakia katika magunia apate kukishikilia, aone kama kweli kingeweza kwenda mwendo wa maili kumi na tisa kwa saa. Mnaona? Lakini laiti ungaliziona hizo barabara, uh-huh; kingeenda tu yapata kumi *hivi*, na tisa juu chini *huku*. Mnaona? Kwa hiyo ukiziweka pamoja, unapata maili kumi na tisa kwa saa.

15 Ninakumbuka sisi sote watoto, Mama angetuogesha sote, yapata sisi watano, tungening'inia kwenye ua huo kukisikia. Tungekisikia kikija, umbali wa maili kadhaa, huku chini kabisa, kikinguruma, nguruma, nguruma, nguruma. Kila mtu angesimama na kuwachukua farasi wao, nami natoa mkokoteni, na kuwashikilia namna *hii*, mwajua. Kitu hicho kikipanda kuja barabarani, jamani, kilikuwa ni kitu cha kushangaza sana. Na—nami nawazia tu, hiyo ilikuwa ni huko nyuma, nilikuwa na umri wa yapata miaka saba, mnaona. Jinsi...Hiyo ilikuwa yapata mwaka wa 1914, na basi wazieni tu jinsi mambo yamebadilika tangu wakati huo. Basi angalieni, na imekuwa tu ni miaka arobaini iliyopita ama kitu fulani. Basi, angalieni, yeye alikuwa na miaka elfu sita kufanya hayo yote pamoja na haya papa hapa, kwa sababu Biblia ilisema ya kwamba angefanya hivyo, "Siku za mwisho, watakimbia huku na huku, na maarifa yataongezeka."

16 Hivi mliweza kuwazia juu ya Nahumu, wakati a—alipoona barabara ya Outer Drive huko Chicago, miaka elfu nne iliyopita? Hivi... Yeye alisema, "Yangesongamana katika barabara pana." Sasa ninii...Nimekuwa katika nchi za kale ambako walikuwa na... barabara zao kama vile katika Oslo na mahali mbalimbali, ni vigumu kupata nafasi ya kutembelea, ni kubwa tu kutoshea ga—gari la farasi kupitia katika miji yao. Lakini labda umbali

ungekuwa kama kutoka hapa mpaka kwenye ukuta ule, huo ndio ulikuwa upana wa barabara zao, pana tu vya kutosha kwa gari la farasi kupitia barabara hiyo. Vema, mnaona, Nahumu alisema, "Zilikuwa barabara pana." Kisha kasema, "Yangekimbia kama umeme," magari haya. "Na yangeonekana kama mienge," hizo ni taa zao. Tena kasema, "Zingegongana moja na jingine," ajali za barabarani. Nabii huyo aliinuliwa juu ya wakati huo na kuangalia huko mbali, miaka elfu nne, na kuona hayo yakija. Wazieni hilo! Uh-hum. Uvuvio.

17 Bali tuko kwenye wakati wa mwisho, enyi marafiki. Ni ninii tu . . . Na vivyo hivyo na Maandiko, kwa kuwa mambo haya yote yanatukia, Maandiko yote yamewekwa mumu humu ndani katika wakati huu wa mwisho papa hapa. Nami niliwazia, asubuhi ya leo, kama Mungu angetusaidia, tungeyafunganisha haya, baadhi ya mambo haya, kadiri tuwezavyo. Halafu usiku wa leo ule wakati mkuu wa mwisho, wa kanisa la Laodikia, jinsi unavyopokea Ujumbe wake na kisha unaenda kombo na kupuuza Ujumbe wake, moja kwa moja unaingia katika hali ya uvuguvugu ambao Mungu anautapika kutoka kinywani Mwake. Mnaona, kwa maneno mengine, linamfanya achefuke tumboni Mwake hata kuwazia juu ya hilo. "Nitakutapika kutoka kinywani Mwangu," Akasema.

18 Sasa, nina baadhi ya Maandiko yaliyoandikwa hapa ambayo ningetaka kuyarejea asubuhi ya leo. Bali nashangaa kama lingekuwa ni jambo gumu sana kwetu, kwa dakika moja tu, kusimama kwa ajili ya maombi:

19 Baba yetu wa Mbinguni mwenye rehema, tunapokuja tena asubuhi ya leo kwenye siku hii ya Sabato. Na huko nje, mvua zimeanza kunyesha, na upepo wenye baridi kama barafu ukivuma; bali tunashukuru sana kwamba tuna paa juu ya vichwa vyetu leo hii, kwamba tuna mahali padogo, na tungali taifa ambapo tunaweza kuja na kumwabudu Mungu kwa njia yoyote ambayo dhamiri yetu inatwambia tuabudie.

20 Halafu tunaona katika Neno Lako ya kwamba hili halitadumu muda mrefu sana, kwa hiyo, Baba, tunaomba ya kwamba utatutia mafuta sana sana leo hii kusudi tupate yaliyo mazuri sana kutoka kwenye hili yaliyopo kwetu kupata, na tuwe tayari kwa ajili ya majira yaliyo mbele ambapo hatutaweza kufanya hivi. Hatujui ni muda gani zaidi, huenda ikawa ni majuma, miezi, ama miaka, hatujui, bali wakati fulani hatutaweza kufanya hivi. Kwa hiyo tunaomba, Baba, ya kwamba utatuweka chini ya uongozi Wako wa Kiungu, na jalia mawazo yetu yawe juu Yako, na tafakari za moyo wetu zikubalike mbele Zako, Ee Bwana.

21 Samehe dhambi zetu. Tunaomba hayo tunapoziungama Kwako, kwamba tumetenda dhambi na kuikosa ile Njia. Nasi hatustahili kuitwa Wako, ila tu tufanye vibarua Wako, Bwana.

Nasi tutakuwa tayari kufanya lolote utakalotwambia tufanye, kazi yoyote iliyowekwa juu yetu. Tuko tayari kuifanya, ila tu utupokee katika Ufalme Wako, Bwana; tupate kufanya kazi katika majira haya ya kutisha sana, yanayoukabili ulimwengu.

22 Tubariki sasa kwa Uwepo Wako, tufundishe kwa Roho Wako Mtakatifu, na ujipatie utukufu kutokana na kuwapo kwetu hapa pamoja. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

23 Sasa ningetaka, kwanza, ningetaka kumtambua kila mmoja wa marafiki zangu hapa, nimekuwa nikiwaona hapa asubuhi ya leo. Ni vigumu sana hapa wakati wa usiku, taa zetu ziko huko nyuma mahali pale panaponing'inia chini wala haziwamuliki watu. Na kwa namna fulani ni vigumu kuona kutoka kwenye mimbara hii usiku hapa, na pia mchana. Ninawaona wengi wa marafiki zetu kutoka sehemu mbalimbali nchini, ambao ninaweza kuwatambua vizuri zaidi leo kuliko vile ningeweza usiku. Na wangekuwa ni wengi sana kuwataja wote, bali ninataka mjue ya kwamba bila shaka ninawathamini. Na baada ya huku kukata-kata sana kwote na kadhalika, ambako imenilazimu kufanya katika Maandiko, kufanya. . .kuileta ile Kweli. Si kile nilichotaka kufanya, bali yale Mungu aliyoandika hapa yafanywe, mnaona. Halafu hicho Ndicho. Na hata hivyo ninawaona wengi wa ndugu zangu ambao ni wafuasi wa madhehebu na kadhalika, wameketi papa hapa pamoja nami bado, kwa hiyo ninawathamini sana, sana. Ninyi. . .Mungu awabariki daima na awasaidie ndilo ombi langu.

24 Na sasa. . .[Ndugu Stricker anasema, "Ndugu Branham?"—Mh.] Naam, ndugu. ["Kama ninaweza kuwa na ruhusa ya kanisa kuzungumza kwa niaba ya watu wote hapa, tunakutaka ujue ya kwamba tunakuthamini."] Asante, Ndugu Stricker. ["Na tunakupenda."] Asante, Ndugu Stricker. ["Nasi tunaomba neema upate kupitia mambo ambayo huenda ikakubidi kuyapitia, ili tuweze kusimama karibu nawe."] Asante, Ndugu Stricker. [Kusanyiko linasema, "Amina!"] Asanteni, kanisa, hayo ni mazuri sana kwenu kusema hivyo. Ninayathamini hayo sana.

25 Mtu fulani alikuwa akisema jana usiku kuhusu. . . Ninaamini ilikuwa ni Ndugu Fred ambaye alinipigia simu na kusema kuhusu ono ama ndoto ambayo ndugu fulani alikuwa nayo, ambayo aliisimulia kabla tu ya kuondoka jana usiku, akaniona nimesimama kwenye ncha ya dunia na wingu jeusi likibingirika kunifuata. Ninajua ananiwinda. Bali huyo. . . mradi tu. . .ha—hataweza kulifanya mpaka Mungu amemaliza, ndipo basi—basi mimi—mimi. . .wakati wangu wa kwenda umewadia basi. Kwa hiyo. . .

26 Lakini na—nafikiri juu ya hili, "kutokuwa mkuu kamwe." La, sitaki kuwa, mnaona. Ila ninawazia juu ya *Zaburi ya Maisha:*

Maisha ya watu mashuhuri yote hutukumbusha (Mnaona, yale Paulo aliyofanya, yale Ireneo aliyofanya, yale Luther aliyofanya, yale Wesley aliyofanya, ama yale Mtakatifu Martin aliyofanya, na yale waliyofanya.)

Na maisha ya watu mashuhuri yote hutukumbusha
Ya kwamba tunaweza kuyafanya maisha yetu adhimu,
Tunapoachana, tunaacha nyuma yetu
Kumbukumbu za kudumu;

Kumbukumbu, ambazo labda mwingine,
Wakati akiabiri kwenye bahari taadhima ya maisha,
(Kwa kuwa baada ya kuondoka kwangu, mnaona, na nimewaacha.) Ndugu mpweke aliyepata maangamizi (hebu chukueni kimoja cha vitabu hivi mkisome),
Akiona, atatiwa moyo tena. (Jambo ndilo hilo.)

Hima tuamke, basi, na tuingie kazini;
Tukiwa na moyo kwa ajili ya wowote . . . mvutano, (napenda hilo, nanyi je?)
Msiwe kama ng'ombe bubu, wanaosukumwa (inawabidi kusukumwa kwake);
Bali uwe shujaa katika mvutano! (Na—napenda hilo.)

27 Sasa, maskini ndugu yetu, George, alikuwa na lile alilolipenda; nilikuwa nalo kwenye ibada yake ya mazishi. Tumetumia . . . Ningeketi na kunukuu *Zaburi ya Maisha,* mwajua, naye angeketi na kunukuu *Kupita Kizuizi*. Mnaona? Nanyi mmelisikia hilo:

Machweo ya jua na nyota ya jioni,
Na wito mmoja dhahiri kwangu!
Na jalia kusiweko na maombolezo kwenye kizuizi,
Nitakapoingia baharini. (Mmelisikia mara nyingi.)

Kwa kuwa wote walio nje wamesogezwa kwa wakati na nafasi,
Mafuriko yanaweza kunipeleka mbali,
Bali ninatumaini kumwona Nahodha wangu uso kwa uso
Wakati nimepita kizuizi. (Nina hakika alifanya hivyo alipoaga dunia.)

28 Na kwa hiyo . . . halafu langu ni:

Kuachana huacha nyuma yangu
Kumbukumbu za kudumu,
Kusudi wengine, wakiona, wanaweza kufuata,
Wajipe moyo na wazidi kuendelea.

29 Kwa maana, siku moja kuu Yesu atakuja (na hilo ndilo tutakalosoma asubuhi ya leo), yote yatakuwa yamekwisha wakati huo.

30 Sasa, niliwazia asubuhi ya leo, kusudi tusiweze katika jumbe hizi za kanisa . . . Sasa, labda, Bwana akipenda, hivi karibuni, huenda nikafanya mfululizo mwingine mdogo wa mikutano juu ya *Kanisa la Kweli na la Uongo,* kote kote kutoka Mwanzo, tulifuatilie kwenye Biblia na tutalipitisha kote hadi Ufunuo. Makanisa yote mawili, vile tu yatakavyofanya. Halafu basi labda siku moja wakati sisi . . . Bwana akipenda, tutalijenga kanisa kusudi mpate nafasi zaidi kidogo ya kuketi . . . Mngeshangaa ni wangapi wamepiga simu na kusema hivyo; wanapita tu hapa kwa magari na kuona lote limejaa, kwa hiyo wanaendelea tu, mnaona. Na kwa hiyo wao . . . hatuna nafasi.

31 Na labda kama kia- . . . wakati wa kiangazi wakati ni joto ama kingine, ambapo tunapata ukumbi wa michezo wa shule ya upili ama chochote kile, itakuwa vema, tuchukue Kitabu cha Ufunuo basi, ama kitu fulani, ama Kitabu cha Danieli na Ufunuo, na kuvifunganisha pamoja ili tuweze kuwa nao.

32 Sasa, hatukufikia kuwashughulikia Wayahudi. Wayahudi walikuwa . . .

33 Sasa, kama nilivyosema, katika—katika Wakati wa Giza wa 1500, ukasisi wa Katoliki, wakati walipokuwa wakijiimarisha, wakaliunganisha kanisa na taifa, hiyo ilikuwa ni "baada ya utawala wa miaka elfu." Walidhani walikuwa—walikuwa kabisa kwenye ule Utawala wa Miaka Elfu kwa sababu kanisa lilikuwa limempokea halifa wake, mmoja kama Kristo kuketi juu ya kiti cha enzi. Nalo lingeunganisha kanisa na taifa, yote yalikuwa ni shwari, ya kwamba "Utawala wa Miaka Elfu ulikuwa umeanza." Wangali wanaamini hilo. Lakini hilo ni kosa. Kwa sababu Utawala wa Miaka Elfu hauwezi kuja, hauwezi kuanza, bila ya kuja kwa Kristo.

34 Kristo anauleta Utawala wa Miaka Elfu, Yeye ndiye Mwana wa ufanisi; na Yeye atakapokuja, basi kutakuwako na miaka elfu. Na itakapotimia, kutakuwako na Unyakuo wa Kanisa litapaa juu, halafu kurudi kwa Kristo. Basi kumbukeni sasa, wakati . . . Kwa kuwa ni jambo gani lingine tunalotarajia? Kunyakuliwa kwa Kanisa.

35 Sasa, msichanganye Kunyakuliwa kwa Kanisa na Hukumu ya Kiti Cheupe cha Enzi. Kwa sababu, Kunyakuliwa kwa Kanisa, hakuna hukumu, mnaona, tayari umekutana nayo papa hapa chini. Hiyo ni kweli, "Kwa kuwa wale walio ndani ya Kristo wako huru na hukumu." Yesu alisema, "Yeye ayasikiaye Maneno

Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna Uzima wa Milele wala hataingia hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani."

36 Tunafanya hivyo vipi? Tunaingia ndani ya Kristo na kubatizwa katika Mwili mmoja, Wakorintho wa Kwanza 12, "Mwili Mmoja." Tumebatizwa katika Mwili wa Yesu Kristo, na Mungu tayari ameuhukumu Mwili huo. Yeye asingeweza kutusimamisha hukumuni tena, kwa sababu tayari ameuhukumu Mwili huo. Na kwa ruhusa na neema ya Kristo Yeye anatuleta kwake Mwenyewe, Wakorintho wa Kwanza 12, "Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja, na ni huru na hukumu zote maana Yeye tayari amezistahimili hukumu." Loo, hivi hamna shukrani sana Kwake! Yeye alizichukua hukumu kwa ajili yetu. Hakuna hukumu tena! Bali wale wanaokataa kuingia ndani Yake, Mwili huo, ule Mwili wa siri . . . Tunaingiaje ndani Yake? Kwa kupeana mikono? La. Kwa barua? La. Kwa namna fulani ya ubatizo, maji? La. "Kwa Roho mmoja, Roho Mtakatifu, sisi sote tumebatizwa katika Mwili huo!"

37 Sasa kumbukeni, tutashughulikia hilo vikali asubuhi hii. Ama wewe uko ndani ya Mwili huo ama nje ya Mwili huo, hakuna cha kuwa katikati Yake. Hakuna Wakristo wema-wazuri. Wala—wala ninii . . . ama wewe ni Mkristo au si Mkristo. Hakuna ndege mweusi-mweupe, hakuna mtu mlevi-asiye mlevi. Huwezi kuwa naye. Ama wewe ni Mkristo au si Mkristo. Ama uko ndani ya Kristo au nje ya Kristo.

38 Sasa, huku kunaweza kukaonekana ni kufundisha, mimi si ninii . . . Niko mbali sana na kuwa mwalimu. Lakini kufundisha ni kukata-kata, hiyo ni karama maalum katika—katika Mwili wa Kristo. Kwanza kuna mitume, halafu manabii, halafu walimu, na wainjilisti, wachungaji; karama tano za huduma Mwilini. Na kufundisha ni moja ya karama za Roho. Sasa, inanibidi tu kuchukua kile ninaona ni kweli na kujaribu kukileta kwa watu, na kusoma na kuyaleta Maandiko pamoja. Sasa, bali ni katika Kristo pekee, Mwili wa Kristo unapaswa kutambuliwa.

39 Sasa, milango mitatu ya kwanza ya Ufunuo inashughulika na Kanisa. Mataifa, Wayahudi, Wahabeshi, Makaburu, kila namna ya watu ulimwenguni wanaenda kwa Mataifa kuufanyiza Mwili huu; mweusi, mzungu, wa hudhurungi, kila kitu, ni shada la maua, na hiyo ni kweli, ambayo Mungu huweka madhabahuni Mwake; na huo umetokana na mataifa yote, makabila, lugha, na watu.

40 Lakini, sasa, baada ya kuondoka kwenye mlango wa 3 (Nyakati za Kanisa hapa), Mungu anarudi na kuwachukua Wayahudi, Kanisa kamwe halionekani tena kwenye wakati huo. Ni Wayahudi. Na Mungu hawashughulikii Wayahudi kama

mtu binafsi, Yeye huwashughulikia Israeli kama taifa, daima kama taifa.

41 Hivyo ndivyo mtu fulani alivyolipata hivi majuzi. Nina—nina barua nyingi sana juu ya hilo, *Dini Chotara,* ambapo nilitoa tamshi juu yake katika . . . Biblia inasema ya kwamba mwana haramu, anayeitwa "mtoto haramu," hangeweza kuingia katika kusanyiko la Bwana kwa vizazi kumi, ambavyo vingekuwa ni miaka mia nne ambapo mwana haramu asingeweza kuingia kwenye kusanyiko la Bwana. Hivyo ndivyo huko kuchanganya mbegu kulivyokuwa kubaya; huyo alikuwa ni mwanamke ambaye alimwacha mwanamume mwingine aishi naye kusudi amzae mtoto, kwamba huyo mtoto alikuwa ni chotara, si kwa baba yake bali kwa mwanamume mwingine. Mnaona? Na hilo lilikuwa ni ovu sana mbele za Mungu, ilichukua vizazi kumi hata kuimalizia mbegu hiyo tena, mbele za Mungu.

42 Lakini hilo halitumiki kwa wakati huu. Mna Kuzaliwa upya sasa. Hawaninii . . . Walikuwa tu na kuzaliwa kumoja huko nyuma, huko kulikuwa ni kuzaliwa kwenyewe kwa kujuana kimwili. Tuna huku Kuzaliwa upya sasa ambako ni kwa kiroho, huko kunaondolea mbali takataka yote. Nasi ni viumbe vipya katika Kristo Yesu, tuliozaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu. Viumbe vipya! Juu ya neno *kiumbe*, kama baadhi yenu wanachuoni wazuri hapa mnaofahamu (Ikiwa hamfahamu, mnaweza kulichunguza.), hilo *kiumbe* linatokana na neno la Kiyunani la "uumbaji mpya." Loo, kama vile ulivyo kiumbe hapa, kilichozaliwa kwa kujuana kimwili; wewe ni kiumbe kipya basi, kilichozaliwa Kimbinguni. Kwa . . . katika uumbaji mpya wa Mungu wa mtu mpya. Uumbaji mpya, katika Kuzaliwa. Lakini hapana budi iwe ni kuzaliwa, kama tu vile kuzaliwa kwa kawaida kulivyo muhimu; Kuzaliwa kiroho ni muhimu vile vile kama kuzaliwa kwa kawaida.

43 Mume na mke vijana huenda wakafunga ndoa na kusema, "Mvulana wetu mdogo wa kwanza, tutamwita 'Yohana.'" Endapo hatazaliwa, Yohana kamwe hatakuwa hapa. Hivyo tu. Jambo lile lile, huenda wewe . . . ni mawazo mangapi ya uongo unayokusanya kuhusu Mbingu, jinsi ilivyo kuu, kama hujazaliwa mara ya pili hutakuwa kule. Hivyo tu, mnaona. Haina budi kuwa hivyo, maana haina budi kuwa ni Kuzaliwa. Mungu ameweka sheria Zake na kila kitu kinafanya kazi kulingana na sheria Zake. Mnaona?

44 Sasa, katika hizi, kuna masalia ya Wayahudi yatakayookolewa. Nasi tutawachukua kwanza, kwa maana linaweka . . . Sasa, sikuzote kuna matabaka matatu ya watu wakati wote, sikuzote. Basi wekeni . . . yawekeni niani mwenu, hayo ni: mwa—mwaminio, anayejifanya mwaminio, na asiyeamini. Hayo yote matatu. Pia kuna Myahudi, ambaye ametupwa nje kusudi tupate nafasi; kuna kanisa vuguvugu; na kuna Kanisa lililojazwa na Roho.

45 Wakati mmoja, Charlie Bohanon alikuwa rais wa ninii . . . ama msimamizi wa wilaya za kusini za Kampuni ya Utumishi wa Umma, nilipowafanyia kazi. Nilikuwa tu nikiyasoma Maandiko wakati huo, kama mvulana. Naye akasema, "Billy, mtu yeyote . . . " Kasema, "Hapana shaka Yohana alikula pilipili nyekundu kisha akashikwa na jinamizi huko kwenye—kwenye kisiwa cha Patimo."

46 Nikasema, "Bw. Bohanon, hukupaswa kusema hivyo." Yeye alikuwa ni bosi wangu, msimamizi.

Akasema, "Vema, ni nani ulimwenguni angaliweza kukielewa Hicho?"

Nikasema, "Kinaeleweka. Kitaeleweka wakati Roho Mtakatifu atakapokuwa tayari kukifunua." Hiyo ni kweli.

47 Naye akasema, "Loo, jamani!" Kasema, "Nilijaribu kukisoma naye mchungaji wangu akajaribu kukisoma," kasema, "tuliingia katika matatizo makubwa mno." Kasema, "Tulikuwa na—na Bibi-arusi amesimama juu ya Mlima Sinai." Mnaona? Kisha kasema, "Halafu tulikuwa na Bibi-arusi huku lile joka likitema maji kutoka kinywani mwake, kufanya vita na masalia ya uzao wa mwanamke. Tulikuwa na Bibi-arusi Mbinguni. Wote watatu, wakati ule ule."

Nikasema, "Huo ni ukosefu wa ufahamu wa kiroho." Mnaona?

Akasema, "Vema, hao hapo, wote kwenye . . . hao watatu wakati ule ule."

48 Nikasema, "Naam, bwana, lakini hivyo sivyo walivyowekwa. Unaona, mliwaita wale mia na arobaini na nne elfu 'Bibi-arusi,' ambao hawakuwa; walikuwa ni Wayahudi. Na wale ambao yule joka aliwatema kutoka kinywani mwake kufanya vita na masalia, wale waliosalia wa ule uzao wa mwanamke walioshika amri na walikuwa na, ushuhuda wa Yesu. Naye Bibi-arusi alikuwa Utukufuni." Mnaona?

49 Wale mia na arobaini na nne elfu, mlango wa 14 wa Ufunuo, walikuwa wamesimama pale juu ya Mlima Sinai, (Hiyo ni kweli kabisa.) wakiwa na Jina la Baba yao kwenye paji la uso wao. Hiyo ni kweli kabisa. Wayahudi, wale masalia wa Wayahudi.

50 Ndipo huyu hapa joka anakuja, ule ukasisi wa Kirumi. (Ambapo, Kanisa lenyewe lilikuwa limenyakuliwa, lilikuwa Utukufuni kwenye Karamu ya Arusi kwa muda wa miaka mitatu na nusu.) Ndipo yule joka, mnaona, *joka* daima ni "Rumi," yule joka jekundu. Sasa kuwahakikishia hilo, katika—katika Ufunuo 12, yule joka alimkasirikia mwanamke aliyekuwa amzae Mtoto mwanamume ambaye atayatawala mataifa yote kwa fimbo ya chuma, naye akatoa katika kinywa chake maji na . . . ama—ama kufanya vita na masalia ya uzao. Lakini yule joka jekundu, kwanza, alisimama mbele ya mwanamke huyu.

Mara tu huyu mwanamke alipokuwa tayari kumzaa Mtoto huyu, alitaka kumla Mtoto huyo mara alipozaliwa. Sasa, ni nani aliyesimama mbele ya kanisa la Israeli (mwanamke Israeli), kumla Mtoto wake (Yesu) mara alipozaliwa? Rumi! Herode alitoa tangazo kwamba—kwamba kila mtu alipaswa kumwua kila mtoto kuanzia miaka miwili kwenda chini, kukatokea mauaji kote ambayo yaliwaua watoto wote wa Kiebrania kote nchini. Jambo lile lile ambalo Farao alifanya kumshika Musa, ambaye alikuwa ni mfano Wake, akawaua watoto wote na akamkosa. Loo—loo—loo—loo, Mungu anajua jinsi ya kuwaficha.

51 Loo, hivi hamna furaha mmefichwa? Loo, mahali pa kujificha! Biblia ilisema, "Kwa maana hamna budi kujihesabu wafu na uhai wenu katika Kristo, umefichwa katika Kristo na kutiwa muhuri kwa Roho Mtakatifu." Ibilisi asingeweza kukupata hata afanye nini. Kamwe asingeweza, unaona. Umefichwa katika Kristo! Jihesabu umekufa! Nao uhai wenu umefichwa katika Kristo, umefichwa katika Mungu kwa Kristo, na kutiwa muhuri kwa Roho Mtakatifu.

52 Sasa, sasa, masalia haya yalikuwa ni mwanamwali aliyelala; ambaye alitoa maji kutoka kinywani mwake kufanya vita na uzao wa mwanamke uliosalia. Sasa, masalia ni kitu gani? Sasa, hapo ina—inawapasa kuweka mifano hii pamoja sasa. Kuna kanisa ambalo ni kanisa la *kawaida*.

53 Ninaenda ku. . .Labda ninaweza kulichora hapa na kulifanya dhahiri kidogo. Sasa, Ndugu Neville, kama nikichukua muda wako kidogo, naomba unisamehe. [Ndugu Neville anasema, "Amina. Sina wowote."—Mh.]

54 Sasa, kuna ninii . . . Sasa kumbukeni ya kwamba kuna nini? Asiyeamini, nitaliandika hilo kama "AS," asiyeamini, na huyo ni mwenye dhambi. Na hapa pana mwingine ambaye ni wa kawaida, nitambandika kama "KA," kanisa la kawaida. Halafu huyu hapa mwingine ambaye ni kanisa lililookolewa, "OK," kanisa lililookolewa. Sasa, yawekeni niani mwenu wakati wote.

55 Sasa, katika kanisa hili lililookoka kuna matabaka mawili, katika kanisa hili papa *hapa* na papa *hapa,* ambayo yalifananishwa na Kristo: moja lilikuwa ni mwanamwali aliyelala, na hilo lingine lilikuwa na Mafuta kwenye taa yake. Sasa, nyinyi—nyinyi nyote. . .Ni wangapi wanaoikumbuka hadithi hiyo? Tutaifikia katika dakika moja tu.

56 Sasa, kwanza, kabla hatujafanya hivyo, tunawaendea wale mia moja na arobaini na nne elfu, wa Ufunuo 7, kusudi lipate kueleweka kabisa. Sasa, hamna budi kukumbuka hili. Nanyi ambao mnaliandika, Ufunuo 7.

57 Hebu kwa namna fulani tuchukue tu wakati wetu. (Na—nanyi ham—hamtabatiza mpaka—mpaka. . .Baada ya ibada asubuhi ya leo, vema.) Tuta. . .Nitajaribu kuweka saa yangu hapa juu na kuangalia ni saa ngapi kusudi tupate kutoka. Sasa

tuna—tuna karibu saa mbili sasa, naye Bwana na atusaidie kutupa somo hili.

> . . . *baada ya mambo haya* . . .

58 Sasa, sisi . . . Mlango wa 6 unashughulika na fa—farasi mweupe, ambaye alikuwa ni Roho Mtakatifu aliyetoka akishinda, apate kushinda. Kisha akaja farasi wa kijivu, Mauti, na Kuzimu yakafuatana naye. Na kila mmoja wa hao wapanda farasi akiwa juu ya farasi.

59 Sasa, "baada ya mambo haya," baada ya maangamizi haya makubwa. Wa kwanza kutokea alikuwa ni Roho Mtakatifu kote duniani, "akishinda, tena apate kushinda"; ndipo akaja yule kwenye ule wakati mkuu wa njaa, "kibaba cha ngano kwa nusu rupia, vibaba viwili vya shayiri kwa nusu rupia, na kadhalika, bali usiyadhuru Mafuta Yangu na Divai"; halafu na kuendelea hata alipoifungua ile—ile mihuri.

> . . . *baada ya hayo nikaona malaika wanne wamesimama katika pembe nne za nchi, wakizizuia pepo nne* . . . *zisivume* juu ya *nchi, wala juu ya bahari,* au . . . *mti wowote.*
>
> *Nikaona malaika mwingine* akishuka *kutoka mawio ya jua, mwenye muhuri ya Mungu aliye hai: akawapigia kelele kwa sauti kuu wale malaika wanne ambao* . . . *kudhuru* . . . *waliopewa kuidhuru* bahari *na* nchi,
>
> *Akisema, Msiidhuru nchi, wala bahari,* wala . . . mti, mpaka *tutakapokwisha kuwatia muhuri watumwa wa Mungu wetu juu ya* vipaji vya uso *wao.*

60 Sasa, kumbukeni, watumishi daima wamekuwa . . . Watumishi wa Mungu ni Myahudi. Ibrahimu alikuwa mtumishi Wake. Mtaifa si mtumishi, ni Bibi-arusi, ni mwana. Hili ni mwana, Kanisa ni mwana. Wayahudi ni watumishi. Loo, laiti mngeweza tu . . . laiti tungalikuwa na wakati wa kuyachambua maneno hayo vilivyo. Mara nyingi mimi hufanya hivyo chumbani mle, ninayachunguza kote kwenye marejeo na kuyaleta. Wayahudi ni mtumishi. Kama nikisimama hapa na kuchukua muda huo wote juu ya "mtumishi," sitayafikia mengine yaliyo muhimu, mnaona. Kwa hiyo kumbukeni tu, fuatilieni hilo kote katika Biblia, nanyi mtaona kwamba Myahudi ni mtumishi wa Mungu.

61 Ni mfano mzuri jinsi gani hapa tungeweza kuendeleza, kama tukitaka kurudi kwenye Ezekieli 4, na kuona hapo kwamba Yeye alisema, "Je, jambo kama hili limetukia hapo awali?" Aliziangalia kuta ndefu, na alipofanya hivyo, aliona machukizo yanayofanywa mjini. Na hapo kukatokea . . . wakaja watu wanne wenye silaha za kufisha. Nao wakaenda kuua kila kitu kote mjini Yerusalemu.

62 Na kabla yeye...hawajaanza kuua, walishika, waliwasimamisha, kwa kuwa alitokea Mmoja amevaa mavazi meupe, mwenye kidau cha wino cha mwandishi (Ni wangapi waliopata kusoma hilo?) ubavuni Mwake, Ezekieli 4. Basi alikuwa na kidau hiki cha wino cha mwandishi ubavuni Mwake, amevaa mavazi meupe, Yeye akasema, "Msiingie mjini, msiue chochote mpaka kwanza mmewatia muhuri watumishi wa Mungu katika vipaji vya nyuso zao." Naye akatoka akaenda akawatia muhuri, hata alisema, kwa watoto wadogo na kila kitu, kuwatia muhuri.

63 Ndipo wale wenye silaha za kufisha, wanne wao walipokuja, wakaingia na kuangamiza kila kitu kabisa, hawakuwa na huruma. Waliwaua wanaume, wanawake, watoto, na kila kitu kisichokuwa na muhuri huu wa Mtu huyu wa kwanza mwenye kidau cha wino cha mwandishi aliyewatia muhuri. Na ninii kuu...

64 Sasa, hiyo ilikuwa ni katika siku za Bwana wetu, wakati alipowaonya juu yake katika Mathayo 24, jinsi ambavyo "Mtakapouona Yerusalemu umezingirwa na majeshi, msiache...msishuke kutoka juu ya paa la nyumba, ama yule aliye shambani kurudi kuichukua nguo yake, bali mwende Yuda." Josephus ameandika hayo hapo, na jinsi walivyotoroka. Basi wale tu waliotoroka walikuwa ni wale walioyachukua Maneno ya Bwana Yesu. Ndipo walipoyaona majeshi yameuzingira, na Tito, katika A.D. 96, walipomwona Tito amezizingira kuta za Yerusalemu na kuwazingira wote mle ndani; walikula nyasi kutoka mitini...walikula gome—gome kutoka kwenye miti, wakala nyasi ardhini, waliwachemsha watoto wao mmoja kwa mwingine na kuwala. Waliwaweka na njaa, wakawaweka tu mle ndani, na hatimaye wakavamia mle ndani na kuwaua hata damu ikatiririka nje ya lango kama—kama kidimbwi kikitiririka, vijito vya damu vikitiririka nje ya lango. Wakaliteketeza hekalu, wakazibomoa kuta, na unasimama pale hata wa leo.

65 Nao Uislamu wa Omar ulijengwa ambapo hekalu lilisimama. Naye Yesu alisema hayo katika Mathayo 24, Akasema, "Mtakapoliona chukizo la uharibifu limesimama mahali patakatifu, ambapo nabii Danieli alinena, alilonena habari zake," halafu yametiwa mabano, kasema, "(asomaye, na afahamu:)" Mnaona, "Mtakapoliona hili chukizo, unajisi wa Uislamu wa Omar umesimama pale ambapo mahali patakatifu palisimama wakati mmoja." Na leo hii huo Uislamu unasimama pale hasa ambapo mahali patakatifu, papo hapo kwenye eneo la hekalu. Uislamu wa Muhamadi umesimama kama vile Yesu alivyosema ungesimama, naam, kama Danieli alivyosema ungesimama, kisha Yesu akathibitisha kwamba ungesimama.

66 Waangalie hao manabii na Mungu hapo wakiyatabiri mambo hayo, ndugu, linapaswa kuzisimamisha nywele nyuma ya shingo

zetu kujua ya kwamba tuko kwenye wakati wa mwisho. Tuko mwisho! Hakuna kilichosalia. Mambo haya yote yanatukia jinsi tu Yeye alivyosema yangetukia, mbona, linapaswa kututia moyo, kutufanya tujitayarishe. Yeye alisema, Yesu alituonya, kasema, "Mtakapoyaona mambo haya yakitimia," kama yale tunayozungumzia, kasema, "inueni kichwa chenu, ukombozi wenu umekaribia."

67 Nalo lingetufaidi nini sisi tukiupata ulimwengu wote? Tutaupoteza, kwa vyovyote vile. Ha—hatuwezi kushinda jinsi hiyo. Kuna ushindi mmoja tu, hiyo ni kwa njia ya Kristo. Mchukue Kristo, ndipo huna budi kushinda. Huna budi kuondoka hapa; huenda ukaondoka kabla ibada hii haijakwisha, huenda ukaondoka kabla ya machweo ya jua usiku wa leo, huenda uka-. . . ukaondoka kabla halijachomoza asubuhi, kabla ya Jumapili ijayo huenda ukawa umeondoka, sisi sote. Hatujui wakati tutakapoondoka, bali unajua huna budi kuondoka. Kwa hiyo si ni jambo la kijinga kuahirisha? Una—unakanyaga-kanyaga, una—unacheza na mauti.

68 Ni kama ile sileji ya kale ya kutelezea. Walikuwa wakipanda sileji na kukizunguka kitu hiki, waone jinsi wangeweza kukaribia; ndipo mara, kabla hawajajua, hao wakateleza mpaka chini. Na hivyo ni kama tu jinsi unavyofanya, unateleza tu huku na huku. Hujui ni dakika ipi kitu fulani kitakapokukatiza, nawe umekwisha; moyo unakoma, ajali ya motokaa, kitu chochote tu kitukie, nawe ufe. Ndipo kikomo chako cha Milele kimewekwa papo hapo mbele zako. Liwazie hilo, ewe rafiki.

69 "Sasa, mtakapoliona chukizo la uharibifu limesimama mahali patakatifu." Sasa, basi, katika siku za kuja kwa Tito baada ya Yesu kuondoka, Roho Mtakatifu alikuwa mtu huyo mwenye kidau cha wino wa mwandishi ubavuni Mwake. Naye alipitia Yerusalemu na kuweka alama juu ya watu. Na sasa nataka uone jambo fulani, ewe mfuasi wa kanisa. Ati unadai kuwa na Roho Mtakatifu? Yeye alisema, "Usitie muhuri yeyote wao ila wale wanaoomboleza na kulia kwa ajili ya machukizo yanayofanywa mjini." Sasa, yuko wapi mtu yeyote aliyelemewa sana kuhusu ulimwengu sasa na hali zake?

70 Vema, "Mimi ni Mmethodisti, mimi ni Mbaptisti, Mpresbiteri, kwa hiyo inaleta tofauti gani?" wao wanasema.

71 Loo, si ule mzigo wa sikuzote kwa ajili ya waliopotea, ule utamu. Usiruhusu chochote kiinuke na kuweka chuki nafsini mwako. Haidhuru mtu yeyote atakufanyia vibaya jinsi gani au chochote kile, kamwe usiruhusu! Usiwe na hatia ya kuachilia kitu hicho kitie nanga nafsini mwako. Kitamhuzunisha Roho Mtakatifu akuondokee. Hakika kitamhuzunisha.

72 Ninakumbuka nikisema kitu fulani hapa miaka miwili ama mitatu iliyopita ambacho kilikuwa kibaya. Ilikuwa ni mawakili walionipigia simu, nami nikaenda na . . . Mke wangu ameketi

pale. Ningeninii . . . kichwa changu, kilienda . . . nilijisikia kana kwamba kinang'oka, nami ni—nikarudi. Nao—nao wakapiga simu na kusema, "Mwambie aje alasiri ya leo."

Naye Meda akasema, "Ni wale mawakili."

Nikatokea upesi mlangoni, nikasema, "Mwambie hata simo humu."

Akasema, "Bill!"

Nami nikasema, "Mwambie siko hapa ndani sasa hivi." Ndipo nikatoka nje.

73 Ndipo nikatoka huko nje na kujisikia vibaya, kisha nikarudi. Naye akamwambia; nikaona ameudhika.

74 Nikaenda kumwombea nanii . . . kulikuwako na mtu aliyeingia hapa, alikuwa na maskini mtoto mchanga mgonjwa. Ndipo nilipoanza kuweka mkono wangu juu ya mtoto huyo mchanga nimwombee, kitu Fulani kikaniambia, "Wewe ni mnafiki." Mnaona? "Unajua ulichofanya."

75 Nami nikasema, "Bwana, sistahili kumwombea mtoto wako. Unaona, Roho Mtakatifu alihuzunika ndani yangu wala hakuna haja ya kuweka mikono yangu juu ya huyu mtoto. Ngoja tu mpaka nitakaposahihisha jambo fulani."

76 Nikashuka na kumwambia . . . nikamwambia wakili wangu, nikasema, "Ni—nilifanya kosa."

Akasema, "Nilifikiri ulikuwa umetoka."

Nikasema, "La." Nikasema, "Hiyo ilikuwa ni . . . Nilimfanya mke wangu kusema jambo ambalo halikuwa kweli." Nikasema, "Sa—samahani, si—siku—sikukusudia kufanya hivyo." Nikasema, "Utanisamehe hilo?"

Kisha nikamwomba mke wangu anisamehe hilo.

77 Ndipo nikarudi huko juu Green's Mill, ilikuwa ni Julai. Loo, kulikuwa kutulivu sana mwituni, nami nilikuwa ndani ya pango alasiri yote, nikiomba. Basi nikaenda na kusimama juu ya mwamba huko nje nami ningeangalia huko mbali kupitia vilimani, na ni kuzuri sana, na majani na kila kitu, kimya tu; yapata saa kumi na moja, thenashara, alasiri, msimu wa kiangazi. Hakuna kitu, kulikuwa kutulivu sana, siku yenye joto. Ndipo nikasema, "Baba wa Mbinguni, Musa, ulimsimamisha juu ya mwamba wakati mmoja Nawe ukapitia karibu." Nikasema, "Kama ukinisamehe uovu huo niliofanya, waweza kupita hapa tena na uniruhusu nikuone?" Na papo hapo mkono wangu wa kushoto kwenye upande mmoja wa kilima palitokea upepo mdogo wa kisulisuli ulioanza kuvuma kwa utulivu sana kwenye majani, ukashuka moja kwa moja karibu nami *hivi* na kupitia moja kwa moja msituni. Nililia tu kama mtoto mchanga.

78 Nikarudi chini, nikasema, "Ninajua dhambi zangu zimesamehewa sasa." Mnaona?

79 Mnaona, daima ondoa mashina yote ya chuki ndani yako. Unaona? Haidhuru mtu yeyote amekufanyia nini, acha . . . mweke Mungu tu mle ndani ambaye ataweka uovu wote mbali na wewe.

80 Sasa, hawa Wakristo waliokuwa na onyo la Kristo, sasa angalieni, mfano wa jambo tunalolizungumzia asubuhi ya leo. Wakristo hawa waliokuwa na onyo hilo, waliondoka Yerusalemu kwa kuwa walijua lilikuwa karibu kutukia.

81 Sasa waangalieni wafuasi wa kanisa, aina ya watu walioenda kanisani, kujiunga tu na kanisa, wote walisema, "Mbona, kuna majeshi yanayokuja, kuna vita vinakuja, sasa hima twende nyumbani mwa Bwana na kuomba." Bali wamechelewa kupita kiasi. Halikuwafaidi kitu, mnaona.

82 Bali walikuwa wakiangalia hilo onyo, hawa wanafunzi, wakijua yale Yesu aliyosema, nao wakaponyoka. (Wanahistoria walisema kwamba "Wale walioitwa 'wala-watu,'" walisema, "waliula mwili wa—wa mtu huyu aliyeitwa 'Yesu' aliyekuwa akiwaponya." Mnaona, walikuwa wakila ushirika. Hawakuninii . . . hakujua ulikuwa ni nini, mnaona, maana alikuwa ni mtu wa kimwili, sio mwaminio, na ni mwana-historia tu. Naye . . .) Nao wakaponyoka hasira iliyoijilia dunia.

83 Sasa, mnaona, kisha Yerusalemu yote ikaangamizwa. Sasa hilo . . . Sasa hili hapa linaenda sambamba kikamilifu, Ufunuo 7. Sasa angalieni! Tangu wakati wa Tito kuuzingira Yerusalemu, duniani kote, hapajakuwapo na wakati kote katika historia ambapo ulimwengu mzima ulienda vitani mpaka mwaka wa 1914. Sasa sikilizeni kwa makini! Sasa hapa ndipo Bw. Rutherford alipoenda kombo, nina hakika, papa hapa. Sasa angalieni:

> *Baada ya hayo nikaona* malaika mwingine amesi- . . . *malaika wanne wamesimama katika pembe nne za nchi,* (Hiyo ni kusimama namna *hii*, kwenye pembe nne za dunia.) *wakizizuia pepo nne za nchi,* (Sasa, mtu yeyote anajua maana ya *pepo* katika Biblia, *pepo* ni "vita, ugomvi," ibilisi ndiye mamlaka, mtawala wa anga, mnaona.) . . . *wakizizuia pepo nne* . . . *upepo usivume* juu ya *nchi,* ama, . . . *bahari,* . . .
>
> *Kisha* . . . *malaika mwingine* akishuka *kutoka mawio ya jua* (ambako Yesu atatokea), *mwenye muhuri ya Mungu aliye hai:* katika kipaji cha uso wake, mkononi mwake: *akawapigia kelele kwa sauti kuu wale malaika wanne,* waliokuwa wauangamize ulimwengu, akisema . . . *waliopewa kuidhuru* bahari *na* nchi,
>
> *Akisema, Msiidhuru nchi, wala bahari, wala* . . . *miti,* hata *tutakapokwisha kuwatia muhuri watumwa wa Mungu wetu juu ya* vipaji vya uso *wao.*

84 Sasa, Mungu hana wakati, Wake ni Umilele. Sisi hupima kwa nyakati, kitu pekee tukijuacho ni inchi na miraba, na maili na kadhalika. Mungu ni Umilele, hana mwanzo wala mwisho. Mnaona, Yeye—Yeye ni wa Milele.

85 Sasa, katika mwaka wa 1914 ulimwengu wote ulikuwa ukielekea Ujerumani kwa ajili ya vita vya dunia, hiyo ni kweli, ulimwengu mzima ukienda kwenye vita vya dunia. Na je, mliona? Hakika lilikuwa ni jambo la ajabu.

86 Ninamtaka rafiki yangu mwema anayeketi hapa, baba ya Ndugu Wood, alipate hili dhahiri. Mnaona, walikuwa . . . yeye ni Shahidi wa Yehova aliyeongoka, mnaona.

87 Na kwa hiyo basi jambo hili, wote walikuwa wakienda vitani. Nyote mnakumbuka hilo vizuri, katika mwaka wa 1914. Sasa, si ni ajabu (mumo humo katika *Kupungua Kwa Vita Vya Ulimwengu,* nina juzuu lake, katika juzuu la pili, yapata ukurasa wa arobaini na nne) kwamba hawajui hata wa leo ni nani aliyesimamisha vita hivyo. Kaiser Wilhelm alisema hakutoa kitu kama hicho. Lakini, mara ghafla, vilikoma wala hakuna ajuaye ni kwa nini. Walikuwa wakipigana, hawa hapa wanakuja . . . huku mbele, na ninii . . . wote wakaja: "Vyote vilikuwa vimekwisha, vita vikaisha." Na walikuwa tayari wametia sahihi mkataba wa amani, pasipo kujua kilichotukia.

88 Sasa, hakika, hiyo ingechukua siku moja ama mbili kuelezea hayo yote. Hawakujua; bali hebu tuyafunike yote na kugusia mambo yaliyo muhimu. Mungu ndiye aliyevikomesha, kulitimiza Neno Lake! Huyo hapo yule Malaika aliyevikomesha. Hao Malaika walitoka wakiwa na vitu vya kufisha (Kitu gani?) kuuangamiza ulimwengu mzima, ndipo Malaika mwingine akasema, "Ngojeni kidogo! Msifanye hivyo, hatuna budi kuwatia muhuri hawa watumishi wa Mungu wetu kwanza katika kipaji cha uso wao, kwanza."

89 Hiyo ilikuwa ni kule tu mwanzoni mwa Pentekoste, huko nyuma mwaka wa 1906, 1914, huko chini. Ni wangapi wenu mnaojua? Je, kuna Mpentekoste yeyote wa kale humu ndani, anayezikumbuka hizo siku mle ndani? Hakika. Wakati huo, kwenye nyakati hizo za mwanzoni, ambapo ndio kwanza Roho Mtakatifu aanze kushuka nao watu wakaanza kumpokea Roho Mtakatifu na kunena kwa lugha na kuwaombea wagonjwa na kadhalika, ndiyo kwanza yaanze kutukia, ama katikati tu ya nyakati hizi mbili hapa; wakati tu ilipoanza, Kanisa lilikuwa ni halisi. Ndipo Pentekoste ikaanza kuchukua dhehebu, Assemblies of God, na Church of God, na kadhalika, ndipo likaingia katika itikadi zao kama vile tu walivyo sasa. Kwa hiyo ni . . . Tuko katika mwisho wa wakati, mnaona. Kila kitu kikielekea kwenye mwisho wake, kila kitu kinaelekea moja kwa moja hapa mwishoni.

90 Sasa, juu ya hawa, wale wanne . . . Unaona, vilikwisha ta—tarehe kumi na moja Novemba, saa tano [Kiingereza: eleven o'clock—Mf.] mchana; mwezi wa kumi na moja wa mwaka, siku ya kumi na moja ya mwezi, na saa ya kumi na moja ya siku. Mnakumbuka basi yale Yesu aliyosema kuhusu hilo? "Mtu mmoja alienda kwenye shamba la mizabibu kufanya kazi wakati mmoja, mmoja akapata rupia moja, na mwingine akaenda," hao walikuwa ni watu wa saa kumi na moja. Hiyo ilikuwa ni kweli? Hao hapo, watu wa saa kumi na moja; vimezuiliwa. Sasa inafikia wakati wao wa kuingia, nao wanakusanyika kutoka kwa Wayahudi hao, kama taifa. Walikuwa wametawanyika kote ulimwenguni, huko chini kabisa Irani na mahali mbalimbali ambako hata hawakujua Yesu alikuwa duniani, kamwe hawakujua lolote kuhusu Agano Jipya wala chochote kile.

91 Na sasa mnaweza kuangalia kwenye gazeti la *Look*, na *Life* na mengineyo, yakionyesha picha zao wakirudi. Hivi Yesu hakusema hilo, "Mtakapoona mtini ukichipusha"? Wayahudi daima wamekuwa ni mtini. "Kizazi hiki hakitapita hata haya yote yatimie." Na sasa wamerudi tayari, tayari ni taifa, tayari wana pesa zao wenyewe na bendera yao wenyewe, na kila kitu, nalo limetambuliwa katika U.N., hao ni taifa. Limetulia! Liko tayari! Sasa, tayari kwa kitu gani? Kule kutiwa muhuri kwa mia na arobaini na nne elfu (Sasa, tutafikia hayo kwa dakika moja tu.) wa Israeli; hao Wayahudi, sio lile kundi la Wall Street ambalo sikuzote limedanganya na kuiba na kila kitu kingine, ninamaanisha Wayahudi halisi, dhahiri, Wayahudi wa kweli wanaotii amri za Mungu huko chini.

92 Sasa, Wayahudi halisi wanakusanyika Palestina tena, na kile hasa nabii alichosema; kama vile Ishmaeli na Isaka walivyokuwa wakishikana koo, siku zote wanapigana, ilitabiriwa watakuwa kule katika siku ya mwisho, nao wale pale wameketi. Ishmaeli papa hapa, na yapata umbali wa jengo la mji hapa na huyo hapo Isaka, na wote wawili (Waislamu na Wayahudi) wakipigana katika nchi-isiyo na mwenyewe.

93 Sasa ili kuona kama Ujumbe huu tulio nao unahusika nalo ama hauhusiki. Saa ile ile ambayo Israeli ilitia sahihi kwamba ni taifa, ilikuwa ndiyo saa ile ile, siku ile ile, mwezi ule ule, kila kitu kingine: nilikuwa huko kwenye Green's Mill, Indiana, wakati Malaika yule aliponitokea na kunituma hudumani na Huu; akiisha kukutana nami huko mtoni na kuniambia kitakachotukia, kisha akaniagiza miaka kumi na mmoja baadaye kwenye saa ile ile ambayo Israeli ilitia sahihi kama taifa. Yote yana uhusiano.

94 Mnaona, Malaika wa Bwana yuko duniani sasa, mnaona, Yeye anazunguka akiandaa kila kitu kwa ajili ya kuja kwa Bwana. Ndio Malaika wale wale waliosikia zile dhambi wakati waliposhuka kwenda Sodoma nao walikuwa wamepata . . .

kasema, “Tumeshuka kuja kuona kama mambo haya ndivyo yalivyo, yale tuliyosikia.”

95 Mnakumbuka hilo? Ndipo Malaika mmoja akashuka akaenda. . .(Mmoja alikaa pamoja na Ibrahimu Mteule.) Sodoma ilikuwa *hapa* chini, naye Lutu alikuwa katika Sodoma, nao Malaika wawili wakaenda kule chini na kuwahubiria na kulitoa maskini lile kundi dogo sana, mwanamwali aliyelala. Mnaona? Vema. (Bali yule Malaika mmoja alikaa pamoja na Ibrahimu.) Hawa Malaika walihubiri *huku* chini, Billy Graham wa kisasa na hao wengine, wakawavuta na kuwatoa.

96 Lakini Malaika aliyesimama pamoja na Ibrahimu alikuwa ameuelekeza mgongo Wake kwenye hema, ndipo Yeye akasema, “Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?” Alijuaje alikuwa ameolewa, alikuwa ameoa? Naye alijuaje alikuwa na mke? Basi alijuaje jina lake, jina la mke lilikuwa ni Sara? Kasema, “Yuko hemani nyuma yako.”

97 Akasema, “Vema, nimekupa ahadi.” “Mimi” Mnaona huyo Malaika alikuwa ni nani. “Nilikupa ahadi. Nitakuzuru kulingana na wakati wa uhai, Sara atamzaa mtoto huyu mchanga.”

98 Naye Sara, kwenye hema nyuma Yake, akacheka kifichifichi. Na yule Malaika, huku amempa kisogo, akasema, “Kwa nini Sara akacheka?” Mnaona ile ishara aliyolipa Kanisa Teule?

99 Mnaona ishara waliyopata Sodoma?

100 Hayo hapo matabaka yako matatu ya watu papo hapo tena, tumeyarudia moja kwa moja tena.

101 Tuna ninii. . .wahudumu hawa wanaohudumia ulimwengu huo huko nje. Baada ya Billy Graham kumpokea Roho Mtakatifu, asingeweza kutoka aingie *hapa*. Huo ni uwanja wake *huko* chini naye anautambua, naye Mungu amemshikilia huko. Mnaona? Kwa mahubiri hayo ya kielimu, jambo analosikia hapa, lakini anajaribu kutoa Sodoma kwa nguvu, kujaribu kuwatoa kwa nguvu, ama kumpa neema yule mwanamwali aliyelala. Mnaona?

102 Lakini huyu *hapa* Ibrahimu na tabaka lake, naye Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.”

103 Mnaona, malaika hao watakuwa hapa duniani wakifanya jambo lile lile. Mnaona, hiyo ndiyo sababu Billy huenda kwa Baptisti na kadhalika namna hiyo. Hana budi kwenda! Mnaona, Jack Shuler na hao wanaume—wanaume wote mashuhuri huko nje wanaoenda. . . wanamiamsho, inawabidi kwa sababu wana—wanawatoa kwa nguvu. Kamwe hawakufanya miujiza kule chini; michache, kama vile kuwapofusha watu. Lakini kuhubiri Injili huwapofusha, mnaona, Biblia inasema hivyo.

104 Lakini jamaa huyu *hapa* nje alifanya ishara hii, ishara ya kimbinguni, kwa Ibrahimu na kundi lake, ambalo ni Kanisa-Teule.

105 Sasa, mwaka wa 1914, ulimwengu uliingia vitani, wala hawajapata kuwa na amani tangu wakati huo; daima wakiingia ndani, wakiingia ndani, wakiingia ndani, na wangali wanafanya jambo lile lile bado. Nao walikuwa wakifanya nini? "Kushikilia!" Ee Mungu, turehemu! Wakishikilia kitu hicho kikuu nilichokiona katika ono (kitu hicho chote kikafikia maangamizi), wanashikilia atomiki, kuvishikilia vita wasije wakajiangamiza mpaka kitu hicho kitakapokuja kuiangamiza; mpaka Israeli watakaporudi na kukusanyika, ndipo Ujumbe utawaendea Israeli nao watatiwa muhuri kwa muhuri huo wa Roho Mtakatifu. Mnaona, baada ya Mataifa kuitwa; watu kwa ajili ya jina Lake wataitwa watoke, ambao katika wakati huu *hapa* wanaitwa. Ndipo Israeli watapokea tu Ujumbe wa miaka mitatu na miezi sita.

106 Danieli alisema hivyo, akasema watakuwa hivyo, kungekuwako, "Kulikuwako na sabini . . . ama—ama miaka saba iliyotabiriwa kwao, ingali imesalia kwa ajili ya wokovu wa Wayahudi." Yeye alisema, "Masihi, aliye Mtawala, ambaye ni Kristo, atakuja na kutabiri katikati ya miaka hiyo sabini . . . ama miaka saba, atakatiliwa mbali." Yesu alihubiri miaka mitatu na nusu kisha akakatiliwa mbali, nayo sadaka ya kila siku ikaondolewa ambayo Danieli alisema. Vema.

107 Halafu kuna wakati uliotolewa kwa Mataifa, na wakafikia kwenye wakati huu. Halafu bado kuna miaka mitatu na nusu iliyosalia kwa Wayahudi. Sasa kama tukifungua Ufunuo 11, tutachukua papo hapo mwisho (Kanisa halionekani mpaka mlango wa 19 wa Ufunuo.), bali mwishoni mwa huo, Eliya na Musa wanarudi tena na kuwahubiria Wayahudi. Watu wawili waliotiwa mafuta kwa Roho huyo, ama labda wao wenyewe, hawakufa. Kwa hiyo wanawaua na kuwekwa katika njia iitwayo *Sodoma* ambapo Bwana wetu alisulubiwa, "Yerusalemu." Ndipo baada ya siku tatu, mbona, uhai (Roho wa Uhai) aliingia ndani yao nao wakapanda juu, wakafufuka. Halafu yapata theluthi moja ya dunia ikalipuliwa vipande-vipande wakati huo. Walifanya maajabu na ishara pamoja na Wayahudi.

108 Sasa hawa hapa wale Wayahudi ambao wanakuja kuwahubiria. Ulimwengu ni . . . hauwezi . . . hauwezi kulipuana ama kuuana, ama maangamizi kuja, mpaka Wayahudi hao warudi mahali pale; hii hapa Biblia ikisema hivyo, aliwaona wale Malaika wanne. Basi angalieni kile hawana budi kupokea; hawana budi kumpokea Roho Mtakatifu kama tu walivyofanya.

109 Kama huyo Mtu mwenye kidau cha wino wa mwandishi alikuwa ni Roho Mtakatifu, (Tunatambua hilo, kila mtu, anayeisoma Biblia.) vema, vivyo huyu ni Malaika yule yule

anayekuja tena pamoja na Roho Mtakatifu, "muhuri wa Mungu aliye hai." Efeso 4:30: " . . . roho Mtakatifu wa Mungu . . . kutiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu."

110 Wala hawawezi kufanya chochote sasa mpaka hao Wayahudi watakaporudi. Na majuma machache tu yaliyopita walikirasimisha kitu hicho chote pamoja na likaingia kwenye U.N. Liko tayari! Tuko kwenye mwisho, kila kitu kimetiwa muhuri sasa.

111 Sasa, sasa angalieni, kuthibitisha kwamba hao ni Wayahudi, sasa, nitachukua ninii:

> *Akisema, Msiidhuru nchi, wala bahari*, wala mti wowote, hata *tutakapokwisha kuwatia muhuri watumwa wa Mungu wetu juu ya vipaji vya* uso *wao*.

112 Sasa, kuthibitisha ya kwamba ufunuo huu ni wa kweli, angalieni hiki, kifungu cha 4:

> *Nikasikia hesabu yao . . . waliotiwa muhuri: na walitiwa muhuri watu mia na arobaini na nne elfu,* wa *makabila yote ya Israeli*.

113 "Israeli." Wako wapi? Ndio kwanza wakusanyike. Wako kule wakiwa tayari, wakingojea wakati wa kutiwa muhuri uje. "Wa kabila la Yuda kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri. Kabila la Rubeni, kumi na mbili elfu. Kabila la Gadi, kumi na mbili elfu. Asa, kumi na mbili elfu. Naftali, kumi na mbili elfu." Na kuendelea na kuendelea, Simeoni na loo, nanii . . . kuendelea hata Benyamini, yale makabila kumi na mawili. Na kumi na mbili mara kumi na mbili ni mia na arobaini na nne elfu. Mnaona? Sasa, hao ndio . . .

114 Sasa kama mkiangalia kwenye mlango wa 14, hebu kidogo tu, hapa mnaona:

> *Kisha nikaona, na tazama, huyo Mwana-Kondoo amesimama juu ya . . . mlima* Sinai, *na watu mia na* arobaini na nne *elfu pamoja naye, wakiwa na jina la Baba yake limeandikwa katika vipaji vya* uso *wao*.

115 "Mlima Sinai." Mwana-kondoo alikuwa amerudi kutoka Unyakuoni. Kisha akarudi, kama tulivyolichukua hivi majuzi usiku, kama vile Yusufu alivyowaondosha Mataifa wote hapo aliposimama karibu na ndugu zake, akasema "Mimi ni Yusufu, ndugu yenu!" Ndipo wakahofu.

116 Mnakumbuka wakati wa kanisa pale mahali tulipokuwa nao, wakati Yeye angerudi? Hata wale waliokuwa wameichoma mikono Yake, basi watasema, "Ulipata wapi makovu hayo ya misumari?"

117 Akasema, "Mikononi mwa rafiki Zangu." Nao wakaomboleza. Na kila familia ikajitenga na nyingine, nao wakaomboleza na kuomboleza na kuomboleza, kwa sababu kwamba walikuwa wametenda uovu huu. Masihi wao

mwenyewe, Mungu Mwenyewe. Naye atawaambia vile vile hasa kama a—alivyowaambia . . . Yusufu alivyowaambia Israeli, alisema, "Msijikasirikie, kwa kuwa Mungu alifanya hivyo kuhifadhi uhai."

118 "Basi Mungu . . ." Biblia inasema kwamba "Mungu aliyapofusha macho ya Wayahudi ili Wamataifa wapate nafasi (sisi, sisi wenyewe), kuwachukua watu kwa ajili ya Jina Lake, Bibi-arusi Wake kutoka kwa Mataifa." Loo, ni zuri! Sivyo? Haya basi.

119 Hao hapo wenu mia na arobaini na . . . Sasa kama ukitaka kuona Bibi-arusi akitokea baada ya hayo, kuonyesha ya kwamba hao mia na arobaini na nne elfu sio Bibi-arusi, endeleeni tu kusoma sasa kutoka kwenye mlango wa 8 na kuendelea; ama, naam, mlango wa 8; ama kifungu cha 8, ninamaanisha, kuanzia mlango wa 7. Hebu tuanzie kwenye kifungu cha 9—cha 9, maana kifungu cha 8—cha 8 ni kule kutiwa muhuri kwa Benyamini, elfu kumi na mbili.

> *Baada—Baada ya hayo nikaona, na tazama, mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu,* (Huyu hapa Bibi-arusi anakuja.) *watu wa kila taifa, . . . kabila, . . . jamaa, na lugha, wamesimama mbele ya kile kiti cha enzi, na mbele za Mwana-Kondoo; wamevikwa* mavazi *meupe, wana matawi ya mitende mikononi mwao;*
>
> *Wakalia kwa sauti kuu wakisema, Wokovu una Mungu wetu aketiye katika kiti cha enzi, na Mwana-Kondoo.*
>
> *. . . malaika wote walikuwa wakisimama* pande zote *za kile kiti cha enzi, na za hao wazee, na za wale wenye uhai wanne, . . . wakaanguka—wakaanguka kifudifudi mbele ya kile kiti cha enzi, wakamsujudu Mungu,*
>
> *Wakisema, Amina:* Baraka, . . . *utukufu, . . . hekima, . . . shukrani, . . . heshima, . . . uweza, . . . nguvu, zina Mungu wetu hata milele na milele. Amina.*
>
> *Akajibu mmoja wa wale wazee akiniambia, Je, Watu hawa waliovikwa mavazi meupe ni akina nani? Na* wametoka *wapi?*
>
> *Nikamwambia, Bwana wangu, wajua wewe. Akaniambia, Hao ndio* wanatoka *katika dhiki ile iliyo kuu, nao wamefua mavazi yao, na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo.*
>
> *Kwa hivyo* wako *mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, nao wanamtumikia mchana na usiku katika hekalu: . . .*

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Mnaona?

120 Mke wako hufanya nini? Hukutumikia nyumbani. Unaketi chini, anakupa chakula chako, anazitengeneza nguo zako. Unaona, anakutumikia usiku na mchana nyumbani. Mnaona?

Naye huyu, hawa wa mataifa yote, Wamataifa, ambao ni Bibi-arusi, wako mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, pamoja Naye mchana na usiku. Nyote mnakumbuka tulilosema, jana usiku na kulizungumzia?

> *. . .na yeye aketiye katika kiti cha enzi atatandaa hema yake juu yao.*
>
> *Hawataona njaa tena, wala hawataona kiu tena; wala jua halitawapiga—halitawapiga, wala hari iliyo yote.*
>
> *Kwa maana huyo Mwana-Kondoo, aliye katikati ya kiti cha enzi, atawachunga, naye. . .atawaongoza* kwenye *chemchemi za* maji *yenye uhai: na Mungu atayafuta. . .machozi yote katika macho yao.*

121 Sasa, hao hapo mia na arobaini na nne elfu wako (Israeli) wanaokungojea kuja kwa Bwana wala hawawezi kuingia mpaka Mataifa wamekwisha, hawana budi kumalizika.

122 Sasa, huenda nikasema jambo dogo tu la kibinafsi, natumaini, natumaini mtalifahamu. Wakati Lewi Pethrus wa Stockholm, Swedeni, yule mwangalizi mkuu, kiongozi wa makanisa ya Filadelfia, yeye alituma kule chini Biblia milioni moja kwa hawa Wayahudi, Agano ndogo. Nina moja ya hizo huko juu, kumbukumbu ndogo kutoka kwake. Myahudi sikuzote husoma kutoka nyuma kwenda mbele, na kwa hiyo mnajua jinsi lugha ya—yao ilivyo. Nao wangevisoma Vitabu hivi, ndipo wakasema, "Vema, ikiwa Yesu huyu ndiye Masihi, Naye amekufa na Roho Wake amerudi katika umbo la Roho, hebu tumwone akifanya ishara ya nabii, ndipo tutamwamini."

123 Ni mpangilio mkamilifu jinsi gani! Nikawazia, "Bwana, huu hapa wakati sasa. Sasa ndio wakati, huu hapa." Kwa hiyo mimi huyo nikapanda ndege, mimi, Billy, Loyce, na kuondoka.

124 Nilikuwa nikienda huko India, ndipo nikasema, "Sasa, nitakapokuwa nikirudi, nitaingia upesi hapa nami nitauleta Ujumbe kwa Wayahudi, na kuwapeleka huko nje na kusema, 'Ni kweli?'"

125 Wayahudi sikuzote huwaamini manabii wao, sote tunajua hilo. Maana Mungu aliwaambia ya kwamba Masihi angekuwa nabii, nao wanawaamini manabii wao, naye Mungu alisema, "Akitokea kati yenu mtu ambaye ni nabii, mwonaji, na ikiwa yeye. . .Nitamshughulikia katika maono na kadhalika. Na—na kama asemayo yakitimia, basi msikieni, kwa kuwa Mimi niko pamoja naye." Mnaona? "Lakini kama lisipotimia, basi msiwe na uhusiano wowote na nabii huyo, maana si—si—siko pamoja naye. Bali kama likitimia, lile asemalo, basi msikieni, maana niko pamoja naye." Nao Wayahudi wanajua hilo.

126 Nami nikawazia, "Loo, jamani! Si ingekuwa ni ajabu sana! Nitajikusanyia yapata elfu nne ama elfu tano wao na kusimama huko nje, na niwaache—niwaache tu waisome

hiyo Biblia na kusema, 'Ikiwa huyu ndiye Masihi, hebu tumwone akiifanya ishara ya nabii.'" Nikasema, "Itakuwa ni mpangilio wa jinsi gani!" Nilikuwa na tiketi yangu mkononi mwangu, yapata tu dakika thelathini kabla ya wakati wa kuitwa kwenye kipaza sauti cha shirika la ndege la Saudia. Kwa hiyo nilikuwa nimesimama huko Cairo, Misri, nami nikawazia, "Mungu asifiwe! Katika saa mbili zingine Wayahudi watapokea kitu kile kile walichokipokea huko Pentekoste, hakika kabisa." Nikawazia, "Nikisimama pale na niweze kuwaambia, 'Nendeni mkajichagulie kundi la watu kutoka miongoni mwenu, mkawalete hapa, muone kama Yeye angali ni Masihi.' Mnaona, ndipo basi nitasema, 'Sasa, katika mahali pale pale ambapo babu zenu walimkataa Masihi huyu, ninyi mpokeeni. Inueni mikono yenu Naye atanini . . . mtampokea Roho Mtakatifu sasa hivi.' Na ndipo watauhubiria ulimwengu katika sehemu yao ya ulimwengu mara wao . . . watakapolipokea. Niwapate viongozi, sio . . . Niguse tu kiini chao, hao viongozi, niwaache wauanzishe."

127 Ndipo kitu Fulani kikanigusa na kusema, "Kamwe usiende sasa, kwa kuwa wakati haujatimia bado." Uh-hum. Mataifa hawajatimia bado, mnaona, siku haijakwisha.

"Loo," nikawazia, "huyo ni mimi tu."

128 Kwa hiyo nikaanza tena, na ikawa mbaya sana hata nisingeweza kuvumilia. Ndipo nikaenda nyuma ya banda la ndege na kuinamisha kichwa changu, nikasema, "Baba, huyo ni Wewe unayesema nami?"

129 Akasema, "Usiende Israeli sasa, saa haijafika bado." Nikaingia tu ndani, nikabadilisha tiketi yangu, ikaelekezwa kwingine, nikaenda kwingine. Mnaona, kwa kuwa ile saa haijawadia bado.

130 Lakini moja ya siku hizi Ujumbe utaenda Israeli, na hilo litaninii . . . Mungu atawatumia Musa na Eliya, katika Ufunuo 11, nao watafanya ishara na maajabu na ishara ya Yehova; huku Mataifa yamekwisha, neema ya . . . siku ya neema italiondokea kanisa la Kimataifa, wakati wa Pentekoste utaondoka. Madhehebu yataendelea kwa sababu watakuja hapa pamoja na mwanamwali aliyelala (Tutaingilia hilo katika dakika moja tu.), bali watatokea katika kundi hilo.

131 Lakini basi watakapofanya, watakapofanya hivyo, Wayahudi wataupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu na kutakuwako na uamsho kule ambao utazifunga mbingu katika siku za, "Isinyeshe!" Watafanya kila namna ya ishara na miujiza. Na hatimaye ukasisi wa Kirumi . . . Wayahudi wana utajiri wa ulimwengu, na—na kwa hiyo Kanisa Katoliki la Kirumi litavunja mapatano yake na Wayahudi baada ya jambo hili kwisha na ndipo kutakuwako . . . (ule mkataba waliotia sahihi kati yao), ataenda huko chini, na ndipo Mungu atakaposimama

kama alivyofanya za—zamani za kale, na kuwapigania Israeli. Hatimaye watawaua hawa manabii wawili, nao watalazwa mtaani, na kuwatemea mate.

132 Kama walivyowafanyia hawa mhudumu wa Kipentekoste na mke wake na watoto hapa majuma machache yaliyopita huko chini, na maskini tumbo hilo likafura kubwa *hivi*, la watoto, ambapo walipita hapo na kuwatemea mate, wakawaacha walale hapo kwenye jua kali kwa siku tatu ama nne pasipo kuwazika.

133 Watafanya jambo lile lile! Biblia ilisema hivyo! Watafanya jambo lile lile pale pale. Basi watakapofanya hivyo, baada ya siku tatu, wamelala maiti, Roho wa Uzima ataingia ndani ya manabii hao wawili nao watafufuka na kupaa Utukufuni. Na, yapata wakati huo, moto utaanza basi. Huo ni wakati wa mwisho. Hapo ndipo itakapoishia.

134 Lakini kabla hilo halijatukia, Wamataifa, Bibi-arusi mteule. . .Kutakuwa na baadhi yenu watakaokuwa wameketi mezani, moja ya asubuhi hizi, mmoja atachukuliwa, huyo mwingine aachwe. Hatimaye utashangaa, "Kwani kuna nini?" Utakuwa ukiendesha gari moja kwa moja, ukizungumza na mtu, mkeo ama rafiki yako ameketi kitini; hawatajibu, hawatakuwa hapo. Utakimbia makaburini, kutakuwako na baadhi ya makaburi yamefunguliwa, hayo mengine yangali yamefungwa, "Kwa maana hao wafu wengine hawakuishi kwa kipindi cha miaka elfu moja." Kumbukeni tu, imekwisha basi!

135 Itakuwa ni kuja kwa siri, hakuna mtu atakayejua itakapotukia. Tumeamriwa kuwa tayari na tukikesha. Hatujui ni wakati gani. Lakini, chochote kile, hatutamzuia yeyote wa hawa *huku* nyuma; kwa maana, mara Yesu atakapotokea, mkesha wote unafufuka. Waliokufa ama walio hai, haijalishi!

136 Hatu—hatukutani na Yeye kwanza, tutakutana sisi kwa sisi kwanza. Biblia ilisema, Waefeso, mlango wa 5, ilisema, "Kwa maana sisi tulio hai na tuliosalia hata kuja kwa Bwana, huku chini, hatutawazuia ama kuwatangulia hao waliokwisha kulala mauti." Hao wa thamani walioitia muhuri damu yao. . .waliotia muhuri ushuhuda wao kwa damu yao. "Hatutawazuia ama kuwatangulia hao waliokwisha kulala, kwa kuwa parapanda italia." Jambo fulani litatukia, "kitu *fulani* cha Injili kitalia," kule kutangazwa kwa kuja Kwake. "Nao waliokufa katika Kristo watafufuka kwanza. Nasi tulio hai na tuliosalia tutabadilishwa." Kusimama, na kuhisi badiliko likija: nywele za mvi zinaondoka, makunyanzi yanatoweka, tutabadilishwa kwa dakika moja, katika kufumba na kufumbua jicho. Ndipo tutakutana na wapendwa wetu kwanza: "Yule pale Mama, Baba, yule pale rafiki yangu. Loo, Haleluya, tuko tayari! Halafu, pamoja na hao waliokuwa wamekufa," yasema Maandiko, "tutatwaliwa juu hewani kumlaki Bwana." Utaratibu wa kule Kuja.

137 Loo, kumwona maskini yule baba yangu! Loo, jamani! Kuwaona maskini wapendwa walioshuka katika Imani huko, kuwalaki. Mnaona utamu wa Mungu, mkijua kama tukikutana Naye kwanza tutashangaa, "Je, Mama alikuwa ndani? Hivi—hivi Mama alifanikiwa hatimaye? Tumehubiri kwa nguvu sana, tu—tulijaribu. Alikuwa hapa? Mjomba Joe yuko hapa? Ndu—ndugu yuko hapa? *Fulani-wa-fulani* yupo?" Mnaona? "Bwana, tunakupenda, tunakupenda, lakini . . ." Kwanza tutakutana sisi kwa sisi! Loo—loo—loo! Hakuna kushangaa juu yake, sote tuko.

138 Si ajabu walisimama na kusema, "Amina, utukufu, na hekima, na heshima, na nguvu, na uweza."

139 Wale wazee ishirini na wanne walitoa taji zao na wakaanguka chini namna hiyo, wote walilala chini sakafuni na kumwabudu Yeye.

140 Moja ya siku hizi tutasimama huko ng'ambo ya nchi, huko juu, mzingo wa dunia, huko ng'ambo mahali fulani hewani; wala hatutakuwa Mbinguni bado, tutanyakuliwa kumlaki Yeye hewani.

141 Wakati Rebeka alipoamua, upesi, akiamua kwamba angeenda pamoja na Eliezeri juu ya ngamia kumlaki Yakobo . . . ama kumlaki Isaka ambaye alikuwa awe mumewe, kamwe hakuwa amewahi kumwona, alijua kwamba Mungu alikuwa akimwongoza. Mwana wa Yakobo, ama . . . Isaka alikuwa akienda zake huko nje kondeni wakati wa jua kupunga. Kumbukeni, ilikuwa ni wakati wa jioni. Naye Rebeka amepanda ngamia. Eliezeri akasema, "Yule pale anakuja sasa." Ndipo Rebeka akaruka akatoka kwenye ngamia, akaondoa utaji usoni mwake. Hakuwa amemwona kamwe. Hakujua . . . Huyo alikuwa ni mumewe, bali yeye hakuwa amemwona. Alikuwa akienda kumlaki kwa imani. (Sijui sura Yake, bali, loo, nitakapomwona!) Huko nje wakati alipomwona, ilikuwa ni mapenzi ya kuonana mara ya kwanza. Wala yeye hakuwa amemwona, kwa hiyo akamwona, mapenzi ya kuonana kwa mara ya kwanza. Nao hawa hapa wanakuja kukutana kondeni. Ndipo akampeleka kuwa ufalme wa baba yake huku na kumwoa.

142 Hivyo ndivyo Kanisa litakavyonyakuliwa hewani, hewani katikati, na kumlaki Bwana wakati akishuka. Loo, litakuwa ni jambo la jinsi gani, mapenzi ya kuonana kwa mara ya kwanza! Ndipo tutakaposimama kule juu ya mizingo ya dunia hii na kuimba nyimbo hizo za ukombozi, loo, jamani! Jinsi tutakavyoimba na kumsifu Yeye kwa ajili ya ninii yetu . . . neema ya ukombozi ambayo ametupa. Wakati Malaika watazifunika du—duara ya dunia kwa vichwa vilivyoimanishwa, pasipo kujua tunayozungumzia. Hao Malaika hawakupotea, hawatajua maana ya kuokolewa. Sisi ndio tuliopotea, sisi ndio. Tutaelewa basi ni kitu cha kuchukiza jinsi gani kilichowekwa mbele zetu,

Naye akatukomboa kwa Damu Yake, kutoka kwa kila kabila, lugha, na taifa. Itakuwa ni siku ya shangwe jinsi gani!

143 Ninaupenda wimbo huo, uliosema:

Kutakuwako na mkutano hewani,
Kwa utamu, kwa utamu hivi karibuni;
Nitakulaki na kukusalimia kule
Katika makazi hayo ng'ambo ya anga;
Uimbaji mzuri sana uliopata kusikika, kusikika na masikio ya mwanadamu,
Itakuwa adhimu, ninatangaza!
Wakati Mwana wa Mungu mwenyewe, Yeye atakuwa ndiye Kiongozi
Kwenye huo mkutano hewani. (Loo!)

Umesikia juu ya mtoto Musa kwenye yale manyasi,
Umesikia juu ya shujaa Daudi na kombeo lake;
Umesikia hadithi ikisimuliwa ya Yusufu aotaye,
Na juu ya Danieli na wale simba tunaoimba mara kwa mara.
Loo, bali wapo wengine wengi, wengi sana katika Biblia,
Nami natamani kukutana nao wote, natangaza! (Hiyo ni kweli!)
Basi ni furaha jinsi gani tutakapokutana nao
Kwenye mkutano huo hewani. (Tunaingojea siku hiyo!)

144 Hao hapo wale mia moja na arobaini na nne elfu wenu wanakuja, wataipokea Injili baada ya sisi . . . hawawezi kuipokea wakati ule ule Nuru ikiwa juu ya Mataifa. Wayahudi wanaikana na kuificha. Sasa, wakati hiyo Nuru . . . Mataifa wananyakuliwa, ndipo Roho anawashukia wawili wapate kuwashuhudia, ndipo Wayahudi wanaipokea, ambao ni mia na arobaini na nne elfu wa makabila yaliyopotea ya Israeli wataipokea Injili; naye Bibiarusi atanyakuliwa.

145 Sasa, kuna "wanawali kumi." Hebu tuiendee Mathayo 21, mara moja. Mnaona, tungali tuna muda mwingi kidogo. Loo, ninaipenda Biblia.

Nitakapochukua likizo yangu Mbinguni,
Jinsi hiyo itakavyokuwa ni safari ya ajabu;
Kusikia burudani za Kwaya ya mbinguni,
Na malango ya ninii yangu . . . uso wa Mwokozi wangu nitauona;
Nikiketi kwenye kingo za ule mto,
Chini ya uvuli wa Mti usiokauka;
Ninataka kutumia likizo yangu Mbinguni,
Hivi hutakuja kuchukua yako pamoja nami?

146 Sasa, katika Ki—Kitabu cha—cha Mathayo Mtakatifu, ninaamini ni mlango wa 25, ninaamini. Nilisema 21, sivyo? Nilikuwa nimeuandika hapa 21, bali hilo ni kosa. Ni 25. Ilinibidi kuharakisha asubuhi ya leo, nilikuwa. . .niliamka nimechoka, na kuchelewa na—nami ni—nilikuwa nikiharakisha. Nilikuwa nikiyaandika tu Maandiko, ndipo nikaandika 21 wakati ni—ni 25.

> *Ndipo Ufalme wa mbinguni utafananishwa na wanawali kumi waliotwaa taa zao, wakaenda kumlaki bwana-arusi.*

147 Sasa:

> *Na watano wao walikuwa wenye busara, na watano walikuwa wapumbavu.*
>
> Na *wale waliokuwa wapumbavu walizitwaa taa zao, wasitwae na mafuta pamoja nao:*
>
> *Bali wenye busara walitwaa mafuta katika vyombo vyao pamoja na taa zao.*
>
> *Hata bwana arusi alipokawia* (hiyo ni katika nyakati hizi za kanisa), *wote. . .wakasinzia wakalala usingizi.*

148 Kote kote safarini, wote wawili wakafa, wakasinzia wakalala usingizi, mnaona, walipokuwa wakishuka kwenda zao. Sasa, hawajapotea, bali "walisinzia tu wakalala usingizi." Wanangojea, mnaona. Hawakusema walikuwa wamekufa, bali "wanasinzia na kulala usingizi." Mnaona?

> *Ndipo usiku wa manane kukawa na kelele, Haya, bwana arusi yuaja; tokeni mwende kumlaki.*
>
> Basi *hao wanawali wote wakaamka, na kuzitengeneza taa zao.*
>
> *Nao wale wapumbavu wakasema—wakawaambia wenye busara, Tupeni mafuta yenu kidogo; kwa maana taa zetu zinazimika.*
>
> *Lakini wenye busara wakajibu, wakisema, Sivyo; yasije yasitutoshe sisi na ninyi: afadhali shikeni njia mwende kwa wauzao mkajinunulie.* (Kunradhi.)
>
> *Na hao walipokuwa wakienda kununua, bwana arusi akaja; na hao waliokuwa tayari wakaingia pamoja naye arusini: mlango ukafungwa.*
>
> Halafu *wakaja na wale wanawali wengine, wakasema, Bwana, Bwana, utufungulie.* (Sasa, mnaona, hawakuwa wasioamini, walikuwa ni watu wazuri.) . . . *utufungulie.*
>
> *Lakini* jibu. . .*Akajibu akasema, Amin, nawaambia, siwajui ninyi.*
>
> *Basi kesheni, kwa sababu hamjui siku wala saa* atakayokuja *Mwana wa Adamu.*

149 Sasa wale wanawali watano wenye "busara." Sasa, *mafuta* katika Biblia yanaashiria "Roho Mtakatifu." Sote tunajua hilo. Hiyo ndiyo sababu sisi huwapaka mafuta wagonjwa, nayo mafuta yanaashiria Roho Mtakatifu. Kwa hiyo wenye busara walikuwa na Mafuta katika taa zao, ambayo yalikuwa ni Roho Mtakatifu, kwa hiyo walikuwa tayari kuingia kwenye Karamu ya Arusi. Nasi tungeweza kurejea katika—katika—katika Ezekieli 9, na kadhalika, na kuvuta na kuonyesha, bali nina kama Maandiko kumi na tano zaidi yaliyoandikwa hapa. Kwa hiyo mafuta hua-. . .Ninaamini tayari tumekuwa nalo katika darasa letu juma hili, kwamba *mafuta* ni, huashiria "Roho Mtakatifu." Sote tunajua hilo.

150 Sasa angalieni, wao. . .wote wawili walikuwa ni "wanawali." Sasa hebu nipate hili. Hapa, hebu tuwachukue hawa wawili papa hapa. *Huyu* ni mwanamwali na *huyu* ni mwanamwali, *huyu* alikuwa ni mwanamwali mpumbavu na *huyu* alikuwa ni mwanamwali mwenye busara, bali wote wawili ni wanawali.

151 Sasa kama utachukua jina hilo *mwanamwali* na kulichunguza, linamaanisha—linamaanisha "mtakatifu, safi, aliyetakaswa." Neno *kutakaswa* linatokana na neno "mtakatifu," ambalo linamaanisha, "safi." Kama vile neno la Kiebrania. . .Sasa, hilo ni neno la Kiyunani, *kutakasa* linamaanisha "safi." Sasa, neno la Kiebrania ni kufanya "takatifu." Mnaona? Nalo letu ni "safi." Sasa, wao wanayachukua hayo maneno matatu, kwamba kila neno lina maana ile ile bali linasemwa tofauti, kama vile ne—neno "safi, takatifu, lililotakaswa," yote matatu ni neno lile lile.

152 Kama vile tulikuwa tuzungumze neno kama *mbwa*. Ningesema "mbwa," hicho ni Kiingereza. Kama ningelisema *mbwa* katika Kijerumani, Fred, ni "hund." Hiyo ni kweli? Ndugu Norman, kama nikisema *mbwa* katika Kihispaniola, ni "ajo." *Ajo*, *Hund*, na *dog* yote ni *mbwa* kwetu, mnaona. Mnaona, ni—ni ninii tu, msemo.

153 Kwa hiyo, neno la Kiyunani la *safi* ni "takasa," neno la Kiebrania ni "takatifu." Takatifu, safi, na takasa, yote ni neno lile lile. Kwa hiyo hili halikuwa ni kanisa lenye kinyaa, chafu; lilikuwa ni kanisa lililotakaswa, safi, "*wanawali* kumi walitoka kwenda kumlaki Bwana-arusi." Hilo lina maana gani? *Makanisa* haya yote. Sio. . .sasa, sio *hapa* chini katika Warumi; bali chini katika madhehebu, Wanikolai. Baptisti inahubiri juu ya Kuja kwa Pili kwa Kristo; Methodisti inahubiri Kuja kwa Pili kwa Kristo; Presbiteri inahubiri Kuja kwa Pili kwa Kristo; Nazarayo inahubiri Kuja kwa Pili kwa Kristo; Pilgrim Holiness inahuburi Kuja kwa Pili kwa Kristo. Hiyo ni kweli? "Wote walitoka kwenda kumlaki Bwana arusi." Sasa m—mnakumbuka ya kwamba kila mmoja wao alikuwa akienda zake kumlaki Bwa—Bwana-arusi.

Sasa, kama Mungu huheshimu hilo tu, basi Yeye angeninii, angewachukua hao pia.

154 Lakini mnakumbuka jambo lile lile, jinsi ambavyo ule mfano hivi majuzi usiku, wakati Mungu alinena nasi katika wakati wa kanisa na kusema ya kwamba "Balaamu, fundisho la Balaamu." Sasa, huyu hapa Balaamu alisimama, ambalo lilikuwa ni taifa zuri, kubwa mno lenye utaratibu. Nao walikuwa waaminio wa Mungu, kwa kuwa angalia yale Balaki aliyofanya aliposhuka kule . . . Balaamu, hasa. Yeye alitoa dhabihu ile ile kwa Mungu yeye yule ambaye Israeli walikuwa naye, Mungu wa Israeli, Yehova. Naye alifanya madhabahu saba. Saba ni namba kamilifu ya Mungu.

155 "Siku sita Yeye alifanya kazi, na ya saba akapumzika," hiyo ni kamilifu, mnaona, saba. Siku sita amefanya kazi ulimwenguni. Miaka ya kwanza elfu mbili, uliangamizwa kwa maji; miaka elfu mbili ya pili, Kristo akaja; na hii ni miaka elfu mbili ya tatu. Mwishoni mwa kila miaka elfu mbili, jambo fulani hutukia, ulimwengu hutikiswa tena. Katika miaka elfu sita, Yeye aliumba ulimwengu; miaka elfu sita kanisa linafanya kazi dhidi ya ulimwengu; na elfu ya saba ni ule Utawala wa Miaka Elfu. Mnaelewa sasa?

156 Sasa, kanisa lina Nyakati Saba za Kanisa, pia. Mungu . . . Na hiyo ni namba kamilifu ya wakati wa kanisa, hizo tu, saba. *Saba* ni nambari kamilifu ya Mungu. Nyakati Saba za Kanisa, miaka elfu saba ya uumbaji, kila kitu kinashughulika katika saba.

157 Sasa, kulikuwako na wanawali waliotoka kwenda kumlaki. Nao wale wanawali "wapumbavu," sasa, hawakuwa na Mafuta kwenye taa zao, bali walikuwa na kila kitu kingine: walikuwa safi, walimwamini Kristo; walilihubiri Neno waliloliamini, lile dhehebu lao lingewaruhusu kuhubiri, walihubiri hilo, Kuja kwa Pili, Dhabihu, Upatanisho. Wanaamini. Ukipata kukabiliana na mwanachuoni mzuri wa Kibaptisti wakati mmoja, (huh) afadhali ujue kile unachozungumzia, uhu-huh, ndivyo hakika.

158 Lakini, mnaona, "Karibu sana," ilisema Mathayo 24, Mathayo 24:24; isome mara moja nawe utaona. Yesu alisema ya kwamba katika siku hizi za mwisho roho hizo mbili zingefanana sana hata ingewapoteza walio Wateule kama yamkini. Zitafanana sana hata zitawashawishi Wapentekoste haraka sana. Hakika! Sasa, Mathayo 24:24, kuna mtu aliye nayo? Sikuipata papo hapo. Unayo pale, dada, ama baadhi yenu? Mathayo 24. Unayo, Ben? Vema, isome.

> [Dada mmoja anasoma: *Kwa maana watatokea* Wakristo *wa uongo, Makristo wa uongo—wa uongo—* Mh.] *Makristo wa uongo!* [*na manabii wa uongo*,] *Manabii wa uongo*! [*nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule*.]

159 Haya basi. Sasa, ni akina nani watatokea? Watatokea Makristo wa uongo, watu wa uongo wakisema, "Mimi ni wa Kristo." Manabii wa uongo, wakisema, "Mimi ni *hiki* na mimi ni *kile*." Nao karibu watawapoteza walio Wateule kama yamkini. Na kuna njia moja tu ambayo unaweza kuokolewa kamwe, hiyo ni wakati ulichaguliwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu; hiyo ni, Mteule, kwa kujua tangu zamani, jina lako liliwekwa kwenye kile Kitabu huko nyuma. "Ishara kuu!"

160 Sasa yaangalieni makanisa haya mawili. Loo, laiti ningaliweza... laiti kungalikuwako na njia ya kuwafanya watu walione. Linawaka tu moyoni mwangu! Hii... makanisa *haya* ni safi tu na matakatifu kama *hili*; kama wote ni wanawali, wote ni wanawali, safi tu *vivyo hivyo*. Tofauti pekee ilikuwa—ilikuwa ni yale Mafuta kwenye taa, Roho Mtakatifu. Naye Roho Mtakatifu, akiwa mle ndani, anatoa moto wa namna ile ile aliotoa huko Pentekoste. Bali hawana moto wowote, hawana Mafuta kwenye taa zao. Wana taratibu za ibada za kanisa, kanisa lenye taratibu za ibada li—liwezavyo kuwa, sherehe za kupendeza (hakuna neno dhidi yake), kanuni za imani ambazo zingeitikisa dhamira yako, na nyimbo kama Malaika wakiimba. Nao ni... utaninii... kuweka kidole chako kwenye ninii yako... maisha yao, usingeweza kufanya hivyo. Lakini hilo lingali ni makosa! Si... ni—ni sehemu Yake, bali si yeye *Wote*. Watu kama hao ndio wanaoukosa Unyakuo. Mnaona? Wao ni ninii tu...

161 Sasa angalieni. Huyu hapa Moabu akishuka. Nitaliweka papa hapa kama mnaweza kuliona. Huyu hapa Moabu, dhehebu kubwa, nitaandika hapa "*wa*" madhehebu; hawa hapa Israeli, "bila" madhehebu. Huyu hapa Moabu, akaweka hapa madhabahu moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba; Israeli walikuwa na madhabahu moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba. Vema. Moabu hapa juu waliweka fahali mmoja, wawili, watatu, wanne, watano, sita, saba; Israeli, mmoja, wawili, watatu, wanne, watano, sita, saba. Vema. Moabu walisema, "Wakati unakuja ambapo kutakuwa na mtu (Kristo) atakuja duniani, kwa hiyo Yeye atakuwa ni Mwana-kondoo wa Mungu aondoaye dhambi ya ulimwengu, tutaweka saba" (ati nini?) "wana-kondoo kwenye madhabahu hii"; Israeli wakasema, "Hiyo ni kweli kabisa, wana-kondoo saba madhabahuni." Mnaona?

162 Sasa, huko mwanzoni kabisa, Kaini aliweka madhabahu, akatoa dhabihu, akaabudu, akafanya kila kitu ambacho Habili alifanya, pasipo... (Loo, lipokeeni!)... pasipo na ufunuo wa Mungu, ambapo, Kanisa lote limejengwa juu ya ufunuo huo. Yesu alisema hivyo, "Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu." Ukweli wa Uungu mkuu wa Yesu Kristo uliofunuliwa kiroho, "Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu."

163 Sasa, kama Mungu anaheshimu tu taratibu zenu, taratibu zenu za ibada, kama Wamethodisti, Wabaptisti, Wapentekoste,

na kadhalika, kama hilo tu ndilo analowatarajia kufanya, kuhubiri kule Kuja mara ya Pili na mambo haya mengine yote (ambayo, ni ya Kimaandiko kabisa), kama Baptisti, Presbiteri, na kadhalika wafanyavyo, basi Mungu anawajibika kuyachukua yote mawili maana hayo tu ndiyo aliyohitaji. Lakini, mnaona, pasipo na ufunuo, hao *hapo* wanawali waliolala; hawa *hapa* wanawali wenye busara. Walikuwa ni dhehebu, taifa kuu.

164 Tulisoma hivi majuzi usiku, ambapo lilisema, "Watu hawa hawatakuwa dhehebu, watakuwa wenye kutanga-tanga kote nchini, wakiishi katika mahema, maskini, wanyenyekevu." Lakini kasema, "Kamwe usijaribu kuwalaani, maana niko pamoja nao." Sasa angalia! Watu hawa wanaamini katika taratibu za ibada zile zile hao walizoamini, na kumwabudu Mungu yule yule. Mnaona? Bali hawakuwa na ishara na maajabu yakiwafuata! Israeli walikuwa na Nyoka ya Shaba, Mwamba uliopigwa, furaha ya Mfalme, uponyaji wa Kiungu, manabii, kila kitu papa *hapa* chini. Nao hawakuwa nayo, walikuwa na taratibu za ibada bila—bila baraka, Mafuta.

165 Jambo lile lile na mwanamwali aliyelala na mwanamwali mwenye busara, wote wawili walikuwa ni watu waliotakaswa. Ila *huyu* alikuwa na Mafuta. Naye *huyu* hakuwa na Mafuta, kwa hiyo wakasema, "Sisi ni wema tu kama mlivyo ninyi." Hiyo ni...Hakuna mmoja wetu aliye mwema, kuhusu hilo. "Mbona, ninyi ni kundi la watakatifu wanaojibingirisha!" Vema, hilo ni sawa, uh-huh, hilo ni sawa. Hakuna mmoja wetu aliye mwema, sote tulitenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. Lakini njia pekee utakayolijua, sio kwa kujiunga na kanisa, sio kwa kujaribu kuishi vema, bali unapompokea Kristo. Si yale ninayoishi; ni kile alichokuwa Yeye. Si kile nilicho mimi; ni kile alicho Yeye. Yeye alifanyika mimi ili mimi niweze, kwa neema Yake, kuwa Yeye, mwana wa Mungu. Mnaliona?

166 Sasa, mwanamwali aliyelala, na mwanamwali mwenye busara aliye na Mafuta kwenye taa yake. Sasa, mara ghafla, sauti ikaja, "Haya, Bwana-arusi yuaja, tokeni mwende kumlaki!" Nao wakaamka. Bali walipoamka, *huyu* angeingia maana walikuwa na Mafuta kwenye taa zao. Hiyo ndiyo iliyokuwa tofauti.

167 *Huyu* asingeweza kuingia, ambapo hapakuwapo na Mafuta kwenye taa; walirudi wapate kuomba vya kutosha, kumpokea Roho Mtakatifu. Lakini, wakati walipokuwa wameondoka, yote yakaisha. Madhehebu yanasema, "Vema, labda tumekuwa makosani. Labda afadhali turudi, tukautafute ubatizo wa Roho Mtakatifu." Hivyo ndivyo wanavyojaribu kufanya sasa. Mliona hilo? Wapresbiteri...Simamisheni kanda yenu kwa dakika moja, sitaki kulitaja jina hili. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] ...?...Bwana-arusi akaja. Na, vema, kuja Kwake kumekaribia jinsi gani, basi, wakati watakapojaribu sasa kununua! Vema, fungulieni kanda yenu, Gene. Sasa, mnalipata? "Walipoenda

kununua," wanajaribu kununua sasa, makanisa yote yanajaribu kuwa na uamsho, uamsho; ni kujaribu kurudi.

168 Sasa, hata kwa Dk. Billy Graham, aliandika katika *Mbiu ya Imani,* mliiona, kutoka Chicago, na kusema kuwa "Hatuwezi kuipuuza huduma ya Kipentekoste." Mnaona? "Hatuwezi . . .-wapuuza, kwa sababu walikuwa na waongofu zaidi katika mwaka mmoja kuliko makanisa mengine yote yakiwekwa pamoja."

169 Huo ni moto huo hasa ukiwaka, ukitikisa, ukikusanya, ukitupa wavu ndani na kuvuta. Na unapotupa wavu . . . Yesu alisema, "Ufalme wa Mungu ni kama mtu aliyeenda na kutupa wavu baharini, ndipo wakati alipovuta, alikuwa na kasa, nyoka, vyura, majoka, kadhalika, bali alikuwa na samaki, pia." Hivyo ndivyo ujumbe wa Pentekoste unavyofanya, unaenea upesi sana duniani; kuitupa ndani na kuivuta, tunapata kasa, kamba wa maji baridi, kamba, viluwiluwi, mbwa-maji, vibisi, na kila kitu kingine mle ndani. Lakini jambo ni kwamba, kunao samaki mle ndani, pia. Hao ndio walio wa Bwana.

170 Vema, kwa baadhi yenu ndugu waaminio washika sheria kwenye kanda hii, mngetaka kuichoma moto: Hao walifanyika samaki lini? Wakati wavu ulipowafunika? Walikuwa samaki hapo mwanzoni! Hiyo ni kweli. Waliteuliwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu! Ni kwamba tu hawajapata kuingia wapate kutumiwa na Bwana.

171 Huyo hapo chura wako. Ukimchukua chura mkubwa na kumtupa ufukoni, atafanya tu "whop, whop" moja kwa moja anarudi majini.

172 Naye maskini kamba wa majini anayeketi pale, aseme, "Aha, hao ni kundi la watakatifu wanaojibingirisha." Huyo anarudi, "Aha—aha—aha—aha. Loo, la!" Anarudi moja kwa moja matopeni upesi awezavyo kwenda. Hiyo ni kweli.

173 Maskini nyoka akitambaa kidogo na mlio wake, "Ninaamini siku za miujiza zimepita, Daktari *Fulani-wa-fulani* na *Fulani-wa-fulani* waliniambia." Kasema, "Aha—aha—aha—aha—aha—aha—aha, huwezi kunipumbaza!" Huyo hapo anaondoka, moja kwa moja kule tena, mnaona.

174 Nyoka, tangu mwanzo! Chura, tangu mwanzo! Paulo alisema katika Biblia, wa aina hiyo, alisema, "Walitoka kwetu kwa sababu hawakuwa wa kwetu tangu mwanzo." Mnaona? Uhum! Vema, mwanamwali mpumbavu.

175 Mwanamwali mwenye busara mwenye Mafuta katika taa yake, alijifanya tayari.

176 Sasa, "alipokuwa ameenda kununua Mafuta," hivyo ndivyo wanavyojaribu kufanya sasa hivi. Makanisa haya makuu ya kiinjilisti, wakijaribu kupata mambo haya makuu, mwajua, na kufanya . . . kurudi kwenye Biblia, kurudi, "tunahitaji Baraka za

Kipentekoste." Mbona, mnaweza kuwazia watakuwa na ibada ya namna gani, mnaona. Hawatashuka waende pale na kuharibu rangi zao za makucha, na yote hayo. Loo, la. Hawataachana na hivyo vilabu vya mashoga na mashirika na vitu kama hivyo. Wakiushikilia ulimwengu kama Esau, katika mkono mmoja, wakijaribu kumshika Mungu kwa huo mwingine. Huwezi kufanya hivyo. Huwezi kuwa Mkristo mwenye makengeza, wajua, ukimwangalia Mungu na ulimwengu pia. Inakubidi kujiweka umelenga Kalvari, ukae papo hapo na Hilo.

177 Sasa, lakini hao hapo wanaenda, nao wanajaribu kurudi. Basi kumbukeni jinsi tulivyo karibu! Wakati ule ule walioenda kununua, hapo ndipo Bwana-arusi alipokuja.

178 Loo, Ndugu Stricker, tumekaribia! Tuko karibu sana na Nyumbani. Loo, moja ya asubuhi hizi:

> Baragumu yake Bwana wakati ikipigwa, na wakati hautakuwapo tena,
> Nayo asubuhi ipambazuke ya Milele, angavu na nzuri;
> Hapo watu Wake waliookoka duniani watakapokusanyika Nyumbani mwao ng'ambo ya anga,
> (Huo utakuwa ni wakati wa jinsi gani!)

179 Naam, mwanamwali aliyelala. Ataninii . . . Huyu mwanamwali aliyelala sasa, mnataka kujua kitakachompata. Sivyo? Jambo moja ninalotaka kuelezea. Itakuwaje kwa makanisa haya? Itakuwaje kwa watu hawa waliotembea sehemu moja ya safari pamoja na Kristo, wala hawakuja, ama hawakumfuata Kristo hadi mwisho?

180 Sasa katika Warumi, ninaamini, 2:22, Biblia ilisema, Paulo alisema, "Ikiwa Roho wa Mungu hayuko ndani yako, wewe si wa Mungu." Wewe ni wa dhehebu bali si wa Mungu. Kama Roho wa Mungu hayuko ndani yako, wewe si wa Mungu. Mnaona. Inakupasa kuwa na Roho wa Mungu upate kuwa wa Mungu. Hakika!

181 Vema, bwana, "ile Dhiki Kuu." Sasa, sasa kama . . . Itawabidi kupitia . . . Sasa, mnakumbuka, Yeye alisema . . . Sasa hebu nipate hayo mengine, "Walitupwa kwenye giza la nje, na huko kungekuwa na kulia, kuomboleza, na kusaga meno." Vema, hiyo ni ile Dhiki Kuu. Sivyo? Ile Dhiki Kuu! Sasa, baada ya Dhiki hii, hao watu . . .

182 Sasa, hebu nilishike tena hapa, ni wale masalia. Sasa angalieni! Hiki *hapa* kitambaa. Vema, huyo mama anakiweka namna *hii*. Sasa atajitengenezea kitu fulani, mwajua, namna fulani ya vazi. Sasa, hiki ndicho chote—kitambaa chote alicho nacho. Sasa, kila sehemu yake ni kitambaa cha namna ile ile. Hiyo ni kweli?

183 Wote wawili walikuwa ni wanawali. Mnaona? Vema. Walikuwa na imani katika Kristo, mfano wa utauwa, wakaenda kanisani, wakafanya mambo mazuri, fadhila, hakuna kitu kingaliweza kusemwa juu ya kazi zao na kadhalika. "Nayajua matendo yako," Yeye alisema katika kila wakati. "Nayajua matendo yako, bali hata hivyo umepungukiwa." Unaona?

184 Sasa, wakati mwanamke. . . yeye huamua niani mwake jinsi ameliweka bombwe lake hapa, naye anaamua niani mwake jinsi atakavyokata bombwe hili, mahali litakapokatiwa. Hiyo ni kweli? Vema, yeye huchukua kile anachofikiria kimemtosha na sehemu iliyo bora sana ya—ya hilo bombwe. Hiyo ni kweli? Maana chote ni kitambaa kile kile, lakini labda anakiweka *hivi* ama *vile*, anakiweka chini. Ndipo anachukua makasi na kukikata. Sasa, kile kilichosalia kinaitwa "masalia." Vema. Sasa, bombwe hili ni nini? Lilijulikanaje? Na yule. . . mahali ambapo mama huyu alichagua kukatia.

185 Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, Yule aliyejua mwisho tangu mwanzo kwa kutangulia kujua, Yeye *alitenga* mahali pa kukatia. Alijua tofauti kati ya Esau na Yakobo. Alijua tofauti kati ya mwenye dhambi na mtakatifu. Yeye alijua tofauti. Anajua kusudi la kila moyo, kwa hiyo alituteua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu na kuweka majina yetu katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo; na pia Mwana-Kondoo aliyekuwa achinjwe (na kuandika majina yetu *kabla* Yeye hajachinjwa), nayo Biblia ilisema ya kwamba Kristo alikuwa Mwana-Kondoo aliyechinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Nayo majina yetu yaliwekwa katika Kitabu hicho wakati Yeye—wakati Yeye alipoteuliwa huko nyuma kuwa Mwana-Kondoo atakayechinjwa, tulichaguliwa kuwa wale ambao Yeye alichinjwa kwa ajili yao. Mnaliona?

186 Sasa, wote ni wanawali. Sasa, haya *hapa* maskini masalia, hayatupwi. Loo, la. Yeye huyaweka, bali anayaweka kando, anaweza kuyatumia kwa kitu kingine. Mnaona? Bali hakitatumika *pale*, hilo ni Kanisa lililokatiliwa mbali. Sasa, itawabidi kuistahimili hukumu (kwa sababu wanapitia kwenye ile Dhiki), hao ndio masalia. Sasa mnalipata?

187 *Hili* hapa Kanisa linaenda, Nyumbani, linaenda Nyumbani. *Hawa* hapa masalia waliosalia. Na hawa *hapa* mia na arobaini na nne elfu juu ya Mlima Sinai, Wayahudi. Sio bibi-arusi watatu mbalimbali. Huh! Ni Bibi-arusi; wale masalia; na wale mia na arobaini na nne elfu. Kweli kabisa. Yeye hakuwa akila chochote ila Chakula cha Roho Mtakatifu kule nje, nadhani, kwa hiyo alikuwa sawa, Yohana hakuwa na kasoro. Mnaona? Basi hao—hao hapo.

188 Sasa, mwishoni mwa wakati, ni wangapi wanaojua ya kwamba Biblia inasema ya kwamba "watakatifu wataihukumu dunia"? Paulo alisema hivyo. Hebu tufungue sasa kwenye—

kwenye Kitabu cha Danieli na tukipate kile Kiti Cheupe cha Enzi. Tungekipata katika Ufunuo bali ninapenda kukichukua kutoka Danieli, ni kitu kile kile. Danieli 7, nasi tutaipata ile—ile Hukumu ya Kiti Cheupe cha Enzi hapa. Hebu tuanzie kwenye kifungu cha 8 cha mlango wa 7 wa Danieli:

> Nami *nikaziangalia sana pembe zake, na tazama, pembe nyingine ikazuka kati yao, nayo ilikuwa ndogo, ambayo mbele yake pembe tatu katika zile za kwanza zikang'olewa kabisa:* (Sasa, tunajua tuko Rumi pale, sasa. Mnaona?) *na tazama, katika pembe hiyo mlikuwa na macho . . . ya mwanadamu,* (Sasa, kumbukeni, pembe hii haikupokea taji, ilikuwa ni kitu cha kijanja. Pembe hizo zingine ziligeuka kuwa wanyama. Hiki kilikuwa ni kitu cha kijanja, ilikuwa ni mwanadamu, papa badala ya upagani, mnaona.) *na kinywa kilichokuwa kikinena maneno makuu.*

189 Sasa tazama, kifungu cha 9:

> *Nikatazama* hata *viti vya enzi vikawekwa,* (Hiyo ni kwamba falme zote za Mataifa zimekwisha. Huyu nabii ananena. Sasa kumbukeni, kila moja ya mambo hayo aliyosema yametukia moja kwa moja hata kufikia kwenye kitu hiki cha mwisho, tunajua hayo kwa historia yetu ambayo tunachukua.) . . . ambaye . . . a—*alitupwa chini, na mmoja aliye Mzee wa siku ameketi,* mavazi *yake yalikuwa meupe kama theluji*, (Mnajua huyo alikuwa nani hivi majuzi usiku katika lile ono? Yesu.) *na nywele za kichwa chake* zilikuwa *kama . . . sufu safi;* na *kiti chake cha enzi kilikuwa miali ya moto, na magurudumu yake kama moto uwakao.*
>
> Na *mto kama wa moto ukatoka ukapita mbele zake;* maelfu mara *maelfu wakamtumikia,* (Hilo hapo Kanisa limerudi pamoja Naye, mnaona.) *na* makumi elfu *mara* makumi elfu *wakasimama mbele zake;* (*Huyo ni Bibi-arusi akija, na walimwengu wengine.*) na *hukumu ikawekwa, na vitabu vikafunguliwa.*
>
> . . . *hukumu ikawekwa, na vitabu vikafunguliwa.*
>
> Nami *nikawatazama kwa sababu ya sauti ya yale maneno makubwa iliyosema ile pembe;* nami *nilitazama* hata *mnyama yule akauawa, mwili wake ukaangamizwa, akatolewa ateketezwe kwa* moto.
>
> Na *kwa habari za wale* wafu *wengine*, ambao *mamlaka yao imeo-* . . . (Namaanisha); *wale wanyama* (namaanisha), *mamlaka yao iliondolewa* kutoka kwao: na *maisha yao yakadumishwa kwa wakati na majira.*

190 Sasa, hukumu iliwekwa na Vitabu vikafunguliwa. Hapo ni wakati Bibi-arusi anaporudi na kuketi kwenye hukumu, na Kanisa lililoteuliwa . . . Kanisa lililonyakuliwa litarudi baada ya

hiyo miaka mitatu na nusu, na baada ya huo wakati . . . Na katika Ufunuo inasema, ilisema kwamba—kwamba hao—hao "wafu wengine hawakuishi tena kwa muda wa miaka elfu." Ninyi, ni wangapi wamelisoma? Mara nyingi, nyingi sana. "Hawakuishi tena kwa muda wa miaka elfu." Yesu anarudi pamoja na Bibi-arusi, pamoja na Bibi-arusi.

191 Sasa kumbukeni, kama nilivyosema, kila kitu kiko katika *tatu*. Kuja Kwake kuko katika tatu: mara ya kwanza, Yeye alikuja kumkomboa Bibi-arusi Wake; mara ya pili, Yeye yuaja kumnyakua Bibi-arusi Wake. Kama uhusiano wa mapenzi, anakuja huku na kumwiba usiku, anamtwaa kutoka ulimwenguni, "kumlaki hewani." Kule kuja kwa siri kwa Bwana, mnaona. Mara ya pili ajapo, ni kumpokea Bibi-arusi Wake. Mara ya kwanza, kumkomboa, mara ya pili, kumpokea; na mara ya tatu, pamoja Naye. Mfalme na Malkia!

192 Na huyu hapa anarudi kwa ajili ya hukumu juu ya mataifa. Paulo alisema, "Yeyote wenu ninyi nyote atathubtu kwenda kotini aliye na jambo dhidi ya mwingine? Hamwezi kuyashughulikia mambo haya madogo, hivi hamjui ya kwamba watakatifu watauhukumu ulimwengu?" Hii hapa hukumu iliyokuwa imetolewa kwa Kristo na upande Wake; hao ndio mawakili kizimbani, na Yeye huyo hapo ameketi kwenye Kiti cha Enzi. Huyu hapa Bibi-arusi, wakili.

193 Na hawa hapa wanakuja. Vitabu vilifunguliwa, na Kitabu kingine ambacho ni Kitabu cha Uzima.

194 Sasa, kile Kitabu cha kwanza kilikuwa ni Kitabu cha mwenye dhambi, aliyetupwa nje. Vema. Kwanza kabisa yeye amehukumiwa. Hao hapo—hao hapo wale mbuzi. Yeye hana nafasi, mnaona, kwanza kabisa yeye ni mwenye dhambi. Vema, sasa, yeye anatupwa nje.

195 Na kwa kondoo, walistahimili hukumu. Iliwabidi kuhukumiwa, nao watakatifu iliwabidi kuwahukumu. Mungu si dhalimu. Kama kafiri huko nchini, nasi tunajenga madhabahu ya dhahabu ya dola milioni nane na kumi hapa Marekani badala ya kuupeleka Ujumbe kwao huko, Mungu atatuwajibisha, bali atawaachilia. Hakika! Mungu si dhalimu.

196 Ni—ninyi hapa, endapo hamjawahi kuuona Huu hapo awali, hu—huenda msiwajibishwe, bali mnawajibika sasa! Mnaona? Nyote mnawajibika . . . Nasi tunawajibika kuupeleka huu Ujumbe, wewe unawajibika kama utausikia ama hutausikia.

197 Sasa, makafiri watainuka, hao watu walio huko nje wakiabudu madhabahu. Hawajui bora zaidi. Hawajui lolote kulihusu. Mungu si dhalimu, Yeye asingewahukumu isipokuwa walikuwa na nafasi. Nao watapewa mahali.

198 Na kwa hiyo Kanisani, kwamba kila wakati kupitia kwenye wakati huu wa kanisa, kuanzia—kuanzia kwa Efeso na kushuka kufikia *hapa* chini, ule Ujumbe, Ujumbe wa kweli wa Kristo

kama ulivyokuwa hapo mwanzo (ubatizo wa Roho Mtakatifu, zile nguvu, ufufuo, kunena kwa lugha, kufasiri lugha, karama za uponyaji, ubatizo katika Jina la Bwana Yesu, mambo hayo yote aliyofundisha), kila mmoja aliye katika Bibi-arusi huyo atasimama kama wakili.

199 Hii hapa kesi ya mtu fulani inakuja: "Ulikuwa na mkutano kwa *Fulani-wa-fulani*, ulimwambia?"

200 Sasa huyo wakili: "Naam, nilimwambia." Lile pale kwenye Kitabu, huwezi kulikana, hata mawazo yetu yako juu ya Hilo. Mnaona? Huwezi kulikana. "Naam, nilimwambia ya kwamba hana budi kubatizwa."

"Huko Jeffersonville, kule maskanini, kule?"

"Naam, Bwana, mimi—mimi . . . Wewe . . . "

201 "Naam, hili hapa kwenye Kitabu, uliwaambia ya kwamba *hawana budi* kufanya hivyo. Hata waliyatafuta Maandiko wakaona ilikuwa ni kweli, bali hawakufanya hivyo."

202 "Ondoka Kwangu, ewe mtenda maovu, hata sikukujua." Mnaona?

203 Hapo ndipo Yeye atakapowabagua mbuzi na kondoo, mnaona, awatupe mkono Wake wa kuume na wengine mkono wa kushoto. Hayo hapo matabaka yako matatu yanarudi tena.

204 Lakini, tabaka *hili* kamwe halitakuwa pamoja na tabaka *lile*, huyo ni Bibi-arusi. Pia, mnaona, Bibi-arusi yuko pamoja na Yeye Hekaluni. Hao wengine wanafanya kazi na kuleta utukufu wao kwenye huo Ufalme, ila Bibi-arusi yuko pamoja na Bwana-arusi sikuzote. Hao wengine kamwe hawatagawiwa; kama *hawa* hapa chini, watatumika, hawatatupwa nje, kwa sababu Yeye aliwabagua kama kondoo kutoka kwa mbuzi. Lakini yeye . . .

205 Lakini mbuzi hakuwa na ufahamu Wake, yeye hakuujali. Yeye alikuwa ni mbuzi, na akaridhika kama mbuzi, na kwa hiyo yeye alikufa tu kama mbuzi na huo ukawa ndio mwisho wake. Hivyo tu, mnaona.

206 Lakini kondoo, kama yeye . . . endapo Mungu atashikilia ya kwamba nilikuwa nimesimama pale na makafiri ambao hawajapata kusikia chochote. Kwa hiyo kama ukiihubiri Injili hii kwa watu . . .

207 Nami inanibidi kusimama. Hivi hamkumbuki katika kule kuhamishwa kukuu alikonipa sio muda mrefu uliopita, ya kwamba sina budi kusimama kule na watu hao na—nami ningewajibishwa kwa ajili yao? Nami nikawaona hao mamilioni wamesimama pale, nikasema, "Hivi hawa wote ni wa Branham?"

Kasema, "La." Kasema, "Hao ni waongofu wako."

Ndipo nikasema, ni—nikasema, "Ninataka kumwona Yesu."

Akasema, “Bado. Itachukua muda kabla Yeye hajaja. Ila atakuja kwako kwanza nawe utahukumiwa kwa Neno ambalo ulihubiri, nao wanategemea Hilo.”

Nikasema, “Itabidi wote wafanyiwe hivyo? Itambidi Paulo kusimama?”

Akasema, “Naam, Paulo atasimama pia, pamoja na kundi lake alilolihubiria.”

Nikasema, “Nimehubiri Ujumbe ule ule aliohubiri.”

208 Basi hao mamilioni wakainua mikono yao na kusema, “Tunatumainia hilo!” Haya basi, mnaona, papo hapo! Naam. Kasema, “Ndipo sote pamoja tutarudi duniani kuuchukua mwili unaoweza kula, na tunywe, na kuishi pamoja katika nyakati zote zisizo na mwisho kule.” Huko ni kule kuja kwa Bwana. Vema.

209 Sasa, hebu kidogo. Sasa, kwenye . . . Kidogo inakaribia sasa, maana karibu inafikia kwenye . . . wakati wa ndugu yetu hapa kwa ajili ya ibada ya ubatizo ama chochote atakachotumia.

210 Vema, sasa, kwenye wakati huu wa kanisa. Loo, hili hapa jambo fulani la kupendeza sana. Ninalipenda hili vizuri sana. Kwenye nyakati hizi za kanisa, kuna roho mbili zinazotenda kazi karibu moja kwa moja kupitia *hapa*; moja ni ya kimadhehebu, hiyo nyingine ni Roho Mtakatifu. Naye Yesu alisema, “Zilifanana sana hata zingewapoteza walio Wateule kama yamkini.” Hizi roho mbili zinawatia alama watu wao kwa ajili ya hukumu ya siku za usoni. Shetani aliahidi ya kwamba ninii yake . . . ya kwamba atakuwa na wengi kuliko Kristo, naye anao. Sasa, angalieni hili kwa makini sana, sana sasa tunapolifikia hili: kuliko vile Hilo—Hilo lingekuwa, akiwatia watu alama.

211 Wengi wako kama Hawa. Hawa alisimama tu muda mrefu vya kutosha kudanganywa. Kama asingalisimama, kamwe kusingekuwako na udanganyifu wowote. Lakini Hawa alisimama, na aliposimama, hapo ndipo alipopata kudanganywa kwake. Badala ya kushikilia na . . . Hivi—hivi mnanifuata—mnanifuata kwa makini sasa? Sikilizeni! Sababu ya Hawa kudanganywa . . . Hebu tuliseme pamoja, kusudi niwe na hakika mmelipata. [Ndugu Branham na kusanyiko wanazungumza kwa pamoja—Mh.]: “Sababu ya Hawa kudanganyika, kamwe hakutii Neno lote la Mungu.” Shetani alimnukulia, bali hakumwambia Ukweli *wote*. Wala madhehebu yake hayamwambii. Mnaona? Lakini yeye alikaa muda mrefu kutosha kupata sehemu ya Neno, wala hakulichukua Neno *lote*.

212 Na hiyo ndiyo shida siku hizi, mwanamwali aliyelala alikaa muda mrefu kutosha kupata sehemu ya Neno bali si Neno *lote*. Kanisa lililodanganyika hukaa muda mrefu kutosha kupata sehemu ya Neno bali si Neno *lote*, nao walikuwa ni waaminifu na wakweli kulihusu. Hawa alidanganyika! Biblia ilisema, “Alidanganyika.”

213 Adamu hakudanganyika. Adamu alijua kabisa alikuwa akifanya makosa; bali mkewe, akifanya mambo aliyokuwa akifanya, akimshawishi ku—kula yaliyokataliwa. Mbona, yeye alikuwa ni mwanaume, mnaona, na i—ilikuwa hivyo kwake hata yeye...Mnaelewa, mnaona. Yeye alijua alikuwa anakosea, bali Hawa alidhani alikuwa akifanya mema.

214 Loo, hivi hamwoni? Hiyo ndiyo sababu Paulo alisema ya kwamba mwanamke kamwe hapaswi kuihubiri Injili. Uh-hum. Alikuwa—alikuwa katika...Yeye ndiye aliyedanganyika. "Simruhusu mwanamke kufundisha, wala kutwaa mamlaka yoyote, bali awe mtulivu." Mnaona? "Kwa kuwa—kwa kuwa Adamu aliumbwa kwanza, halafu Hawa. Wala Adamu hakudanganyika, bali mwanamke alidanganywa, akawa makosani." Kasema, "Hata hivyo, sasa, yeye hajapotea; ataokolewa kwa kuwazaa watoto (kama yuna mume), na kadhalika, akiendelea mbele, imani na kiasi na utakatifu wote pamoja na mambo kama hayo, yeye ataokolewa. Lakini kamwe msimruhusu mmoja kufundisha wala kuchukua mamlaka!" Mnaona? Paulo alisema, "Msifanye hivyo!" Kasema, "Sasa, nafikiri ninayo nia ya Bwana," akasema.

215 Wao walisema, "Mbona, ninii...Mbona, manabii huko walitabiri na kutwambia ya kwamba 'tunapaswa kuhubiri.'"

216 Yeye akasema, "Au je? Neno la Mungu lilitoka kwenu, na hivi lilikuja kutoka kwenu peke yenu? Kama mtu yeyote akijiona kuwa ni wa kiroho ama nabii, na atambue ya kwamba yale nisemayo ni Amri za Bwana." Mnaona? Hiyo ni kweli. Yeye alijua alichokuwa akizungumzia.

217 Lakini kasema, "Kama yeye ni mjinga, acha tu awe mjinga. Hivyo tu. Ha—hatalisikiliza, vema, acha tu aendelee, yeye anaelekea moja kwa moja shimoni. Mnaona, lakini endelea tu." Lakini hapo, hizo roho mbili.

218 Hoja. Kama vile walivyo na wanawake kwenye jeshi la polisi, huko nje mitaani. Hiyo ni fedheha kwa bendera ya Marekani, kuwaweka hao akina mama huko mtaani. Huku makumi ya maelfu ya wanaume hawana kazi! Mbona, ni taifa la mwanamke, ni mahali pa mwanamke, mwanamke atatawala. Ni kuabudiwa kwa mwanamke. Ni ile roho ya mafundisho ya sharti ya Kikatoliki, kumwabudu mwanamke kama mungu. Hii hapa hiyo ninii tu...Yote yako tayari, hivi hamwoni huo mpangilio?

219 Hakuna kitu ambacho Mungu angalimpa mwanamume cha kupendeza kuliko mke, mke halisi. Lakini wakati anapopata kitu kingine zaidi ya hicho, yeye—yeye yuko nje. Hiyo ni kweli kabisa. Mungu kamwe hawakusudii wanawake kufanya kazi katika yoyote ya sehemu hizi na kufanya mambo kama hayo. Wanawake hawa, nyinyi ni...inawapasa kuzaa watoto na kuwalea watoto wao. Wote ni wahubiri wadogo, kila mmoja wao,

bali wana uchungaji wao wenyewe nyumbani pamoja na watoto wao, wakiwalea watoto wao. Vema.

220 Sasa, roho mbili, karibu zinafanana. Ni kama tu Hawa, karibu kuninii . . . Mbona, Shetani, alisema, "Mungu amesema . . . "

"Uh-hum."

"Mungu amesema . . . "

"Uh-hum, hiyo ni kweli."

"Mungu amesema . . . "

"Uh-huh."

221 "Mungu amesema, lakini, loo, hakika Yeye hangetuhukumu kama tumebatizwa katika jina la 'Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.' Huo si ungekuwa ni sawa vile vile?" Ewe mnafiki mtelezi! Naam, bwana. Mungu kamwe hakusema *hivyo*!

222 Hakuna kitu kama hicho, kwa vyovyote vile. Kimekufa! Hakuna kitu kama hicho! Niambieni ambapo jina la "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu" lilipo. Hamna jina kama hilo, basi limekufa! Lilitoka wapi? Katika *Sardi*, kanisa "lililokufa." Hakuna kitu kama hicho! "Unalo jina kwamba u 'hai,' nawe wasema wewe ni 'kanisa la Kikristo,' bali umekufa!" Hiyo ni kweli, hakuna kitu kama jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu."

"Loo, vema, hilo si litakuwa ni zuri vile vile?"

223 Na halitakuwa, Paulo alisema halifai; kasema, "Je, mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?"

"Hatujui kama kunaye . . . "

224 Kasema, "Basi mlibatizwaje?" Kasema, "Njoni mkabatizwe tena katika Jina la Yesu Kristo!" Kasema, "Kama malaika akija kutoka Mbinguni, akifundisha lingine lolote, na alaaniwe!"

225 Hiyo ni Kweli! Mimi ninawajibika tu kwa kulisema Hilo. Mnaelewa, zaidi sana sio ninyi, ni kanda hizi ndizo ninakemea, mnaona, maana ninajua mahali zinakoenda (kila mahali), na kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo. Vema. Sio . . .

226 Hawa alidanganyika, yeye aliona sehemu ya Neno. Moabu walidanganyika. Mwanamwali aliyelala alidanganyika. Kanisa limedanganyika. Madhehebu yamedanganyika. Mnaona?

227 Dumuni na Neno! Hiyo ndiyo njia pekee. Dumuni moja kwa moja nalo, msiliondokee. Dumuni moja kwa moja Nalo, endeleeni moja kwa moja na yale Mungu aliyosema mfanye. Haijalishi mtu mwingine yeyote anasema nini, kaeni kwenye maeneo ya Mungu.

228 Sasa, mwanamwali aliyelala, alipoteza mahali pake, tunajua hilo. Anakuja hukumuni. Na kama amewahi kuisikia Kweli,

amehukumiwa. Hiyo ni kweli. Kamwe hutampata Yesu mahali popote ila pale ulipomwachia.

229 Yuda angeweza kuja . . . Kumbukeni! "'Wale wanawali waliolala' mnasema, 'wangeweza kuvuviwa na ibilisi'?" Kabisa! "Huku wangali wakiishi safi?" Naam, bwana. Yuda aliishi safi; akaokoka, akatakaswa, akahubiri uponyaji wa Kiungu, akawatoa pepo. Mbona, yeye alikuwa ni mnyofu kabisa, karibu vile vile tu hao wengine walivyokuwa. Lakini ilipofikia kwenye Pentekoste, hapo ndipo alipoonyesha kwamba yeye ni nini. Hakumpokea Roho Mtakatifu, naye akageuka ghafla na kumkana Bwana Yesu. Hivyo ndivyo makanisa yalivyofanya hasa. Ilipofikia kwenye Baraka za Kipentekoste, waliziacha. Loo, hivi hamlioni, enyi darasa?

230 Loo, sasa usiku wa leo lile Jiwe kuu la Kufunika. Lakini hebu kidogo, nafikiri tuna wakati mwingine zaidi kidogo hapa, ningetaka kuliendea jambo lingine. Ninataka ku- . . . ninyi a—alama ya mnyama. Alama ya mnyama, hebu tuchukue Ufunuo 13, kwa dakika moja. Ufunuo 13:15, na tusome tu yale ninii . . . yale atakayofanya. Ufunuo 13:15:

> *Akapewa kutia pumzi ile sanamu ya mnyama* . . . (sasa, hiyo ni, "kwa makanisa ya Kiprotestanti, makanisa ya Kiprotestanti.")

231 Alikuwa na mamlaka, kwa sababu walifanya sanamu: makanisa ya Kiprotestanti. Kupitia kwa—kwa Baraza la Makanisa, wanafanya mahali ambapo ushirika wote wa Kiprotestanti itabidi uungane. Ni wangapi wanajua ama wamesoma juu ya lile jengo kuu la Muungano walilo nalo kwa ajili ya makanisa ya ulimwenguni? Hakika. Mnaona? Huko katika . . . huko juu sasa, kama vile tu mataifa ya U.N. Nayo yote yako huko, kila moja yao, hata Assemblies of God. Yako huko! Wako huko, mnaona. Ni unyang'au. "Kama nguruwe aendavyo kwenye mgaagao wake, na mbwa kwenye matapiko yake," wanarudi moja kwa moja kwenye kitu kile kile (Kabisa!), karibu wakikana msimamo wao wa kiinjilisti. Haya basi, wanataka kuwa wakubwa, wanataka kutenda kama walimwengu wengine, kama vile Israeli ilivyofanya wakati walipowaona wale wafalme na kusema, "tufanyie mfalme." Mnaona?

> *Naye* . . . akafanya *sanamu ya mnyama,* hata *ile sanamu ya mnyama inene, na kuwafanya* . . . *hao wote wasioisujudu sanamu ya mnyama* . . .

232 *Sanamu* ya mnyama, "dhehebu la Kiprotestanti," sio Katoliki. Hii ni Marekani anayonena habari zake hapa, mnaona, maana mlango huu wa 13 unahusu Marekani, yule mnyama aliyejitokeza kutoka . . . Mnaona, wanyama wengine wote walitoka *majini,* ambayo yanamaanisha "halaiki na umati wa watu." Bali mnyama huyu hapa, yeye alijitokeza kama mwana-kondoo, kutoka ardhini ambapo hapakuwapo

na watu; alikuwa na pembe mbili, kisha akanena kama joka. Nao wakafanya sanamu ya mnyama ambaye alikuwa huko Ulaya, kisha wakamfanyia huyu hapa sanamu yake. Muu-. . .kuyaunganisha makanisa na kufanya ushirika huu wa Kiprotestanti, ndipo basi wakayalazimisha makanisa mengine yote, hata wasingeweza kununua wala kuuza au kitu kingine chochote pasipo kuwa na sanamu hii ya mnyama.

233 Sasa angalieni kinachotukia hapa:

> *Naye* akawafanya *wote,. . .wakubwa, matajiri. . . maskini, huru,. . .watumwa, watiwe chapa katika mkono wao wa kuume, au katika* vipaji vya uso *wao*;
>
> *Tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa. . .ana chapa ile, yaani, jina la mnyama yule, ama hesabu ya jina lake.*
>
> *Hapa ndipo penye hekima. Yeye aliye* na *akili, na aihesabu* hesabu *za mnyama huyo, maana ni. . .hesabu ya kibinadamu. na hesabu yake ni Mia sita, sitini na sita*. (Ambapo tunajua huyo ni nani; ni ukasisi wa Rumi: papa.)

234 Nimekuwa moja kwa moja kule na kuliona mwenyewe, ningejua, mpaka kwenye mahali pake (kiti chake cha enzi, tuseme) kama vile walivyomwinua Boniface wa kwanza, wa III, huko mwanzoni mwa wakati wa Kikatoliki *hapa*. Na pale juu ni *Vicarivs Filii Dei*, ambalo linamaanisha “halifa wa Mwana wa Mungu.” *Dei, Dei*, “Uungu,” mnaona. Mnaona, “Halifa wa Mwana wa Mungu.” Kwa maneno mengine, “Kama tu Mwana wa Mungu akiketi hapa duniani,” mnaona, “mamlaka yote ya kuibadilisha Biblia,” kubadilisha chochote atakacho. Kwa hiyo, “Semeni ‘Salamu Maria’!” Papa anasema nini? “Tutakuwa na ‘Salamu Maria’!” Hilo latosha. Uh-huh, uh-hum. “Vema, tutafanya *hivi-na-hivi*.” Asemayo papa, ndivyo hivyo, hakuna lingine. “Halifa badala ya Mwana wa Mungu.”

235 Hivi majuzi tu walileta fundisho lile la sharti kwamba “Mariamu hakuzikwa,” (Nao wamelitia alama kaburi lake na kadhalika mahali alipozikwa.) kasema, “La, yeye aliamka tena na kufufuka.” Papa alisema, “Ndilo hilo!” na ni hivyo tu. “Haliwezi kukosea, mnaona,” papa alisema hivyo. Mnaona, “Halifa wa Mwana wa Mungu.”

236 Naye akasema, “Sasa, mtu yeyote anayetaka kujua huyo mnyama ni nani, mahali mamlaka haya yanapotoka,” Hilo lilisema, “hesabu hiyo hesabu hapo na aliye na hekima. . .” Hapo, hiyo ni moja ya karama za Roho Mtakatifu, ni hekima. Mnaona? Yeye aliye na hekima na aihesabu hesabu ya mtu huyo, maana ni. . .aihesabu hesabu ya huyo mnyama, maana ni hesabu ya kibinadamu, na hesabu yake ni mia sita sitini na sita. Sasa, chukua ninii. . .na kuliendeleza jina hilo, V-i-c-o, na—na kulingana tu na hayo maneno, kisha uchore mstari hapa na. . .

ama uongeze hizo tarakimu za Kirumi, nawe utaona hapa una mia sita na sitini na sita. Hiyo ni kweli.

237 "Na sasa hebu tufanye sanamu ya mnyama yule." Na huko katika nchi hii wakafanya sanamu ya mnyama: muungano wa madhehebu pamoja, Wanikolai wakikutanika pamoja na kujifanyia dhehebu. Ndipo hatimaye wataunganisha udugu huu, sio kuingia kama Ukatoliki, bali wataungana kama udugu kujaribu kuuangamiza Ukomunisti.

238 Nayo Biblia ilisema ya kwamba Mungu aliinua Ukomunisti apate kulipizia kisasi juu ya mataifa kwa ajili ya yale yamewafanyia watoto wa Mungu. Hiyo ni kweli kabisa. Yeye alisema, "Na wao—wao—wao watampa yule mnyama mamlaka yao na kila kitu kwa muda wa saa moja, na kuwalipizia watu kisasi, ninii . . . cha damu waliyokuwa wamemwaga." Basi wakati hilo bomu la atomiki ama chochote kile kitakapoupiga Mji wa Vatikani, basi ukasisi wa Kirumi hautakuwapo tena, Lilisema, "Na ndani yake ilipatikana damu ya kila mfia imani aliyepata kuuawa ulimwenguni." Naye huyo hapo. Na hii hapa ile sanamu yake, muungano wa makanisa.

239 Haitachukua muda mrefu hata itakapotubidi kuifunga hiyo milango huko ng'ambo, hiyo ni kweli, ama labda tuichukue alama ya kimadhehebu. Nasi tutaifunga milango, hiyo ni kweli, tutaninii . . . tunajua vema kuliko hivyo.

240 Sasa, sasa, ninataka, kwa ajili tu ya sehemu ya kufinyilia, kabla hatujaondoka katika dakika chache zijazo. Sasa, *muhuri* wa Mungu ni "Roho Mtakatifu." Nyote mnajua hilo, sivyo? Vema, sote tunajua hilo, ya kwamba muhuri wa Mungu ni Roho Mtakatifu. Sasa hilo linapatikana . . . Hebu chukua Ufunuo 9—9:1 hadi 4, utaona kwamba wote walikuwa na muhuri kwenye paji la uso wao. Wakorintho wa Kwanza 1:22, Paulo alisema, "Ambapo ametutia muhuri kwa Roho Wake Mtakatifu hata siku . . . " Waefeso 4:30, inasema, "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu," huyo ni yule Malaika aliyekuja akiwatia muhuri kwenye paji la uso wao. Sasa, hilo halimaanishi nyinyi . . . Yeye anachukua na kuweka alama pale juu; paji lako la uso ni ufunuo wako, unaona, na mkono wako ni yale unayofanya kulihusu. Unaona, ni alama ya kiroho. Mnaona? Yeye hachukui stampu kubwa kukutia muhuri namna *hiyo*. Loo, la.

241 Kama hapa miaka michache iliyopita wao walisema, wakati hii N.R.A. ilipotokea, ilikuwa *hivi, vile* ama . . . Msiyatazamie hayo, yapo tayari. Biblia ilisema ilianzia moja kwa moja huko nyuma, karibu imekwisha sasa. Mnaona? Hiyo ni kweli.

242 Lakini Yeye alitia alama waliotiwa Muhuri. Mnaona? Sasa, ule muhuri wa kwanza ulikuwa—ulikuwa vipi, ulionekanaje? Wao walijazwa na Roho Mtakatifu, hiyo ni kweli, nazo kazi zao zilikuwa ni kazi za Kristo. Waliweka mikono juu ya wagonjwa nao wakapata afya, walifanya kila namna ya ishara na miujiza

na maajabu. Na kwenye paji la uso wao, walitiwa muhuri kwa ufunuo ya kwamba Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu, nao walikuwa—walikuwa wakifanya kazi pamoja Naye (U—Uungu wa Kristo), hiyo hapo ile alama.

243 Mnasema, “Vema, sasa, Yeye ni mtu wa tatu, ama wa pi-. . . ” Hujatiwa muhuri bado, kwa hiyo li—liache tu. Unaona, tayari uko nje, umetolewa kwenye karatasi pale, kwa hiyo hakuna kitu kama hicho katika Biblia. “Tunambariki . . . Tunaamini katika utatu mtakatifu.” Uko mbali . . . Hata huko kwenye karatasi sasa, unaona, maana hakuna kitu kama *utatu* kilichopata kutajwa katika Biblia. Litafute neno *utatu* katika Biblia kisha uje.

244 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . ? . . . katika Mwana, unaoitwa uwana; sasa Yeye yuko ndani yako, ubatizo wa Roho Mtakatifu; Mungu yule yule. Roho Mtakatifu alikuwa ndiye Baba wa Yesu Kristo. “Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena,” kasema Yesu, “Nimetoka kwa Mungu, tena narudi kwa Mungu (Roho Mtakatifu tena). Nami nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata mwisho (kwenye ukamilifu wa dahari). Kote kote chini, nitakuwa moja kwa moja kupitia kwenu namna hiyo ambapo . . . Na kazi zile zile nifanyazo ninyi nanyi mtazifanya. Kazi ambazo nimekuwa nikifanya zitafuata moja kwa moja, hiyo ndiyo itakayokuwa ishara ya mwaminio kote kote. Enendeni mkahubiri, mkiwabatiza katika Jina la Bwana Yesu, nao watajazwa na Roho Wangu; nao wakijazwa, ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, hata ukamilifu wa dahari. Niko pamoja nanyi daima, hata mwisho wa ulimwengu.” Yeye alipokelewa juu Utukufuni. Jambo ndilo hilo, nasi tunamtarajia aje siku moja. Sasa, huo ndio muhuri wa Mungu, tunajua hilo.

245 Basi kumbukeni, kuna mia moja na arobaini na nne elfu tu ya Wayahudi waliotiwa muhuri, ambao walikuwa ndio masalia ya Wayahudi waliosalia. Lakini katika jambo hili, katika Bibi-arusi wa Mataifa, katika Bibi-arusi wa Mataifa, kulikuwako na makumi elfu mara maelfu, ya wale ambao wametiwa muhuri mle ndani, maana hao ni wale wafia imani na kadhalika waliopitia katika zile nyakati kule; watafufuka katika siku hiyo ya hukumu.

246 Unafikiri itakuwaje wakati hiyo miguu ya shaba ya hukumu itakaposimama pale kwenye siku hiyo na hao wafia imani wasimame hapo mbele ya hao Warumi (labda Wanikolai huko nyuma ambao waliwafanya wachomwe moto kwenye nguzo na kutupwa kwenye matundu ya simba na mambo kama hayo), nao wasimame pale kama wakili wao kwenye ki- . . . kwenye kizimba cha wazee wa mahakama hapa? Huku Hakimu ameketi pale kwenye kiti, “Hivi mliwahubiria Injili?”

“Nilitia muhuri maisha yangu huko katika kinywa cha simba kwa ajili yao.”

247 Loo, ndugu! Nena kuhusu "ondokeni Kwangu," jehanamu itakuwa ni nzuri sana kwao! Hiyo ni kweli kabisa.

248 "Shikilieni sana. Ninawajua hao wajiitao . . . (Wanikolai), na kujiita 'waliojazwa na Roho' wala sio." Hapo, mnaona, haya basi. Loo! Ni saa ya jinsi gani inayokuja, ni wakati wa kuogofya jinsi gani. Mungu atalipiza kisasi! "Nitalipiza kisasi," asema Bwana, "Nitapatiliza!" Na kila tendo ovu litapata ninii . . . Kila kitu ulichowahi kufanya au kuwazia maishani mwako kitashikiliwa dhidi yako kule, kwenye kile kitu kikuu cha sumaku pamoja na kila wazo ovu lililopitia niani mwako. Tubuni, enyi watoto!

249 Kuna njia moja ya kuepukana nalo, ingia ndani ya Kristo, na wakati unapoingia kwenye ubavu Wake wa kupendeza uliojeruhiwa mara tano kule, yale majeraha matano ya thamani mwilini Mwake, ukiuona huo ukitokwa na damu huko nawe ujifiche humo, useme, "Mwamba wa Miaka, mimi sifai kitu. Nifiche, Mwamba wa Miaka." Mhisi Roho Mtakatifu wa thamani, kufa tu na uingie kwenye mwili wa Kristo; inuka, upate kuamkia mambo mapya, ni ulimwengu mpya uliokuzunguka. Dhambi ambazo wakati mmoja ulizipenda ziko nyuma yako. Loo, hakuna chochote cha usoni, hakuna cha wakati uliopo, mauti, hakuna kitu kingine kitakachokutenganisha na Hilo. Umetiwa muhuri hata siku ya ukombozi wako, kwa Roho Mtakatifu. Unao ufunuo wa Yeye ni Nani. Unajua moyoni mwako umepita kutoka mautini ukaingia Uzimani.

250 Angalia kazi zako pamoja na mikono yako basi, unaona. Huibi tena, hufanyi maovu tena. Mikono yako ni safi kutokana na damu yote. Nawe umesimama, unahubiri Injili, unasema yaliyo kweli, na kuishi kilicho sahihi, na kufanya yaliyo haki, naye Roho Mtakatifu yu pamoja nawe akionyesha ishara na maajabu kila siku; Mungu akikujalia kujua jinsi, "Wewe ni mtoto wangu mbarikiwa nami ni—niko pamoja nawe. Haijalishi uko wapi, niko pamoja nawe. Nitaambatana nawe katika saa zenye giza na kila mahali." Loo, ni—ni Nanga ya jinsi gani!

> Nimeitia nanga nafsi yangu katika mahali pa Raha,
> Nisiabiri bahari zenye tufani tena;
> Loo, mawimbi huenda yakavuma kwenye vilindi vikali, vyenye tufani,
> Lakini katika Yesu mimi ni salama milele.

251 Hata mauti yakija yakiimba huku moja ya siku hizi, na kuruka kama nyuki karibu na kichwa chako namna hiyo, unaweza kusema, "Ee mauti, uko wapi mwiba wako?"

252 Kama vile maskini Sara alivyoandika hivi majuzi asubuhi, maskini msichana wangu mdogo anayeketi pale nyuma. Alikuwa akiandika muhtasari, yeye pamoja na msichana mdogo wa Ndugu Collins, ninaamini, juu ya yale niliyokuwa nikitaka kusema. Kwa hiyo nilikuwa nikisoma hiyo karatasi, mimi na

mama yake, naye alisema, "Kitabu cha mapinduzi." Amina. Akasema... Nanyi mnajua ile hadithi ndogo niliyosimulia mwishoni juu ya *mauti,* mwajua. Mmeisikia, *kutokuwa na mwiba*. Ulikuwa hapa wakati hiyo iliposimuliwa? Mnaona, mauti wakati mmoja ilikuwa na mwiba ndani yake, lakini wakati...

253 Shetani hakuwa na hakika sana kama Mtu huyo alikuwa ndiye Mwana wa Mungu au siye. Ungemwona amesimama pale wakati... Shetani alimjia akasema, "Vema, kama unaweza kufanya miujiza, kama Wewe ni jamaa anayefanya miujiza, Wewe ni yule Mwana wa Mungu. Nitakwambia, imeandikwa katika Biblia, unaona, ya kwamba... Basi—basi kama—kama Wewe ndiwe, hebu nione ukifanya mwujiza. Sasa, Wewe una njaa, hujala kwa muda wa siku arobaini, kwa nini usilichukue jiwe hilo ukalifanye mkate kisha uketi chini ule? Hebu nikuone ukifanya hilo nami nitaamini Wewe ni Mwana wa Mungu."

254 Kasema, "Mtu hataishi kwa mkate pekee, bali kwa kila Neno." Loo, jamani! Yeye alijua hakukutana na Musa hapo, sivyo? Musa alizitupa chini amri na kuzivunja; bali alijua alikuwa amegusa zaidi ya Musa.

255 Ndipo akampandisha juu, naye akasema, "Unaziona hizi falme zote za dunia? Ile pale Marekani, ile pale Uingereza, zile pale hizo zote zinazoibuka hapa katika miaka ijayo." Kasema, "Kila moja ya hizo zitakuwa ni zangu, Wewe unajua hilo." (Huyo ndiye anayezitawala.) Kasema, "Ni zangu nami nitafanya nazo, ninazipeleka vitani, ninafanya lolote ninalotaka kufanya nazo. Ni zangu." Kasema, "Nitakupa Wewe ikiwa tu utaniabudu mimi."

256 Kasema, "Rudi nyuma Yangu, Shetani." Yeye alijua atazirithi kwa vyovyote vile, mwishowe, kwa hiyo Yeye akasema, "Rudi nyuma Yangu, Shetani."

257 Hatimaye wakati walipompata kule chini siku moja, na wa—wakachukua kitambaa na kuufunga uso Wake namna *hii*, ninawazia ni maskini skafu chafu, na kupata... wakaivuta kichwani Mwake. Naye ameketi hapo, akitokwa na damu na kuumia. Asubuhi, upepo baridi ukivuma. Walikuwa tayari wamempiga mijeledi, na damu ikitiririka juu ya mabega Yake, wakamzungushia kitu namna *hiyo*; na hiyo damu ikinata mgongoni Mwake, ameketi pale, na taji ya miiba imevutwa usoni Mwake namna hiyo. Nayo damu, na mate kutoka kwa wale askari, kote usoni Mwake, ameketi pale. Hiyo si ilionekana kuwa tamasha ya kusikitisha sana? (Ee Mungu!)

258 Unasema, "Vema, kama ningalikuwa pale, ningalifanya jambo fulani kulihusu." Vema, mbona usifanye jambo fulani kulihusu sasa? Maana kama wewe... Ungalifanya jambo lile lile unalofanya sasa.

259 Huyo hapo, ameketi pale, akidhihakiwa na kutemewa mate. Hao hapo wanafunzi wamesimama kule nyuma, wakisema, "Loo, jamani, ingewezekana? Mtu huyo, Ambaye angeweza kumwita mtu aliyekufa kutoka kaburini, na kumwangalia pale." Bali walishindwa kuyajua Maandiko. Hivyo ndivyo ilivyo, mnaona.

260 Na kwa hiyo, damu na mate usoni Mwake. Wakafunga kitambaa machoni Mwake, na kusema, "Mwajua, wananiambia 'Yeye alikuwa na utambuzi wa kiroho, mwajua. Yeye ni nabii, angeweza kuwaambia watu. Alimwambia yule mwanamke kisimani dhambi zake. Pia alimwambia Simoni ya kwamba jina la baba yake lilikuwa ni Yona, na yote kuhusu hilo.' Hebu tuone kama Yeye anaweza, yale anayoweza kufanya sasa."

261 Wao walisema, "Tutampa jaribio dogo." Huyo alikuwa ni ibilisi akitenda kazi katika watu hao. Wakaweka kitambaa juu ya macho Yake namna *hiyo,* wakachukua fimbo na kumpiga nayo kichwani, wakasema, "Kama Wewe ni nabii, twambie ni nani aliyekupiga." Hata hakufungua kinywa Chake, aliketi tu pale.

262 Shetani alisema, "Mnajua huyo hawezi kuwa . . . huyo—huyo hawezi kuwa ni Mungu."

263 Hilo ni jambo lile lile maskini hilo dhehebu la kale lisemalo leo, "Kundi hilo la watakatifu wanaojibingirisha, huyo hawezi akawa ni Mungu." Bali hawajui. Hawajui. "Huyo hawezi akawa ni Mungu akifanya mambo hayo, hiyo ni telepathia ya akili. Hao ni—hao ni wapiga ramli." Kamwe hawakulipata, hivyo tu.

264 Kwa hiyo wakaanza—wakaanza kupanda kilimani, wakamvika vazi hilo. Nguo pekee alizowahi kuwa nazo, nadhani, wakati alipokuwa mwanadamu, Mariamu na Martha walimtengenezea maskini joho moja; joho zima, lisilo na mshono. Wakaliweka mgongoni Mwake. Basi kulikuwako na matone madogo kotini Mwake wakati akipanda kile kilima; akikokota, akiugongesha-gongesha msalaba huo wa kale. Nao maskini mwili wake mnyonge, akipiga hatua; nao wakimpiga mijeledi, na kadhalika, wakimfanya aendelee hivyo. Maskini msalaba huo wa kale, "bump-bump," na migongo yake ikikwaruzwa, Naye angeyumbayumba, kisha angeendelea.

265 Ndipo hayo matone madogo yakazidi kuwa makubwa, mpaka baada ya kitambo kidogo yote yakakusanyika katika tone moja kubwa. Shetani wa kale akaja, mwajua, katika umbo la "nyuki," hayo *mauti*, mwajua, na kusema, "Aa, aa, aa! Hilo? Mungu asingefanya hivyo." Kasema, "Yeye ni mwanadamu tu, anajifanya." Angali anawazia hilo. "Anajifanya tu, kwa hiyo nitamwuma tu. Kama Yeye alikuwa Mungu asingeweza kufa. Kwa hiyo nita—nitamwuma nione kuhusu hilo, namna hiyo. Nita—nitamjaribu."

266 Kwa hiyo alipompeleka msalabani, aliuchomeka mwiba huo ndani Yake; lakini alipofanya hivyo, akapoteza mwiba wake. Huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu, alimwuma Mungu wakati huo!

267 Na hiyo ndiyo sababu yeye alisema, "Ee mauti . . . " wakati Paulo . . . Mna—mnajua, nyuki, akiisha kuchoma ndani kabisa, hawezi kuchoma tena. Nyuki amekwisha basi. Anaweza kulia na kufanya makelele, bali ha—ha—hawezi kuchoma, maana hana mwiba. Kwa hiyo mauti hayana mwiba wowote tena. Paulo, wakati walipokuwa wakijenga mahali pa kukikatia kichwa chake, mauti yalikuwa yakimcho- . . . yakilialia kumzunguka, yeye alisema, "Ee mauti, u wapi mwiba wako?"

268 Kaburi likasema, "Nitakupata, Paulo. Nitakuvingirisha matopeni." (Nilienda kule mahali walipokikata kichwa chake na kukitupa kwenye mfereji wa maji machafu pale.) Kaburi likasema, "Ni—ni—nitauharibu mwili wako, nitakuozesha kabisa."

269 Ndipo akasema, "Loo—loo, Ee kaburi, u wapi ushindi wako?" Mnaona? "Lakini ashukuriwe Mungu Yule atupaye ushindi kwa Bwana Yesu Kristo!" Mauti yalipoteza mwiba wake kwake. Kasema, "Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo wangu nimeumaliza, Imani nimeilinda. Na baada ya hayo nimewekewa taji ya haki ambayo Bwana, Hakimu mwenye haki atanipa siku ile. Wala si mimi tu, bali na watu wote pia wanaopenda kuonekana Kwake." Amina! "Kikateni sasa mkitaka." Huh! Loo, jambo ndilo—ndilo hilo. Hivyo ndivyo, ndugu. Hiyo—hiyo ndiyo Roho halisi ya Kikristo.

270 Sasa—sasa, kama ukipokea nafasi, unaipataje alama ya mnyama? Ningetaka kusema hili kwa sababu tu nilifikiri ningefunga katika kusema hili. Unaipataje alama ya mnyama? Mngetaka kujua? Matokeo ni yapi? Alama ya mnyama ni nini?

271 Tunajua muhuri wa Mungu ni nini. Muhuri wa Mungu ni nini? Vema, hebu tufungue Waefeso 4:30, na ndipo—ndipo mlipate, halafu mjisomee wenyewe pale. Ama—ama au wengine wenu mnaweza kufungua Ufunuo—Ufunuo 9:1 hadi 4. Na wengine, Wakorintho wa Pili 1:22. Kuna mahali pengi. Niliyaandika machache pale. Lakini hebu tufungue Waefeso 4:30, ndipo mnaweza kuona muhuri wa Mungu ni nini; na haya mengine, ama popote pale. Chukua tu neno *muhuri* katika kamusi yako, na ulifuatilie kila mahali utakapo. Vema, Waefeso 4:30, sikilizeni hili:

> *Wala msimhuzunishe roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri* mpaka *siku ya ukombozi* wenu.

272 Muhuri wa Mungu ni nini? Roho Mtakatifu. Hakika. Vema, sasa, "Yeye asiye na Roho wa Mungu si Wangu." Endapo una Roho Mtakatifu, wewe ni sehemu ya Mungu kwa sababu wewe

ni Wake. Yeye—Yeye amekutia muhuri Naye yuko ndani yako, akitenda kazi ndani yako, nazo ishara afanyazo Yeye wewe nawe unazifanya. Sasa, kila mtu anaelewa hilo, enyi darasa? Inahitaji Roho Mtakatifu upate kuwa wa Mungu; Roho Mtakatifu. Na endapo wewe ni wa Roho Mtakatifu, unafanya kazi ambazo Yesu alifanya. Mnaona? Upendo wako . . .

273 Wakati hao wanapokutemea mate usoni Mwako na kukupiga jinsi hiyo, hapakuwapo na shina la uchungu. Yeye aliinama akawaangalia, akasema, "Baba, wasamehe kwa kuwa hawajui watendayo." Mnaona, hawakujua.

274 Ungeweza kuwazia hilo? Watoto Wake Mwenyewe wakiililia Damu Yake! Muumba wa mbingu na nchi akining'inia kwenye msalaba ambao aliufanya Mwenyewe, akaukuza kutoka ardhini. Ndipo watoto Wake Mwenyewe! (Wazia juu ya watoto wako, ninyi akina baba, watoto wako mwenyewe.) Wakimlilia, "Hatumtaki! Tupe Baraba, yule mwizi kule."

275 Loo, nilikuwa huyo Baraba, mimi ndiye niliyestahili kufa Naye akapachukua mahali pangu. Jinsi maskini Baraba hapana shaka alijisikia asubuhi hiyo wakati vishindo vya akida vikishuka kupitia pale, na kuufungua mlango. Naye maskini Baraba akisema, "Loo, jamani! Muda kidogo tu nami nitaangamia. Mimi ni mwuaji, mimi—mimi ni mwizi. Wataniua leo, najua wataniua. Ni siku ya pasaka, kwa hiyo mimi—mimi kweli . . . Ninajua nitakufa leo hii." Wasiwasi, usiku kucha, akitembea huku na huku kama mwenye dhambi mwingine yeyote. Muda si muda mwajua, huyu hapa mlinzi anakuja. Akasema, "Loo, loo, huyu hapa. Sina budi kwenda, sina budi kwenda." Ndipo ufunguo ukaingia na kualika.

Mlinzi akasimama wima, "Toka nje, Baraba!"

"Uh-huh, naam. Naam, ninajua ninaenda, ninaenda."

"Hapana, endelea ukafanye utakacho."

"Ati nini?"

"Nenda ukafanye utakacho. Toka, uko huru."

276 "Niko huru? Mbona, mlinipa hukumu ya kifo." Hiyo ni kweli, Mungu huwapa wenye dhambi wote hukumu ya kifo. "Mlinihukumia kifo, nitakuwaje huru?"

277 "Njoo hapa, Baraba. Angalia, akipanda pale mlimani, sikiliza msalaba huo ukigongagonga sakafuni. Sikiliza misumari hiyo wakati ikipigiliwa mikononi Mwake. Mwangalie akilia pale, machozi ya chumvi na damu yakichanganyikana kupitia usoni Mwake. Yeye alipachukua mahali pako, Baraba, alikufa kwa ajili yako."

"Unamaanisha Yeye alikufa nipate kuwa huru?"

"Naam."

278 "Vema, sawa, nitaanza kuua tena basi." Loo, jinsi usivyo na shukrani; unastahili kufa.

> Ni—niwonapo ule Msalaba wa ajabu,
> Alipofia Mfalme wa Utukufu,
> Sifa zangu zote ni hasara ya bure.

Loo, jamani! Si ajabu mshairi alisema:

> Alipoishi, alinipenda; alipokufa, aliniokoa;
> Alipozikwa, aliziondolea mbali dhambi zangu;
> Alipofufuka, alinihesabia haki bure milele:
> Siku moja yuaja, loo, siku ya ajabu!

279 Ningewezaje kamwe kumkataa wakati ninapoona yale aliyonifanyia? Ningewezaje? Ningekuwa tayari kupoteza kila rafiki niliye naye duniani. Jinsi, wakati mimi . . . Ningekuwa tayari kufukuzwa na madhehebu na kurushwa-rushwa, wakati kila kitu kingine. Ninapoangalia huko, wakati nilipohukumiwa kifo, Naye akapachukua mahali pangu! Hakika, Bwana. Kila kitu, ninahesabu kila kitu kingine kuwa hasara ya bure. Loo, nijalie niukumbatie Msalaba, Ee Bwana.

> Katikati ya miamba inayopasuka na anga zinazoingia giza
> Mwokozi wangu alikiinamisha kichwa Chake akafa,
> Pazia lililofunguka lilifunua njia
> Ya kwenda kwenye raha za Mbingu na siku isiyo na mwisho.

280 Loo, nijalie—nijalie nikae karibu na Wewe, Yesu. Usinifukuze kutoka ubavuni Mwako mpendwa, nikiona majeraha Yako matano yakitokwa na damu. Ee Mfalme wa Mbingu, jinsi alivyokufa, alinifia mimi! Akafa ili niweze . . .

281 Aliyehukumiwa . . . katika minyororo ya dhambi, katika jela ya kuzimu, amehukumiwa, mwenye hatia, akienda apate kuangamizwa milele, ndipo Mtu fulani akapachukua mahali pangu. Ndipo wao . . . Nikilima hapa nilipokuwa m- . . . ; ilikuwa yapata umri wa miaka kumi na minane, ishirini, siku moja Roho Mtakatifu . . . Nikasema, "Vema, mimi ni nani? Nilitoka wapi? Ninaenda wapi?"

282 Yeye alisema, "Alipachukua mahali pako, ulikuwa ukienda *kule*. Yeye akapachukua mahali pako, Yule pale."

283 Nikasema, "Ee Mwana-kondoo wa Mungu! Ee Mwana-kondoo wa Mungu, naja! Naja! Sina cha mkononi, sina kitu cha kukutolea, Bwana, nashikilia msalabani Pako tu; hayo tu ndiyo niliyo nayo." Naye akaniingiza ndani. Akanivisha nguo kama yule baba aliyekuwa na yule mwana mpotevu, akanivisha vazi jipya, vazi lisilo langu, vazi Lake la haki Yake alinivisha; na pete ya arusi kwenye kidole changu, kwamba nitakuwa pamoja na Bibi-arusi siku ile. Sasa ndama mnono amechinjwa, nasi

tunashangilia kwa sababu wakati mmoja nilikuwa nimekufa na sasa ni hai, wakati mmoja nilikuwa nimepotea na sasa nimepatikana.

Neema ya ajabu! jinsi inavyosikika tamu,
Iliyomwokoa mwovu kama mimi! (Mwovu kuliko Baraba.)
Wakati mmoja nilikuwa nimepotea, lakini sasa nimepatikana,
Nilikuwa kipofu, bali sasa ninaona.

Neema ndiyo iliyoufundisha moyo wangu kuhofu,
Neema ndiyo iliyoondoa woga wangu;
Jinsi hiyo neema ilivyoonekana ni ya thamani
Ile saa niliyotangulia kuamini!

Tukishakuwa huko miaka elfu kumi,
Tukiangaza sana kama jua; (Si nyota tena, Jua.)
Hatutakuwa na siku pungufu kuimba sifa Zake
Kuliko tulipoanza mara ya kwanza. (Tuko katika Umilele basi.)

284 Loo, jinsi ninavyompenda Yesu, kwani alinipenda kwanza. Loo, ni ajabu jinsi gani!

Fungueni pamoja nami sasa katika Kutoka, sivyo, mlango wa 21.

285 Ushauri wa "Roho" Wake, sasa tutazungumza juu ya jinsi ya kupokea . . . Niliwaonyesha, na kuwaambia matokeo, "Yule *pale*."

286 Sasa, unaipokeaje alama ya "mnyama"? Nami nitakuonyesha kilicho maangamizi yako *hapo*. Sasa, alama ya mnyama, Kutoka mlango wa 21. Tukiitoa katika Agano la Kale kusudi mpate kuona hapa. Pia katika Agano Jipya ninayo Maandiko mengi yaliyowekwa hapa ambayo sisi sote tunayajua. Sasa hebu tusome:

Basi hukumu utakazoziweka mbele ya watu ni hizi.

Ukimnunua mtumwa wa Kiebrania, (Sasa, kumbukeni sasa, ni Mwebrania, huyo ni mwaminio, mnaona.) . . . *mtumwa wa Kiebrania atakutumikia muda wa miaka sita: mwaka wa saba atatoka kwako huru bure.*

Kwamba aliingia kwako peke yake tu, atatoka hivyo peke yake: kwamba alioa, mkewe atatoka aende pamoja naye.

Kwamba ni bwana wake . . . aliyempa *huyo mke,* . . . *amemzalia wana wa kiume au wa kike; yule mke na*

wanawe watakuwa ni mali ya bwana wake, naye mume atatoka . . . peke yake.

287 Sitaninii . . . Na—na—na—najua muda wangu umekwisha. Samahani, Ndugu Neville, bali i—inanibidi kulishindilia hili, ndugu.

288 Angalieni hapa. Sio kile mama yako alicho, kile baba yako alicho, ni wewe! Si mke wako, unaona; mke wake hakujalisha, watoto wake hawakujalisha. Ni yeye! Haijalishi . . . Huenda mama yako alikuwa ni mtakatifu, huenda baba yako alikuwa ni mtakatifu; vivyo hivyo na baba na mama wa Esau, bali yeye alikuwa ni mtu wa kazi ngumu. Mnaona? Lakini, yeye . . . bali ni mambo ya mtu binafsi pamoja *nawe*.

289 Unasema, "Baba yangu ni mhubiri." Hilo halina uhusiano wowote nawe. "Mama yangu ni mwanamke mtauwa. Loo, yeye yuko Mbinguni." Huenda hiyo ikawa ni kweli, lakini vipi kukuhusu wewe? Wewe ndiwe!

Lakini ikiwa huyo mtumishi . . .

290 Sasa, hapa ndipo yeye . . . Sasa angalia hii alama ya mnyama sasa. Sasa, si—sina wakati wa kurudi nyuma taratibu, maana imebaki dakika ishirini. Lakini nataka kuwaambieni.

291 Sasa, kulikuja wakati ulioitwa kila baada ya mwaka wa saba. Hiyo ilikuwa ni miaka sita. Katika mwaka wa saba (wanafunzi wa Biblia, wahudumu, na kadhalika walioketi hapa, wanajua hili kuwa ni kweli.) uliitwa . . . mwaka wa saba uliitwa mwaka wa yubile; kila kitu kilipumzika. Hakuna mimea iliyopandwa katika mwaka wa saba, shamba lilipumzika, kila kitu. Waliokota tu masazo, mnaona. Kila kitu kilipumzika kwenye mwaka wa saba. Na katika mwaka wa saba palitokea ku—kuhani ambaye alipiga baragumu. Basi kama mtu alikuwa ni mtumwa, sijali deni yake ilikuwaje, yeye alikuwa huru.

292 Sasa, huo ni mfano wa Baragumu ya Injili. Huenda umemtumikia ibilisi miaka hii yote, katika minyororo, pamoja na kunywa pombe, kuvuta sigara, kucheza karata, na dhambi, mambo machafu, haidhuru umefanya nini, bali utakapoisikia Baragumu ya Injili ikilia, ni ishara ya kwamba unaweza kuwa huru. Unaweza kuondoka! "Imani chanzo chake ni, [Kusanyiko linasema, "Kusikia."—Mh.] kusikia, Neno la Mungu." Sasa mmeisikia Injili yote, haikubidi kudumu mfungwa tena.

293 Sasa, kama ukikaa tu na kusema, "Loo, niliisikiliza, bali sikuisikia." Unaona? Vema, basi si kwa ajili yako. Uhu-uh. Ni kwa ajili ya wale wanaoisikia. Vema, endapo unaweza kusikia.

294 Sasa angalieni yale Yeye aliyosema hapa. Sasa kulithibitisha hili, sasa angalieni kwa makini sana na kuyaweka mawazo yenu sasa kwa dakika zingine mbili ama tatu.

> *Lakini mtumishi* (Huyo ndiye mtu aliyekuwa a—awekwe huru.) *akisema waziwazi, Mimi nampenda bwana wangu*, . . .

295 "Loo, ninapenda kwenda kwenye dansi. Siziachi dansi zangu kwa ajili ya mtu yeyote. Siachani na *hili*, *lile*, au *linginelo,* kwa ajili ya mtu yeyote; mke wangu, watoto wangu, mambo ya dunia hii niyapendayo. Sasa, angalia hapa, Ndugu Branham, nitakwambia, unamaanisha itanibidi . . .?" Haikubidi kuacha chochote. Wewe ingia tu, hujikomesha lenyewe. Lakini—lakini unasema, "Vema, nisingefanya hilo. Si lazima nifanye hivyo, mimi ni mfuasi wa kanisa nami ni bora tu kama ulivyo wewe ama mtu mwingine yeyote." Vema, ndugu. Hilo ni sawa, umesikia yaliyo Kweli. "Vema, sasa, sikilizeni hapa, si 'Baba, Mwana, Roho Mtakatifu' . . .?" Vema, ukitaka kushikilia njia hiyo, endelea tu moja kwa moja.

296 Umesikia kile Baragumu ilitolea sauti, na ulisikia sauti iliyotoa. Nayo Biblia ilisema . . . (Ee Mungu!) Angalieni hilo! Hivi hilo si lingenifanyia somo sasa hivi kwa saa moja ijayo? "Kama baragumu ikitoa sauti isiyotambulikana." Kama dhehebu lako likisema "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," hiyo haisikiki kama ni Baragumu. "Kama baragumu ikitoa sauti isiyotambulikana, ni nani atakayejiweka tayari kwa vita?"

> . . . *mtumishi akisema waziwazi, Mimi nampenda bwana wangu,* . . .

297 "Na—nampenda ibilisi a—anayenifanya nifanye mambo haya, hilo ni sawa. Wala sidhani . . . Nafikiri wewe una mawazo finyu sana hapo—hapo juu. Nafikiri wewe ni finyu sana." Vema. "Nayapenda mambo hayo. Na—nafikiri inatupasa kuwa na mambo haya makubwa *hivi*, na kufanya *hivi*, ulimwengu . . . Nasi tunayo madansi, tuna karata kanisani mwetu, na vitu kama hivyo, nasi sote tuna wakati mzuri, nao ni wazuri tu kama yeyote wa kundi hilo mlilo nalo hapo juu;" Sawa, hilo ni sawa. Vema.

> . . . wala *sitaki mimi kutoka* katika uhuru huu wa Roho mnaonena habari zake:

> *Ndipo huyo bwana wake* (ibilisi) *atamleta mbele ya waamuzi*; na *kumleta mlangoni,* . . .

298 Hmm! Ati nini? Mlango ni Nani? [Kusanyiko linasema, "Yesu Kristo."—Mh.] "Ninaweka mbele zenu Mlango." Alama hiyo ya mnyama ilikuja lini? Katika wakati huu ambapo Mlango uliwekwa. Hii ala- . . . kutia alama ya mnyama kwa mara ya mwisho.

> . . . *kumleta mlangoni, au* penye . . . *mwimo;* (hiyo ni Ka—Kalvari, vema) . . . *na bwana wake atalitoboa sikio lake . . . alitoboe sikio lake kwa uma; ndipo atamtumikia sikuzote.*

299 "Una maana gani, Ndugu Branham?" Kama ukiisikia Kweli ya Injili nawe ukatae kutembea ndani Yake, basi Mungu analitia sikio lako alama ambapo hutaisikia Hiyo tena. Umevuka mstari kati ya Uzima na mauti. Ndipo utaendelea na shirika lako, dhehebu lako, siku zako zo-. . .milele. (Tembeeni katika Nuru, enyi watoto, Hiyo ni kweli.) Utamtumikia bwana huyo milele.

300 Hebu hiyo. . .Hutaki kuninii. . .Unaona, Baragumu ililia naye anaweza kuwekwa huru, ni neema ya Mungu. Ni mwaka wa yubile, ukamilisho. Siku ya dhambi imekwisha, ndugu. Ninamwambia kila mmoja wenu anayeitumikia dhambi (kanda, ama kusanyiko linaloonekana), ninyi ni. . .kila mtu anayeitumikia dhambi, siku ya dhambi imekwisha! Yesu alikufa, haikubidi kuitumikia dhambi tena. Haikubidi kufungwa katika kanuni za imani na madhehebu. "Yeye ambaye Mwana amemweka huru ni huru kweli." Ukitaka kuwekwa huru na kuwa huru katika Mwana, jiweke huru na mambo yote ukamtumikie Yeye, hima!

301 Lakini iwapo hutaki, basi shirika lako, bwana wako, yeyote yule unayemtumikia, ataweka alama sikioni mwako wala hutaweza kuisikia tena. Kama Mungu kamwe akinena na moyo wako kwamba "Njoo, huu ndio wakati," nawe ukatae, basi unapokea alama yake, umefanywa mgumu kutoka kwa Kweli. Hiyo hapo alama ya ibilisi, alama ya mnyama. Unaona? Alama ya mnyama hufanya nini? Inaenda na kukurudisha kwenye Urumi, umadhehebu, wala kamwe hutaingia na kuwekwa huru; utalitumikia hilo milele. Hiyo hapo alama ya mnyama.

302 Hilo ni gumu, enyi marafiki, hilo linakata, bali hivyo ndivyo ninii. . . Siwajibiki kwa ajili ya . . . ni yale tu Biblia isemayo.

303 Sasa, huo ulikuwa ni mfano katika Agano la Kale ambao ulionyesha awali kule kuisikia Injili ya habari njema kwamba "Uko huru!" Haikubidi kufungwa tena, uko huru kabisa katika Kristo Yesu. Hakuna dhambi tena na kadhalika. Huninii . . .

304 Ninyi mnaoupenda ulimwengu, Biblia ilisema, "Ukiipenda dunia au mambo ya dunia, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako." Hiyo ni kweli? Ukiipenda dunia au mambo yaliyo katika dunia, kumpenda Mungu hakumo ndani yako. Basi vipi kuhusu mambo haya yote makubwa yanayoendelea ulimwenguni leo hii chini ya jina la dini? Mambo ya ulimwengu! Nao watu wanayameza tu kwa pupa kama nguruwe katika kizimba chake, mnaona, "Loo, *hili* ni zuri. Hakuna kitu kuhusu *Hilo*!" Mnaona, wametiwa muhuri na kutiwa alama wakaondolewa. Mnaona?

305 Sasa mnaelewa masalia ya Wayahudi ni nini, wale mia moja na arobaini na nne elfu? Mahali wanapoketi, wanapongojea? Moja kwa moja katika saa hii. Mnaweza kuona sasa ya kwamba wale wanawali wapumbavu ambao hawatachukua ninii. . .wasingeyachukua Mafuta, nao itawabidi kufufuka na

kubaguliwa, mema na mabaya kwenye siku ya hukumu? Mnaelewa ya kwamba wakati yule—yule mwanawali mpumbavu alipoanza kupokea, kama tu sasa, kwamba alihitaji Haya, akayaendea; ndiyo dakika ile ile ambayo Bwana-arusi alikuja?

306 Basi tuko karibu jinsi gani? Sasa hivi! Tuko sasa katika wakati mfupi, sijui itakuwa muda gani zaidi. Nisingeweza kusema ni lini, si—sijui. Huenda ikawa ni mwaka mwingine, huenda ikawa ni miaka mingine kumi, miaka arobaini, huenda ikawa dakika arobaini. Si—sijui, siwezi kusema. Lakini ninajua iko karibu, iko karibu sana. Naye Roho wa Bwana . . .

307 Sasa, utakuja wakati ambapo, muda si muda mwajua, kanisa litaanza tu kuingia baridi. Sasa, ni watu wangapi ambao—ambao wamekuona kule kuingia baridi kwa kanisa katika miaka michache iliyopita? Hakika. Linaingia katika nini? Laodikia. Ambako, tutalichukua usiku wa leo na kumwelezea malaika wa kanisa la Laodikia, tulielezee waziwazi pale kusudi mpate kuliona, na muuone Ujumbe wake na jinsi utakavyokuwa, na katika mwisho wa Wakati wa Kanisa la Laodikia wakati linapoingiana na kuenea katika Umilele basi.

308 Loo, ninampenda tu. Nanyi je? Naam, bwana. Loo, ninii . . . Ni nini—ni nini Muhuri wa Mungu? Roho Mtakatifu. Alama ya mnyama ni nini? Kumkataa. Hizo ndizo zile mbili. Moja ni kuona, na . . .

309 Vema, wao ni . . . Na ni wangapi waliokuwa duniani ambao hawakumpata? "Wote ambao hawakutiwa muhuri walitiwa alama ya mnyama." Wote, wasiokuwa na Roho wa Mungu, walikuwa na alama ya mnyama. Muhuri wa Mungu ni Roho Mtakatifu. Biblia ilisema hivyo. Kila mahali katika Maandiko pananena habari Zake, panasema Hiyo ndiyo alama ya Mungu, "muhuri wa Mungu." Na wote ambao hawakuwa Nao, ndio walioukataa. Nao waliukataa namna gani? Kwa kukataa kulisikia. Hiyo ni kweli?

310 Sasa kumbukeni, mnaipataje imani? "Kusikia." Alama ilitiwa wapi? Mkononi? La. Kichwani? La. Sikioni, mnaona. *Sikioni*, "kusikia." Ilifanya nini? Iliharibu kusikia. "Wala hapana tena," unasema, "silitaki Hilo tena. Sitaki uhusiano wowote Nalo. Sitaki uhusiano wowote na Hilo." Ni kama tu wao . . .

311 Ndugu Neville, ni—ni—nita—nitaliachilia hilo liendelee mpaka . . .

312 Nilitaka kuwaambia juu ya hilo "haiwezekani kwa hao waliokwisha kupewa nuru," mnaona, "kuingia—kuingia katika ule Ufalme," mnaona. Ni kama hao waaminio wakwamia mpakani:

> Tazameni, *haiwezekani kwa hao waliokwisha kupewa nuru . . . na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu,*

> . . . wakaonja nguvu *za zamani—zamani zijazo,*
>
> *Wakaanguka baada ya hayo, haiwezekani kuwafanya upya hata wakatubu; kwa kuwa* wangemsulibisha *Mwana wa Mungu* . . . na *kumfedhehi kwa dhahiri.*
>
> *na* . . . kuhesabu *damu ya agano aliyotakaswa* kwayo *kuwa ni kitu ovyo* . . .

313 Mnaona, kwa Wateule kufanya hivyo, haiwezekani kabisa, hata kidogo. Asingeweza kufanya hivyo, mnaona. Kwa sababu yeye angefanya nini? Mnaona? "Lakini kuihesabu ile Damu ya Agano . . . " Sasa, mnaona, kama yeye ni mteule na yuko katika kundi hilo, hawezi kufanya hivyo. Haiwezekani kwake kulifanya.

314 Sasa, tumelichukua, tukalitoboa moja kwa moja:

> . . . maana *mvua* . . . *inayoinyeshea* nchi, kuzaa mboga . . .
>
> . . . na *miiba na* michongoma ambayo . . . *hukataliwa; ambayo mwisho wake ni kuteketezwa.* (Ngano itapelekwa Nyumbani kwenye Ghala.)

315 Lakini mvua hii inayotoa uhai huyanyeshea magugu pamoja na ngano. Yote mawili hushangilia na kujisikia vile vile kuihusu wakati ninii . . . yanafurahia kuona mvua ikija. Bali kwa matunda yao utawatambua, kama yana matunda yao ya gugu ama matunda ya nafaka (sasa, ya ngano).

316 Sasa, hii ndiyo njia ya kuifanya. Sasa kuonyesha ambapo hawa wakwamia mpakani, ambapo huyu . . . Ninajaribu kumleta *mwanamwali* huyu kwenu, mnaona, mpate—mpate kuelewa. Sasa katika mwaminio mkwamia mpakani, angalieni lililotukia wakati walipofikia Kadeshi-barnea, hao wana wa Israeli. Nililielezea huku na huku katika Mwanzo, na huku na huku katika Kutoka, na popote pale, nikijaribu kutoa mfano kwa ajili yenu, mnaona, ili kwamba hili darasa lisilikose.

317 Sasa, wakati watu hawa katika—katika hii . . . katika kule kutoka, walipofika Kadeshi-barnea. Kadeshi-barnea ilikuwa ndicho kiti cha hukumu cha ulimwengu, wakati huo. Hapo ndipo Israeli ilipopata kiti chake cha hukumu. Ambapo walikuwa ndiyo kwanza . . . Ilikuwa tu ni siku kumi na moja kutoka kwenye ule mlima ambapo walipokea zile amri mpaka wakafikia ile hukumu, "safari ya siku kumi na moja kwenye ufuko wa bahari," Biblia ilisema. Safari ya siku kumi na moja, ndipo wakafika Kadeshi na hapo wakahukumiwa. Ambapo Mungu angewavusha, katika yapata siku nne, walirudi moja kwa moja huku nyuma nyikani kule na kuzurura huko; wakapata zi—zile amri na kadhalika namna hiyo, kisha wakarudi, na jinsi, yale yaliyotukia. Ndipo wakaja huku . . . Na siku kumi na moja kutoka hapo, wakafika kwenye hukumu yao kule Kadeshi-barnea.

318 Ni kitu gani kilitukia? Yeye alichukua mmoja kutoka kwa kila kabila na kusema, "Nendeni mkaipeleleze nchi, mwone ni nchi ya jinsi gani." Vema, wote wakaenda kule na kuiangalia.

319 Wawili wao wakaingia na kukata kichala kikubwa mno cha zabibu. Loo, kichala kikubwa mno, ilihitajika watu wawili kukibeba.

320 Sasa, walifanya nini waliporudi na kuona ilikuwa ni nchi ya namna gani? Waliwaona Wa—Wa—Waamori na—na—wengine mbalimbali mle ndani, nao wakasema, "Mbona, hao ni majitu!" (Hao walikuwa, hakika, wana wa Kaini ambao hatimaye walifika kule kwenye—kwenye nchi hiyo.) Yeye akasema, "Hao ni—hao ni—hao ni majitu!" Kisha kasema, "Hatu—hatu—hatuwezi ku—kuichukua. Ardhi ya—ya—ya—yao imezungushiwa nyua, na kuta kubwa mno. Na, mbona, tunaonekana kama panzi, kando yao."

321 Walikuwa wamefanya nini? Mbona, walikuwa—walikuwa wameiona hiyo nchi kabisa. Wakaonja tunda lake. Mnaona, Kalebu na Yoshua walienda huko na ku—kupata ushahidi na kuuleta, walikuwa nao begani mwao. Walilionja tunda! Hiyo ni kweli. Kamwe hawakupata kuwa kule, bali Kalebu na Yoshua walienda kule, wakaleta ushahidi. Kalebu na Yoshua wakasema, "Tunaweza kuiteka!" Mnaona? Kwa nini? Kwa sababu Kalebu na Yoshua walikuwa wakiliangalia Neno.

322 Mungu alisema, "Nchi hiyo ni yenu. Yote imejaa Waamori na Wahivi na kila namna ya -kina nani kule, lakini," kasema "ni yenu. Na kila mahali miguu yenu inapokanyaga, nitawapa ninyi." Hiyo ni kweli. "Endeleeni tu kutembea, mnaona, ni yenu."

323 Bali hao wakasema, "Loo, la! Tusingeweza kuwa na uamsho kama huo. Loo! Loo, loo, mbona, mwajua nini? Askofu mkuu, ama askofu, ama viongozi, ama mtu fulani atashuka na kutufukuza sisi sote." Huh! Endelea, hiyo ni kweli, tutaipata.

324 Sasa, ndipo basi hawa wawili wakarudi kule na kusema, "Sisi tunaweza hata na zaidi kuiteka, kwa kuwa Mungu alisema hivyo! Hima twendeni tukaiteke!"

325 Lakini, mnaona, hawa waaminio wakwamia mpakani, walikuja umbali wa kutosha ku—kuionja Hiyo. "Ladha yake ni nzuri, naam. Lakini, loo, hatuwezi kuiteka."

326 Sasa, hiyo ni nini? Huyu hapa mwaminio siku hizi. Sasa, mwangalie jamaa huyu *papa* hapa. Mungu anampa wito. Uh-huh. Vema, sasa yeye anaokoka. Mama yake ni mfua nguo, naye anamtuma kwenye chuo fulani apate elimu yake ya jinsi ya kuhubiri. Vema, anatoka huko, angali anafikiri yeye . . . kila anapowaona wanawake waliovalia kizinifu, hilo linamfanya . . . linamvuruga; kila wakati a—anaposikia harufu ya sigara, kamwe hawezi kujizuia kuvuta moja. Anajua hilo ni kosa. Hataki

kufanya hivyo. Kwa hiyo akasema, "Bwana, nitakase, niondolee vitu hivyo."

327 Mungu alisema, "Vema, nitafanya hivyo kwa ajili yako, mwanangu, nikuondolee yote."

328 Usiku mmoja yeye anayumbayumba akaingia kwenye misheni ndogo mahali fulani, naye anausikia ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kasema, "Aisee!"

329 Ameifikia hatua ya kwanza, kuhesabiwa haki; akapanda kwenye hatua ya pili, utakaso; sasa yuko tayari kwa ajili ya Ubatizo. Mnaona: moja, mbili, tatu. Yuko tayari kwa ajili ya Ubatizo. Anapofikia pale juu, anasoma kwenye Biblia, akasema, "Hivyo ndivyo walivyofanya hasa. Naam, hivyo ndivyo hasa. Huo ubatizo katika Jina la Yesu, hivyo ndivyo walivyofanya. Hiyo ni kweli. Akasema 'isome hiyo tena,' niliisoma yote katika Biblia naye yuko sahihi kabisa juu ya Hilo."

"Askofu, ni nini wewe. . . "

"Sitaki chochote cha upuuzi huo!"

"Loo, kumbe."

330 "Walimpokea Roho Mtakatifu, wakanena kwa lugha, wakafanya mambo haya, wakawaponya wagonjwa. Loo, naam, hiyo ni kweli kabisa." Alikuwa akiangalia, mnaona, akiangalia mpakani.

331 "Loo, kama ningelifundisha Hilo kanisa langu. . .Loo! Mimi ni Mpresbiteri, Methodisti, Bapt-. . .mwajua. Loo, askofu atanitupa nje. Vema, kamwe hatuwezi kufanya hivyo. Hatuwezi kuwa na mkutano kama huo kanisani mwetu, kila mmoja wao angeamka na kuondoka."

332 "Yeye aliyekwisha kupewa nuru, na ameonja Karama za mbinguni, akaanguka tena kutoka kwenye njia aliyochukua, kurudi akajifanye upya tena katika toba kwa sababu amefanya dhambi dhidi ya Mungu. . . " Dhambi ni—ni nini? Kutokuamini! Ametenda dhambi dhidi ya Mungu. Naye amefanya nini? Amehesabu Agano, ambamo alitakasiwa, kana kwamba lilikuwa ni kitu ovyo, na kuifedhehi kazi za neema zilizompandisha kule juu. Haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi kwake, bali kuna kuitazamia hukumu yenye kutisha, na hasira iliyo tayari kuwala wao wapingao. "Kwa kuwa kupatiliza kisasi ni kwangu Mimi," asema Bwana.

333 "Kwa kuwa Neno la Mungu ni kali, tena lina nguvu kuliko upanga ukatao kuwili, ukikata hata kuugawanya mfupa, na huyatambua mawazo na makusudi ya nia." Haya basi, haya basi. Unapoiona Nuru, tembea ndani Yake! Tembea! Hujui uendako, bali endelea kutembea. Kutembea ukielekea Kalvari, ukiitazama Kalvari kwa akili timamu. Tembea! Tembea!

334 Ee Mungu, jalia siku moja. . .Kanisa, ambalo ni mfano wa Henoko. Miaka mia tano yeye alitembea pamoja na

Mungu. Kutembea! Kutembea Nuruni, akiwa na ushuhuda ya kwamba "Kila kitu alichosema Mungu, yeye alikitimiza." Yeye hakumkasirisha. Yale Bwana alisema yatendwe, Henoko aliyatenda. Sasa, yeye alikuwa ni mfano, kumbukeni. Safina ni mfano wa Wayahudi, wale mia na arobaini na nne elfu waliobebwa, ambao ni Nuhu na kundi lake; bali Henoko alienda Nyumbani muda kidogo tu kabla ya ile gharika. Mnajua hilo. Kwa hiyo Henoko aliendelea tu kutembea Nuruni. Kwa hiyo siku moja aliihisi miguu yake ikiondoka ardhini, akaendelea tu kutembea, ndipo akatembea akaingia Utukufuni pasipo hata kufa. Hiyo ni kweli. Mungu alimchukua kwa sababu alikuwa akitembea katika Nuru, akiwa na ushuhuda ya kwamba "yeye alitembea katika Nuru ya Mungu." Akaendelea kutembea, kutembea.

335 Hebu tuvae viatu vyetu vya kutembea, enyi Kanisa:

> Tuendelee kutembea Nuruni, Nuru nzuri,
> Huja ambapo matone ya umande wa rehema yanang'aa;
> Tuangazie kote mchana na usiku,
> Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Hebu tuuimbe sasa:

> Tutatembea Nuruni, Nuru nzuri,
> Loo, njoo ambapo matone ya umande wa rehema yanang'aa;
> Tuangazie kote mchana na usiku,
> Yesu, Nuru ya ulimwengu.
>
> Enyi watakatifu wote wa Nuru tangazeni,
> Yesu, Nuru ya ulimwengu;
> Ndipo kengele za Mbinguni zitalia,
> Yesu, Nuru ya ulimwengu.
>
> Tutatembea Nuruni, Nuru nzuri sana,
> Loo, njoo ambapo matone ya umande wa neema yanang'aa;
> Tuangazie kote mchana na usiku,
> Loo, Yesu, Nuru ya ulimwengu.

336 Na tuviinamishe vichwa vyetu, na kwa mu—muda kidogo tu. Sijui kama kuna wengine humu ndani wangetaka kuwa na ujuzi wa kujazwa na Roho Mtakatifu, semeni, "Nikumbuke, Ndugu Branham. Nikumbukeni, enyi kanisa. Ninataka kutembea katika Nuru. Ninataka utamu huo, pasipo na shina la uchungu ndani yangu, ninataka kuwa tu mtumishi wa Mungu." Inua mkono wako, ukisema, "Nikumbuke, Ee Bwana." Naam, mikono ishirini ama zaidi, imeinuliwa.

337 Sasa endeleeni tu kuinamisha vichwa vyenu wakati tukiimba pole pole pamoja:

Ee Yesu, Nuru ya ulimwengu.
Tutatembea katika Nuru hii, ni Nuru nzuri sana,
Huja ambapo matone ya umande wa rehema yangang'aa;
Tuangazie kote mchana na usiku,
Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Njoni, enyi watakatifu wote wa Nuru, tangazeni,
Ee Yesu, Yeye ni Nuru ya ulimwengu;
Ndipo kengele za Mbinguni zitalia,
Ee Yesu, Yeye ni Nuru ya ulimwengu.

Loo, tutatembea katika Nuru hii, ni Nuru nzuri sana,
Inakuja ambapo matone ya umande wa rehema yanang'aa;
Tuangazie kote mchana na usiku,
Ee Yesu, Nuru ya ulimwengu.

338 [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Yesu, Nuru Ya Ulimwengu*—Mh.] Bwana Yesu, wakati wakiuvumisha wimbo huu, wakitaka kutembea katika Nuru ya Injili, ichukue mioyo hiyo ya thamani, Bwana. Wao ni Wako, wasafishe, ondoa uovu wote, ondoa kutokuamini, jalia Yesu Nuru ya ulimwengu aingie ndani. Leso zimewekwa hapa, Bwana, kwa ajili ya wagonjwa na wanaoteseka. Njoo kwao, Bwana Yesu, kawaponye wapate kutembea katika Nuru. Tujalie, Bwana.

339 Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya somo letu, kwa ajili ya Uwepo wa Roho Mtakatifu, amekuwa hapa pamoja nasi na kutuweka, saa kadhaa, tukiketi hapa. Watu wakiketi kwenye chumba hiki chenye joto, wakingojea. Wanatarajia na kungojea na kushangaa, Bwana. Kwa kuwa wanatambua, wakati wakilisikia Neno likisomwa, kwamba tuko katika wakati wa mwisho. Hakuna kilichosalia, ni mizaha tu ya ulimwengu. Na moja ya siku hizi huo uigaji itabidi ukome.

340 Nami ninaomba, Mungu, ya kwamba Wewe utamwokoa kila mtu aliye kwenye Uwepo wa Kiungu, waokoe kwa Roho Wako. Pia jalia Roho Mtakatifu ashuke juu ya kila mmoja wao na kuijaza mioyo yao kwa wema, na amani, wapate kuzaa tunda la Roho, ambalo ni, uvumilivu, upole, amani, saburi, unyenyekevu, imani, katika Roho Mtakatifu. Tujalie, Bwana. Nitawakabidhi Kwako sasa kwa ajili ya utumishi Wako, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana Wako. Amina.

Tutatembea Nuruni, . . .(Na tuinue mikono yetu tunapoimba.) . . . Nuru nzuri,
Huja ambapo matone ya umande wa rehema unang'aa;

Tuangazie kote mchana na usiku,
Ee Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

341 Loo, hivi Yeye si ni wa ajabu? Tutakuwa na ibada ya ubatizo kwa yapata dakika kumi sasa, kumi na tano, wowote ule. Kuna . . . Nafikiri kuna msichana hapa anayepaswa kubatizwa. Hiyo ni kweli? [Ndugu Neville anasema, "Wapo wengi."—Mh.] Vema, ni wangapi wanaopaswa kubatizwa asubuhi ya leo wasioweza kurudi usiku kwa ajili ya ibada ya ubatizo jioni ya leo? Moja, mbili, tatu, watatu wasioweza kuja alasiri ya leo ama kabla ya ibada ya jioni kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Mungu awabariki, enyi watoto. Nina furaha ya kwamba Mungu ameweka mbele zenu Mlango uliofunguliwa. Nanyi mko tayari kuingia sasa, mnaingia kaburini, ili kwamba mambo yote ya kale yamekufa na kuzikwa. Sasa, kumbukeni, ubatizo wenu ni onyesho la nje tu ya kwamba jambo fulani limetukia *hapa* chini.

Halafu tutatembea katika Nuru hii, (wanajiandaa) Nuru nzuri,
Loo, tuangazie kote usiku na mchana,
Ee Yesu, Nuru ya ulimwengu.

342 Loo, ushirika huu mkuu! Hivi hamjisikii vizuri? Loo, ninajisikia tu vizuri sana. Inaonekana kama ni kitu nimekuwa nacho, moja ya hizi brashi za kusugulia za mtindo wa kale, nawe unisugue tu kabisa kwa sabuni ya magadi.

343 Ndugu yangu alisema labda ninyi nyote mnaotaka kubatizwa asubuhi ya leo, jitayarisheni. Suti na kadhalika zitakuwa zimelowa maji usiku wa leo, bali ni sawa kama mkitaka kufanya hivyo. Lakini kama uko tayari kubatizwa asubuhi ya leo, sawa.

344 Ninaamini itatubidi kuondosha hiki, sivyo, Ndugu Neville? Vema, bwana. Sasa, ni wangapi wanaotaka kukaa na kuona ubatizo? Chukueni tu dakika chache na, jamani, labda hamjawahi kuona mmoja ukiendelea. Endapo huwezi kukaa, vema, basi wewe hakikisha utarudi usiku wa leo. Lakini laiti ungaliweza, na kukaa dakika chache kuiona ibada ya ubatizo. Tutakiondoa hiki na kuna kioo kikubwa nyuma hapa kinachoonyesha kila mtu anayeingia ndani. Litakuwa ni jambo la kushangaza kwako, nina hakika. Tunazikwa pamoja na Bwana katika ubatizo. Amina. Wakati akifa, tunazikwa katika mauti Yake; tukafufuliwa katika kufufuka Kwake, tupate kutembea katika upya wa maisha. Bwana awabariki.

345 Ni wangapi wanaojua somo la usiku wa leo ni lipi? Laodikia, wa mwisho, na upeo wa Nyakati za Kanisa.

346 Vema, tutakuwa na ibada ya ubatizo. Teddy, kama utaweza . . .

347 Unataka kuba-. . .? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . tayari umebatizwa. Kuna baadhi yao hawana budi kuondoka kwenda Chicago sasa hivi, mnaona.

Na tuombe:

348 Bwana Yesu, wameketi na kuisikiliza ibada yote. Tunawakabidhi Kwako sasa, Bwana, wanapokwenda Chicago. Nenda pamoja nao, Bwana, na jalia kila mmoja wao aichukue Nuru hii nzuri sana na kuitawanya, Bwana, kote katika jiji la Chicago, kila waendako. Kuwa pamoja nao. Hata tutakapokutana, jalia roho zao zitiwe nanga ndani Yako. Katika Jina la Yesu. Amina.

349 [Ndugu Neville anatabiri—Mh.] Hebu tuinue mikono yetu na kusema, "Asante, Bwana Yesu, Jina Lako lisifiwe." Asante, Bwana. Tunatambua hilo, Bwana, ya kwamba Wewe . . . siku moja Roho alishuka juu ya mtu mmoja, katika Biblia, na kusema siri zote za Mungu, yale yangetukia. Baba, tunajua kwamba Wewe ungali Mungu yeye yule. Na hapa umeshuka juu ya maskini mchungaji huyu mnyenyekevu hapa, Bwana, asubuhi ya leo, ambaye wakati mmoja alikuwa huko nyuma katika Unikolai; bali Wewe ukamtikisa; akaiona Nuru na kutoka. Na hapa moyo wake umefunguliwa sana hata Wewe utazungumza naye, mpaka hata hajui yale atakayosema, na kusimama na kumwacha Roho Mtakatifu atende kazi kupitia kwake katika sauti ya unabii kwetu. Asante, Baba. Nami ni—nitakutazamia kwa ajili ya ratiba zangu. Amina.

350 [Dada mmoja ananena katika lugha nyingine. Sehemu tupu kwenye kanda. Dada mwingine anatoa tafsiri—Mh.] Amina. Mlipata hilo, sivyo? Mnaona hiyo ilikuwa ni nini? Angalieni toni ya sauti ya mwanamke huyo mmoja akinena, kisha mwangalie fasiri ikirudi katika toni iyo hiyo. Mnaona? Hao hapo wanawake wawili mbalimbali, nina shaka kama hata wanafahamiana ama la. Ha—hawafahamiani. Huyo hapo Roho Mtakatifu, angalieni tuni ya sauti namna hiyo. Hivi hamtambui ya kwamba huyo ni Kristo miongoni mwa watu hapa? Hiyo ni kweli.

351 Una kitu unachotaka kusoma, Ndugu Pat? Endelea, unaona. [Ndugu Pat anasema, "22:16 ya Ufunuo ninasoma katika Jina la Bwana Yesu: Mimi Yesu nimemtuma malaika wangu kuwashuhudia mambo haya katika makanisa."—Mh.] Amina.

352 Sasa, huo ni uongozi wa kiroho, wa Kiungu. Mnaona, Roho Mtakatifu akitenda kazi kupitia kwa walei, akitoka huko nje, akinena. Loo, Yeye si ni wa ajabu? Kuwazia, enyi marafiki, hilo ni jambo lile lile lililonenwa na Biblia. Nalo liko hapa leo hii, haitulazimu kushangaa juu yake tena. Loo, njoni mkampokee, watu wangu wa thamani. Njoni, mkampokee.

353 Teddy, tunapojitayarisha kwa ajili ya ubatizo, (nami ninaomba Mungu ataiweka tayari mioyo yenu) *Aniongozapo Nitafuata*.

354 Naweza kuwasaidia hapa ndugu zangu? Vema, inawabidi—inawabidi kuvizima hivyo vipazasauti. Uh-hum. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

355 Ninawaapisha kwa Mungu aliye Hai na kwa ushawishi wa Neno Lake kwamba mje mkabatizwe katika jina la Yesu Kristo. Kumbukeni ninafanya hivyo kwa sababu Biblia inatushurutisha kufanya hivyo. Na—naye Paulo alisema tufanye hivyo; na kama malaika akifundisha lingine lolote, na alaaniwe. Nami na—nataka tu kutangaza hili mwishoni mwa safari yangu kama yeye alivyofanya: sijaacha kuwatangazia maagizo yote ya Mungu kama niyajuavyo, vivyo hivyo hasa. Hakuna damu ya mtu yeyote juu yetu.

356 Loo, hivi hamumpendi? Loo, jinsi ninavyompenda. Vema, hebu tusimame tunapoimba wimbo wetu wa kupumukana. Vema, mpaka wakati huo tuta-:

Peleka jina la Yesu,
Mwana wa huzuni na majuto.
Litakupa furaha na faraja,
Peleka kila uendako.

Jina la thamani (Jina la thamani), Ee jinsi lilivyo tam- . . . (Loo jinsi lilivyo tamu),
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.
Jina la thamani (Jina la thamani), Ee jinsi lilivyo tam- . . . (Loo jinsi lilivyo tamu),
Tumaini la duniani na furaha ya . . .

Sasa tunapoviinamisha vichwa vyetu tunaimba:

Tukiliinamia jina la Yesu,
Tukisujudu miguuni Pake,
Tutamvika taji Mbinguni kama Mfalme wa wafalme,
Safari yetu itakapokamilika . . .

Wale Wanawali Kumi, Na Wayahudi
Mia Na Arobaini Na Nne Elfu SWA60-1211M
(The Ten Virgins, And The Hundred And Forty-Four Thousand Jews)
Mfululizo wa Ufunuo Wa Yesu Kristo

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili asubuhi, tarehe 11 Desemba, 1960, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org